

UCHANGANUZI WA UWASILISHAJI WA KIFO KATIKA MASHAIRI TEULE YA
KISWAHILI

NA

ORINDA FREDRICK ODONGO

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KAMA SEHEMU YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA
KISWAHILI

KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI YA JAMII

CHUO KIKUU CHA MASENO

KENYA

© 2014

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya shahada katika chuo kikuu kinginecho. Sehemu yoyote hairuhusiwi kunakiliwa bila ya idhini ya mwandishi na/au Chuo Kikuu cha Maseno.

Orinda Fredrick Odongo

Tarehe

PG/MA/014/2010

Tasnifu hii imetolewa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Maseno.

Prof. Indede Florence

Tarehe

Idara ya Kiswahili na

Lugha nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Maseno

Prof. Mohochi Ernest

Tarehe

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu Kishiriki cha Rongo

SHUKRANI

Utafiti huu haungekamilika bila misaada ya watu wengi walionipa himizo na mwongozo katika kila awamu ya kutekeleza utafiti wenyewe. Shukrani zangu nyingi nazitoa kwa Chuo Kikuu cha Maseno kwa kunisajili kama mwanafunzi kusomea uzamili na pia kunifadhili pakubwa. Pili, nawashukuru wasimamizi wangu, Dkt. Florence N. Indede na Dkt. Mohochi Ernest ambao mwongozo wao ulinifaa kwa kila hali ili kuibuka na kazi kamilifu ya utafiti huu. Bila ya himizo na maelekezo yao singeweza kukamilisha utafiti huu. Usimamizi wao ulikuwa wa manufaa makubwa na Mungu azidi kuwapa nguvu na hekima katika kazi zao. Wahadhiri wangu wengine walionipa maelekezo ni pamoja na Bi. Amukowa, Bi. Asiko na Bw. Lumwamu. Nawashukuru sana kwa kunisaidia kulihali.

Tatu, nawashukuru wazazi wangu ambao walijitolea sabili kunisomesha ili nipate mafao maishani. Shukrani ziwaendee; mamangu Ludovica Were na babangu James Orinda ambao wote walihakikisha kuwa sikukosa chochote nilichohitaji wakati wa kutekeleza utafiti huu. Pia nawashukuru ndugu zangu wote ambao walinivumilia wakati huu wa utafiti.

Nne, nawashukuru marafiki zangu walionipa moyo mbele ya magumu wakati wa utafiti huu. Wema wenu ulikuwa na umuhimu mkubwa kwangu na Mungu awabariki nyote. Marafiki zangu wa karibu Suleiman Mwakwina, Jefwa Yaa, Jack Yongo, Salim Mwatengar, Arthur Oyugi, Obunga Odieny na Eunice Anyango mionganoni mwa wengine nawashukuru sana kwa udugu na uvumilivu wenu.

Mwisho nawashukuru wapiga taipu wa kazi hii ambao bila ya kuipiga taipu isingepata kuchapishwa na kuwa na sura iliyo nayo leo.

Kwa yote haya namshukuru Mungu kwa kunipa siha na kumbukizi nzuri wakati wa utafiti huu.

TABARUKU

Kwa mamangu mpendwa. Kiu yangu ya Kiswahili umeipa dawa mwafaka kwa jitihada pevu ya
kujitlea kufa kupona ili kunipa elimu na nasaha bora.

IKISIRI

Kifo ni swala zito na linaloibua hisia zaidi. Uwasilishaji wa dhana ya kifo katika tanzu anuwai za fasihi huwa kwa namna tofauti. Katika ushairi kifo huibuliwa kwa lugha ya pekee yenye mnato wa hisia na mashiko zaidi. Ushairi hutumia lugha ya mkato na mapigo ya sauti yanayovutia na kunata pindi yanapowasilihwa kupitia kughani, usomaji na ukariri. Uchambuzi mwangi wa dhana ya kifo katika ushairi wa Kiswahili uliwahi kufanywa katika ushairi mbolezi amba ni wa kisimulizi lakini swala hili katika ushairi andishi hutajwa tu kwa ufinyu wala haushughulikiwi kwa kina. Utafiti huu ulichambua uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Uchambuzi huu ulifanywa kwa malengo ya; kutambua na kueleza taswira ya kifo; kubainisha visababishi vya kifo; na kuchunguza utata unaojitokeza katika ufanuzi wa dhana ya kifo kama wanavyodhiihirisha wasanii katika mashairi teule ya Kiswahili. Malengo haya yalifikasiwa kwa kuzingatia mashairi matatu teule; *Inkishafi, Mwana Kupona* na ‘Usiniwe’ katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia kama ilivyofafanuliwa na Georg Lukacs (1938). Mihimili ya nadharia hii iliyyotumika ni pamoja na tajriba ya mwandishi, historia ya jamii, muundo wa kazi, vielelezo na lugha. Utafiti ulikuwa wa kimaktaba. Mtafiti aliteua matini tatu za ushairi wa Kiswahili na kujikita maktabani na kuzichambua kwa kina huku akirejelea malengo ya utafiti. Uteuzi ulifanywa kimaksudi kwa kuzingatia usawirishaji wa dhana ya kifo. Muundo wa uwasilishaji data ulikuwa wa kimaelezo. Kupitia mihimili ya nadharia ya uhalisia, utafiti huu ulibaini kuwa; taswira ya kifo kulingana na mashairi teule ni pamoja na dhoruba ya kifo, kifo kinatamausha, uchungu wa mauti, kifo ni hatima ya kila kiumbe, kifo kina upweke, kifo si mwisho wa maisha na kifo kina ukatili. Usawiri wa kifo pia hujikita katika mazingira ya mtunzi ambayo hujitokeza katika vipengee vya wakati, dini au utamaduni na lugha. Aidha, kifo ni kitu kilicho na chanzo chake ikiwa ni Mungu, shetani na mtu. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa hakuna mpaka bayana baina ya kifo na uhai hivyo mwanadamu anajikuta katika mkanganyiko wa kuishi huru duniani kwa hofu ya yatakayompata akhera. Utata huu hujitokeza katika kuelewa mwanzo na mwisho wa maisha, maisha baada ya kifo na uwezo wa kuzungumza na Mungu katika ufu. Utafiti huu ulihitimisha kuwa kifo ni hatima ya kila kiumbe na ni vema mwanadamu kukikubali na kuwa radhi nacho kwani huletwa na nguvu za kimaumbile nje ya uwezo wake. Akiishi mwanadamu, huwa yu mbioni akingoja kifo na ahera kwa kutegemea alivyoishi duniani. Ni mapendekezo ya utafiti huu kuwa kifo ni kiungo cha maisha kinachofanya uhai kuthaminiwa zaidi. Uwepo wa kifo hupatia maisha maana na ukosefu wake huyafanya kukosa kufasiriwa. Kutohana na utata wa dhana ya kifo, ni muhimu utafiti zaidi ufanyike kwa kuzingatia dhana ya uhai ili kuweka mwangaza zaidi kuhusu mpaka baina ya kifo na uhai na chanzo cha kifo; na utafiti linganishi ufanywe ili kubainisha taswira ya kifo katika tanzu nyinginezo za fasihi.

ABSTRACT

Death is a very heavy and an emotional subject. Depiction of death in various genre of literature is vast and varied. In poetry, death is depicted in a unique language which draws attention and touches the feelings of the audience. Poetry uses short form of language and rhythmic pattern which attracts and holds the attention of the audience during performance through singing, reading and recitation. Several studies on the aspect of death in Swahili poetry have been on dirges while in written poetry this aspect is being mentioned briefly in several analyses. This study analysed depiction of death in the selected Swahili poetry. The specific objectives of this research were: to explain the image of death; to explain the causes of death; and to investigate the ambiguities which occur in the explanation of death as depicted by artists in the selected Swahili poetry. These objectives were achieved by analyzing three selected poems; *Inkishafi*, *Mwana Kupona* and ‘Usiniuwe’ from *Sauti ya Dhiki*. This research was guided by the theory of realism as expounded by Georg Lukacs (1938). The tenets of this theory that were used include author’s experience, societal history, models, language and form. This research was library based. The researcher selected three poems which were analysed in line with the objective of the research. Purposive sampling was employed in selecting the poems of research by looking at depiction of death. This research adopted an analytical approach. Through the tenets of theory of realism, this research conclude that the image of death in line with the selected poems includes death’s blow, death brings hopelessness, death is painful, death as the end of every soul, death as the equalizer, death as loneliness, death is not the end of life and death is brutal. Depiction of image of death was also realized based on the environment which encompasses time, religion or tradition and language. Death, however, has its causes like God, devil and human being. There is no clear gap between death and life thus making man to live in fear anticipating what lurks in the hereafter. This ambiguity is depicted in the understanding of the beginning and the end of life, life after death and the ability to talk to God in death. This research concluded death is an end to every soul and is better for human being to accept it because it is brought by extra forces beyond human ability. Human being lives waiting for death hoping for heaven based on how he lived here on earth. This research recommends that death is apart of life which makes it meaningful and valuable. The presence of death gives meaning to life and vice versa. Due to this ambiguity of death, there should be critical examination on the aspect of life in order to realize a clear boundary between life and death and origin of death; and comparative research should be conducted on image of death in other genre of literature.

YALIYOMO

MADA

KURASA

IKIRARI	ii
SHUKRANI.....	iii
TABARUKU.....	iv
IKISIRI	v
YALIYOMO	vii
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI.....	1
1.1 Usuli wa utafiti.....	1
1.2 Suala la utafiti	5
1.3 Maswali ya utafiti	5
1.4 Madhumuni ya utafiti.....	6
1.5 Upeo wa utafiti.....	6
1.7 Umuhimu wa utafiti	8
1.8 Nadharia ya utafiti.....	9
SURA YA PILI.....	17
MAPITIO YA MAANDISHI.....	17
2.1 Utangulizi.....	17
2.2 Historia fupi ya Ushairi wa Kiswahili	17
2.3 Dhana ya kifo.....	19
2.4 Chanzo cha kifo na ukubalifu wake.....	23
2.5 Ukweli wa uwepo wa kifo na hatima ya maisha.....	27
2.6 Mjadala wa kifo katika fasihi ya Kiswahili	30
2.7 Hitimisho.....	36
SURA YA TATU	37
NJIA NA MBINU ZA UTAFITI	37
3.1 Muundo wa utafiti.....	37
3.2 Njia ya utafiti	37
3.3 Kikundi Lengwa.....	38
3.4 Uteuzi wa sampuli.....	38
3.5 Mbinu za ukusanyaji wa data.....	39
3.6 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data	39
SURA YA NNE	41

MAWANDA YA KIFO KATIKA MASHAIRI TEULE YA KISWAHILI.....	41
4.1 Utangulizi.....	41
4.2 Diwani teule za ushairi wa Kiswahili	43
4.2.1 Inkishafi	43
4.2.2 Utenzi wa Mwana Kupona.....	45
4.2.3 Sauti ya Dhiki	47
4.3 Taswira ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili	49
4.3.1 Dhoruba ya kifo	51
4.3.2 Kifo kinatamausha	54
4.3.3 Uchungu wa mauti	58
4.3.4 Kifo ni hatima ya kila kiumbe	61
4.3.5 Upweke wa kifo	64
4.3.6 Kifo si mwisho wa maisha.....	68
4.3.7 Ukatili wa mauti.....	71
4.4 Mazingira katika usawiri wa kifo	73
4.4.1 Wakati	74
4.4.2 Dini au utamaduni.....	81
4.4.3 Lughna na mauti	90
4.5 Visababishi vya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili	93
4.5.1 Mungu	94
4.5.2 Shetani.....	98
4.5.3 Mtu kwa mtu	100
4.6 Utata wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili	105
4.6.1 Adhabu na kuzawadiwa peponi	106
4.6.2 Mazungumzo na Mungu	109
4.6.3 Utabaka	111
4.6.4 Mwanzo na mwisho wa maisha	115
4.6.6 Hitimisho.....	117
SURA YA TANO.....	119
HITIMISHO.....	119
5.1 Muhtasari wa tasnifu.....	119
5.2 Taamuli.....	122
5.3 Mapendekezo ya Utafiti.....	124

5.4 Hitimisho.....	125
MAREJELEO	126

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

Katika sura hii tumetoa ufanuzi kuhusu usuli na msingi wa mada ya utafiti. Tumeorodhesha maswali yaliyoongoza utafiti huu na pia tumeonyesha malengo na madhumuni ya utafiti huu. Vilevile tumeonyesha upeo na umuhimu wa utafiti kisha tukajadili nadharia iliyotumika kuongoza utafiti huu.

1.1 Usuli wa utafiti

Kwa kipindi kirefu swala la kifo katika ushairi simulizi uliwahi kushughulikiwa na watafiti mbalimbali katika jamii tofautitofauti za Kiafrika. Ushairi simulizi hudhihirisha pakubwa swala la kifo katika kipera chake cha ushairi mbolezi. Ushairi simulizi huwa na mazingira hai kutokana na uhusiano unaokuwepo baina ya msimulizi na hadhira yake. Ushairi simulizi ni milki ya jamii nzima na mtazamo unaoibuka huwa ni wa jamii kwa ujumla kama wanavyodai Miruka (1994) na Alembi (2001). Hali hii ni tofauti na ushairi andishi ambapo mawazo ya mtu binafsi au falsafa yake hujitokeza kama mali yake, (Wamitila 2001). Licha ya swala la kifo kujitokeza katika ushairi andishi, halijajadiliwa kwa kina na wataalamu wa ushairi wa Kiswahili. Ni wataalamu wachache sana ambao wamewahi kulishughulikia swala la kifo katika ushairi andishi huku wakijikita katika utungo mmoja pekee. Wataalamu kama vile Hichens (1972) na Mlamali (1980) wamewahi kuchunguza dhana ya kifo katika utenzi wa *Inkishafi*. Walakini walizingatia pakubwa falsafa ya mtunzi wa utenzi huu katika kuasa moyo wake kuhusu kifo huku wakijadili zaidi swala la ufupi wa maisha na mapito ya wakati wa mwanadamu humu duniani. Halikadhalika

wamejaribu kuangazia upeo wa juu wa lugha uliotumika katika utungo huu wa *Inkishafî*. Mlamali kwa mfano amejikita zaidi katika lugha ya *Inkishafî*, kulinganisha utenzi huu na tenzi nyinginezo na pia kuichukua kama mawaidha ya wale wanaopita mpaka kwa kutenda yasiyofaa wanapoishi duniani. Utafiti huu nao ulijikita tu katika kuangazia dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili ili kuonyesha uhalisia wake kisanaa na kimaisha.

Massamba (1983) anaeleza kuwa kwa kawaida mshairi anapotunga shairi hutoa hisia au maoni yake juu ya jambo fulani. Maoni hayo hutolewa kufuatana na jinsi anavyoliona jambo lile. Hii ina maana kwamba maoni yake hutolewa kulingana na imani yake binafsi. Mshairi kama mwanadamu yejote awaye, huwa na imani fulani kuhusu mambo mbalimbali yanayomzingira. Lakini jambo muhimu ni kwamba imani yake kuhusu tukio, hali au kadhia fulani si lazima iwe sawa na imani ya mtu mwingine. Imani hii ya mshairi ndiyo ijengayo msimamo wake kuhusu dhana mbalimbali katika maisha.

Wanamapokeo kama vile Mayoka (1984) walishikilia kuwa usawiri wa maudhui katika fani ya ushairi huandamana na muundo au umbo la shairi. Anaeleza kuwa uteuzi wa vina na mizani kwa ukwasi mkubwa hujenga vyema maudhui katika shairi. Hii ni kwa sababu vina hivyo pamoja na mizani huleta mrindimo fulani kusawiana na mada inayozungumziwa. Kwa hali hii hisia zilizokusudiwa na mtunzi hujitokeza waziwazi na makini ya hadhira kushikwa na kudhibitiwa pindi shairi linaposomwa au linapoghaniwa au kukaririwa. Waaidha, ili mtunzi apate kuibuka na mizani na vina vinavyofaa ni lazima awe mzoefu wa lugha yake ndiposa aweze kuteua misamiati mwafaka ili kujenga na kuwasilisha ujumbe wake kikamilifu. Mawazo haya yanashadidiwa na wengi wa washairi jadi kama vile Abedi (1954), Mnyampala (1965), Chiraghdin (1977), Abdalla

(1979), Ruo (1988) na Wallah (1988). Mtazamo wa wanamapokeo hushadidiwa na Bashir (1972) anayepiga hatua mbele zaidi kwa kueleza kuwa maandishi fasaha na matumizi matamu ya maneno ya fikra hupatikana kwa wingi katika tenzi na mashairi. Utafiti huu uligundua kuwa vipengee vya vina na mizani bado ni muhimu katika kusawiri mada ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

Usawiri wa dhana ya kifo katika tanzu nyingine za fasihi hujadiliwa chini ya tanzia. Tanzia ni msiba ambao humkumba mhusika mkuu katika riwaya au tamthilia. Kwa mujibu wa Indangasi (1992) mhusika huyu mkuu wa tamthilia au riwaya huwa na mahasidi ambao daima humtafutia maovu ya kumwangamiza. Lengo la maadui hawa ni kumshinda mhusika mkuu. Mhusika huyu hatimaye hufa na hapa ndio upeo au kilele cha tungo za kitanzia. Utokeaji wa kifo katika ushairi nao ni tofauti kwani si kitu kinachomkumba mhusika fulani bali hutokea kama mada inayojadiliwa na mtunzi wa kazi husika. Ushairi huwa na muundo wa kipekee unaotumika wakati wa kuwasilisha mada mbalimbali.

Kifo ni tukio ambalo limewashughulisha wataalamu wengi hususan wanafalsafa na wale wa dini. Hii ni kwa sababu japo kifo ni tukio la kawaida na lazima kumkumba kila mwanadamu, kuna utata wa kuelewa chanzo na hatima yake kwani fasiri zake ni nyingi na hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine na pia mtu mmoja hadi mwengine. Utata huu huzuliwa na mazingira tofauti, mila na itikadi zisizofanana pamoja na mabadiliko ya kiwakati. Wataalamu mbalimbali hutoa fasiri ya dhana ya kifo kwa njia nyingi na tofauti.

Neno *kifo* ni nomino. *Kifo* hutokana na kitenzi ~*fa*. Kamusi ya *The Oxford English Dictionary* (1989) inafafanua kifo kama tendo au uyakini wa kufariki; mwisho wa maisha; hatua ya mwisho wa kutoweka kwa ufanyakazi wa kimsingi wa viungo vya mwili wa mnyama ama miti. Kifo pia ni hali ya ufu; hali ama hatua ya kutokuwa na maisha ama kuteweza kutekeleza shughuli yoyote. Nayo kamusi ya *Macmillan English Dictionary* (2002) inafafanua kifo kama wakati ambapo kitu kinamalizika, kwa mfano, kifo cha utawala wa kibeberu kule Afrika Kusini. Kwa mujibu wa TUKI (2006), kitenzi ~*fa* humaanisha kufariki, kuaga dunia, kumalizika ama kuvunjika. Kwa hivyo nomino kifo humaanisha ufu au mauti.

Kifo hutazamwa kama maagano baina ya watu waliokuwa safarini. Aliyetangulia ni mfano wa mtu aliyeungana na wahenga katika safari nyingine tofauti na safari ya awali ambayo alikuwa hai na wenzake duniani. Mabadiliko maalum yajitokezayo ni kuoza kwa mwili lakini roho bado hubaki hai katika dunia nyingine kama anavyodai Carnley (1997). Kifo hapa huonekana kama kitu katili na kisicho na huruma kwa yejote hata yule mtoto mdogo ambaye hana hatia yoyote.

Kutokana na mawazo mbalimbali ya wataalamu kifo hujitokeza kama swala tata ambalo halieleweki bayana hata kupitia mbinu za utunzi, dini wala uchawi. Mwanadamu hujikuta akiwa katika mkanganyiko pindi anapokumbwa na kifo, kwa hivyo anabuni mbinu za kuwasilisha hisia zake kuhusiana na kifo. Ushairi humpa mkondo mwafaka wa kutoa hisia hizo kutokana na mbinu zake za kubana maneno, kuyakariri, kuyaghani na kuyaimba ngomani. Ushairi huwa na upekee wa uteuzi wa maneno yenye mrindimo na mkarara, maneno yanayoibua taswira na kunasa hisia kutokana na ufupi wa maelezo yake na uzito wa kauli zake. Kifo pia humtatiza mwanadamu na humtia kihoro kikubwa kwani hawezi kufasiri sababu zake, chanzo wala hatima yake kwa njia

inayofaa. Utafiti huu uliangazia taswira ya kifo, chanzo na utata unaoibuka katika usawiri wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

1.2 Suala la utafiti

Ingawa swala la kifo limewahi kushughulikiwa sana katika mbolezi ambayo ni mashairi ya kisimulizi, swala hili katika mashairi andishi hutajwa tu kwa ufinyu wala halijashughulikiwi kwa kina. Kifo mara nyingi hurejelewa kwa ujumla kama tukio la kimaumbile pasi na kueleza vipengee vyake anuwai. Kwa lengo la kuleta upana wa maelezo ili kuelewa dhana ya kifo, utafiti huu uliazimia kuchanganua uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Tulijikita katika kung'amua taswira ya kifo, visababishi na utata unaojitokeza katika fasiri ya dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Fasiri ya dhana ya kifo huwa changamano kwa sababu huibuliwa kisanaa kwa kutegemea msimamo wa mtunzi binafsi na jumuiya anayoiandikia. Mazingira ya mtunzi pia huwa na michango katika uwasilishaji wa kifo kwani mtunzi huwa hajengi kazi yake nje ya mazingira iliyomkuza. Mazingira hujitokeza kama mwangwi katika utunzi wa kisanaa kwani huibua uhalsia wa kiwakati na wa kisaaa. Hivyo basi utafiti huu ulijikita katika kulichanganua swala hili la kifo ili kuibua taswira na utata unaojitokeza na kuvielewa vipengele vinavyoliunda kwa undani, hususan katika mashairi teule ya Kiswahili.

1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo ambayo yaliwezesha kufikiwa kwa malengo yake:

- i) Kuna taswira zippi za kifo zinazowasilishwa katika mashairi teule ya Kiswahili?
- ii) Ni visababishi vipi vya kifo vinavyojitokeza katika mashairi teule ya Kiswahili?

- iii) Utata upi unaojitokeza katika ufanuzi wa dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili?

1.4 Madhumuni ya utafiti

Azma ya utafiti huu ni kuchunguza uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Ili kufanikisha lengo hili kuu, malengo haya mahususi yalizingatiwa:

- i) Kuchanganua taswira za kifo zinazowasilishwa katika mashairi teule ya Kiswahili.
- ii) Kubainisha visababishi vya kifo vinavyojitokeza katika mashairi teule ya Kiswahili.
- iii) Kufafanua utata unaojitokeza katika ufanuzi wa dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

1.5 Upeo wa utafiti

Utafiti huu ulishughulikia uchanganuzi wa uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Tenzi mbili na shairi moja linalozungumzia kifo liliteuliwa kimakusudi. Uteuzi huu ulijikita kwenye misingi kuwa tenzi hizi mbili na shairi hili moja huwasilisha kiwango kikubwa cha mjadala kuhusu kifo. Pili, haya ni mashairi ya kirasimi ambayo yanawakilisha lugha pevu ya utunzi wa mashairi katika lahaja za Kiamu na Kimvita ambazo zilitoa nafasi nzuri ya uteuzi wa vina mwafaka katika kibwagizo au bahari za mashairi haya yote ili kuoana na swala la kifo kama anavyoeleza Chiraghdin (1971). Tatu, mashairi haya yanatumia mandhari tofauti; dhahiri na dhanifu na hivyo kutupatia uwanja mwafaka wa kujadili kifo katika udhanifu na udhahiri wake.

Watunzi wa mashairi haya yote pia wamewahi kuishi katika mazingira moja japo kwa nyakati tofauti na wote ni waislamu na Waswahili, jambo ambalo lilituwezesha kuoanisha misingi ya mawazo yao kuhusiana na kifo. Tenzi zilizoshughulikiwa ni *Inkishafi* (1810-1820) na *Utenzi wa Mwana Kupona* (1858). Tenzi hizi ziliteuliwa kutokana na upekee wa mitindo yao ambayo imekwepa kusimulia maswala ya kishujaa kama utenzi wa *Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* na *Utenzi wa Ras l'Għuli*. Shairi la ‘Usiniuwe’ liliteuliwa katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973). Shairi hili tofauti na mashairi mengine yenye umbo linalofanana nalo, limetumia mazingira dhahania kwa kutuwasilishia picha ya mtoto tumboni mwa mamake akisihi asiuliwe. Katika diwani hii nzima ni shairi hili pekee ambalo limezungumia swala la kifo.

1.6 Misngi ya uteuzi

Utafiti huu ulichanganua uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Mada hii iliteuliwa kwa misngi kuwa dhana ya kifo huwasilishwa kwa upekee katika ushairi kwa namna inayonasa na kudhibitit hisia za msomaji au msikilizaji wa shairi husika. Hali hii hutokana na mfumo wa shairi ambao unabana lugha kwa kauli fupifupi lakini zilizo na uzito wa mawazo. Swala hili la kifo mara nyingi huzungumziwa kwa ujumla pindi watunzi wa mashairi wanapozungumzia mada walizozingatia katika tungo zao. Hata miongozo anuwai ya vitabu vyar riwaya na tamthilia haijadili kifo kwa kina. Pakubwa tunashuhudia mijadala kuhusu tanzia katika kazi hizo. Tanzia ni msiba unaomkumba jaribosi au mhusika mkuu katika kazi za tamthilia au riwaya. Hali hii ni tofauti na namna kifo kinavyowasilishwa katika ushairi ambapo hupewa sura ya kitu kisicho na ubaguzi bali humkumba kila kiumbe. Ushairi huwasilisha kifo kama mada inayoweza kutawala utunzi mzima huku maswala yote mengine yazungumzwayo yakiongozwa kwenye msingi wa kifo.

Utafiti huu vilevile ulichukulia swala la kifo kama tukio la kipekee ambalo mara nyingi huwasilishwa kupitia mashairi wakati wa maombolezo. Wakati wa kuomboleza wafu, waombolezaji mara nyingi hutumia mbolezi au mashairi ya kuomboleza huku wakitaja sifa za marehemu na kusikitika kwa kuondoka kwake wakati usiofaa. Mashairi mbolezi pia hutumika kujiliwaza au kuwaliwaza wafiwa, Chiraghdin (1971). Mashairi teule ya Kiswahili yanaonyesha namna watunzi wanavyosawiri kifo mbali na uwanja wa maombolezo bali kama tukio fulani la kimaisha linalowasilishwa katika fasihi. Kwa hivyo, uteuzi wa mada hii ulichocheza na kule kutoshughulikiwa kwa kina swala la kifo katika ushairi andishi wa Kiswahili.

1.7 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu unachangia kuonyesha kuwa kuna maandalizi wanayokuwa nayo wanadamu ili wapate kukabiliana na kifo. Maandalizi hayo hujumuisha wosia amba o hutolewa na mzazi kwa mwanawe ama wosia kwa moyo wa mtu binafsi ili kujirudi dhidi ya maovu ya dunia. Wosia huu hudhamiriwa kuongoza na kuelekeza moyo katika njia nyofu na kubalifu kwa mwenyezi Mungu.

Utafiti huu pia ulibaini kuwa kifo ni swala halisia ambalo huweza kumulikwa kifasihi. Dhamira ya fasihi ni kueleza kila kipengee cha maisha namna wanavyoona watu wa jamii na mazingira fulani. Matumizi ya mazingira asilia na halisia huibua taswira bayana katika usawiri wa dhana ya kifo kama tulivyobaini katika utafiti wetu. Ilidhihirika kuwa kifo ni tukio ambalo haliwezi kuepukika, humkumba kila kiumbe, huja wakati usiotarajiwa na hutia watu huzuni kubwa.

Utafiti huu uligundua kuwa kifo ni swala ambalo haliwezi kupuuzwa katika kazi ya fasihi kwa

kuwa huweza kuwa msingi wa kazi nzima ya sanaa. Kutohana na athari za kifo pamoja na hofu aliyo nayo mwanadamu, msukumo wa kuandika huibuka. Watunzi wengine huandika kujiliwaza kutokana na msiba uliowakumba au hali ngumu waliyo nayo ilhali wengine huandika kuzindua wenzao na nafsi zao pia.

Utafiti huu vilevile umeonyesha namna ambavyo tukio la kihistoria kama vile kuporomoka kwa Dola ya Pate linavyoweza kufungamanishwa na tukio la kimaumbile kama kifo ili kuibuka na kazi ya fasihi. Kwa hivyo utafiti huu unadhihirisha namna ambavyo matukio ya kihistoria ni fumano la hali halisi ya jamii na ni kama fasihi halisi, hivyo fasihi ni kama juhudini mbalimbali kuhusu matukio ya jamii. Utafiti huu basi unachangia katika kuitumia fasihi kama kigezo cha kuchora uhalisi wa kifo.

1.8 Nadharia ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia iliyowekewa msingi na mwanafalsafa Hegel (1770-1831) na kufafanuliwa na Georg Lukacs (1938). Nadharia hii pia kwa mujibu wa Wamitila (2002) huhusishwa na wataalamu Gustave Flaubert (1830-1886) na Maxim Gorki (1868-1936). Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa na hivyo kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari yanayooana kwa kiasi kikubwa na uhalisi wa jamii ya mwandishi anayehusika. Kwa mujibu wa Lukacs (1938), swala muhimu katika sanaa si ukinzani ulioibuliwa na wananaadharia wa usasa kuhusu urasimi wa kifasihi bali ni ule uwezo wa sanaa kupata kuibua na kukabili ukweli wa maisha jinsi ulivyo duniani. Anadai kwamba sanaa huwa na lengo moja kuu; kuwasilisha maisha jinsi yalivyo katika jamii husika. Nadharia ya uhalisia huipa fasihi jukumu la kutoa ukweli wa maisha ambao husetiriwa katika mikondo ya

kijamii, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Kipengele cha uhalisia katika utafiti huu kilifanikishwa kwa kuangalia taswira ya kifo katika uhalisi wake kisanaa na kimaisha.

Gikandi (1987) anaeleza kuwa uhalisia ni hali ya kuelewa misukosuko katika jamii zetu na kutambulisha mbinu tunazoweza kutumia katika kuyakwepa masuala magumu yanayoleta madhila na vikwazo katika maendeleo yetu. Kupitia uhalisia tuligundua kuwa mashairi teule ya Kiswahili huonyesha namna mwanadamu anavyojiandaa ili kukwepa shida na mateso yanayotokana na kifo cha mtu binafsi au kifo cha mwenzake.

Kwa mujibu wa Msokile (1993), misingi ya nadharia ya uhalisia ni pamoja na uwezo wa sanaa kutoa na kueleza ukweli na iwakilishe au kuwakilishwa kwa maneno halisi; iseme ukweli na iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira; uhalisia ulichukulia sanaa kama kioo cha uhalisia wa maisha; uhalisia kutojihusisha na matusi, kuchagua mambo ya kuandika; mandhari iwe ni ya asili, msanii asichague, aeleze kila kitu kama kilivyo na ujenzi wa wahusika ulingane na hali halisi, mhusika awe na sura ile ile ya maisha ya kawaida. Wanauhalisia wanaeleza vitu namna wanavyoviona kwa leo. Hivyo ni bayana kuwa uhalisia hutegemea wakati na mazingira ya mtunzi. Uhalisia hubadilikabadilika kwa duru ya wakati.

Vuzo (1999) anaeleza uhalisia kama mtindo wa sanaa unaozingatia ukweli wa mambo. Sanaa hueleza mambo halisi katika jamii kwa njia inayoafiki hali halisi ya mambo katika jamii. Yale yanayotokea katika sanaa si mambo ya maajabu nje ya jamii bali ni yale yaliyomo katika jamii.

Wamitila (2002) naye anaeleza kwamba msingi mkuu wa uhalisia ni usimulizi wa kimuhakati.

Huu ni usimulizi unaosimulia matukio jinsi yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inavyokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Tatizo lililoko ni kuwa wasomaji mbalimbali hawawezi kuuangalia uhalisi kwa njia sawa. Anachokiona msomaji mmoja kama uhalisia huenda mwingine asikione kama uhalisia. Hivyo basi kila kizazi kina uhalisia wake.

Dhana ya uhalisia pia hutumiwa kuashiria kipindi maalum katika historia ya fasihi ya Ulaya na pia kuelezea aina ya mtazamo au tapo la fasihi ambalo huchukuliwa kuwasilisha ukweli au uhalisi fulani wa maisha. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), kazi ambazo ni za kihalisia zinatarajiwa ziwe na akisiko la hali halisi ya maisha ya jamii inayohusika. Wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi, kuyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao, na kusawiri na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), uhalisia hutumiwa kutathmini hali au halia. Huu ni uhalisia wa maisha. Uhaliisa wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Uhaliisa unahusisha uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Anayehakiki kazi za kihalisia ni lazima amtathmini mwandishi kwa namna ambayo huyo mwandishi alijibidiisha kuonyesha ukweli katika kazi yake. Mwandishi wa kihalisia naye anatarajiwa kuitoa picha ya jamii bila kuipigia chuku wala kuidunisha. Uandishi wa kihalisia hivyo basi hupaswa kuwa na mlingano mkubwa na kinachoonekana katika jamii.

Nadharia ya Uhaliisa nayo imekuwepo tangu karne mbili zilizopita. Nadharia hii ilitumika sana katika karne ya ishirini na sasa katika karne ya ishirini na moja. Thomas Aquinas ni mmoja wa

waasisi aliyechukua mstari wa mbele. Hii ni nadharia ambayo huipa fasihi jukumu la kuonyesha ukweli wa maisha. Ukweli huo hujitokeza katika mikondo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Pia fasihi hujaribu kueleza sababu za matukio katika jamii na kuonyesha mielekeo yake. Kipengele cha uhalisia kilifanikishwa katika utafiti huu kwa kuchunguza taswira ya kifo.

Wataalamu Msokile (1993), Wamitila (2002), na Wafula na Njogu (2007) kwa kurejelea mawazo ya Lukacs (1938), Tolstoy (1828-1910), Aristotle (384-322KK) na Hegel (1770-1831) wanaeleza misingi ya nadharia ya uhalisia ambayo ilikuwa muhimu na mwafaka katika kufanikisha ufikiaji wa malengo na madhumuni ya utafiti huu. Sifa hizo ni pamoja na tajriba ya mwandishi, vielelezo, historia ya jamii, muundo wa kazi na lugha.

- Tajriba ya Mwandishi

Kazi anayoiandika mwandishi ni lazima ioane na uelewa na tajriba yake. Mwandishi huathiriwa na mazingira yake kielimu, kijamii na kisiasa pamoja na harakati za kiuchumi. Hivyo basi tajriba anayokuwa nayo ni mchango wa jamii nzima kama anavyodai Caudwell (1947). Fasihi kwa hivyo ni lazima ifanyiwe uchunguzi kwa kutegemea athari ya yote yale yanayojenga tajriba anayoibuka nayo mtunzi katika kuandika kazi yake. Naye Nanyama (2005) anatueleza kuwa fasihi ina jukumu la kumulika uhalisi wa kijamii na wanafasihi huelezea matatizo na mafanikio ya jamii kama wanavyoyaona kulingana na tajriba zao. Mwandishi huyafichua matatizo na mafanikio ya jamii kwa kuyaweka kwa lugha ya wazi yenye kuelewaka. Utafiti wetu ulibaini kuwa tajriba ya mshairi humfunulia mwanya wa kuelewa na kusuka kazi yake kikamilifu. Ilibainika kuwa watunzi wa mashairi teule ya Kiswahili wanalizungumzia swala la kifo kwa misingi ya mazingira yao na mafunzo ya dini zao.

- Historia ya jamii

Kazi ya sanaa mara nyingi hujikita katika wakati fulani kihistoria. Mwandishi atungapo kazi yake huwa anachota maudhui na lugha kutoka katika mazingira yake katika kipindi fulani maalum cha kihistoria. Kwa kufanya hivi anaibua uhalisia wa historia katika kazi yake. Historia ya jamii hudhihirisha mabadiliko ya dhana fulani pamoja na fasiri zao. Kipengee hiki cha nadharia huonyesha namna dhana inayoshughulikiwa inahusiana na mazingira ya kihistoria yanayomhusu mwandishi na mazingira yake. Mahusiano haya huonyesha kuwa dhana inayozungumziwa katika kazi ya sanaa inaweza kuwa imewahi kutokea katika jamii au ni ubunifu lakini ina uhusiano na athari katika maisha ya mwandishi. Kwa kutumia kipengee hiki cha nadharia ya uhalisia, tulibaini namna mtunzi huweza kutumia tukio la kihistoria kama vile kuanguka kwa Dola ya Pate ili kusawiri tukio la kifo katika maisha ya mwanadamu. Kuanguka kwa dola hii ni sawa na kufa kwa mwanadamu na hivyo mtunzi hutumia tukio hili ili kuikanya nafsi yake dhidi ya kupenda dunia ambayo haidumu bali ni mapito ya muda.

- Vielelezo

Uhalisia huiga mazingira na matukio yake. Uigizaji huu hujihusisha na kile kinachoigwa ili kudhihirisha ukweli kwa kudodosa mambo. Mwandishi hivyo basi hana budi kuyaeleza mambo yale kwa uyakinifu na ukamilifu ili kuonyesha ukweli wa maisha. Nochlin (1971) anashadidia uwasilishaji wa mambo kihalisia ili kuondoa maruweruwe ya ufahamu katika kutafsiri mambo hayo. Hivyo basi mwandishi hana budi kuyachota maudhui yake kutoka katika mazingira halisia kama anavyoeleza Stromberg (1968). Ni kutohana na maslahi na mahitaji ya jamii ndipo tunapata kwamba fasihi inatakiwa kutoa vielelezo vyta ukweli wa maisha ambavyo ni vyta manufaa kwa umma. Fasihi kwa hivyo hutumika kuielekeza jamii katika njia faafu ili kukwepa

mitego ya maisha. Katika utafiti wetu, ilibainika kuwa washairi hutumia mazingira yao ili kudhihiri kupanda na kushuka kwa maisha.

Kwa kutumia vielelezo vinavyofaa dhana ya kifo imeweza kusukwa kwa uwazi na uzito katika mashairi teule ya Kiswahili. Watunzi wa ushairi wametoa ishara ya kufa na matukio ya baadaye baada ya kufa kwa kuchuja vitu vinavyotisha kama vile moto wa jehanamu. Waaidha kipengee hiki kinatuelekeza kutopuuza kile kinachotajwa katika fasihi kwani kila kinachotumika kina jukumu na maana mahususi katika kuendeleza na kuukuza ujumbe wa shairi.

- Muundo wa kazi

Mwandishi anafaa atumie muundo unaokubalika katika utunzi wa sanaa yake. Huu ni muundo ambao umekubaliwa na wanajamii kuwa ndio msingi unaokubalika katika utunzi fulani. Katika lugha ya Kiswahili, utunzi wa ushairi mapokeo uliwekewa kanuni zilizofafanuliwa na Abedi (1954) na kushadidiwa na Mayoka (1984) na Ruo (1988). Ushairi wa kimapinduzi nao uliwekewa msingi na tungo za Kezilahabi (1974) na Mulokozi na Kahigi (1979). Washairi wa Kiswahili hivyo basi hawana budi kujikita katika mojawapo ya muundo wa mashairi kwa kutegemea mapote hayo mawili.

Muundo wa mashairi ya arudhi hubainika katika matumizi ya vina na mizani. Uteuzi mzuri wa vina na mizani hutupatia mrindimo na hisi mbalimbali kwa kutegemea ujumbe unaozungumziwa. Tulibaini kuwa ukariri wa vina vya aina fulani hujenga hisia za uchungu, kutamauka na hofu wakati swala la kifo linapozungumziwa.

- Lugha

Lugha anayotumia mwandishi ni lazima iafikiane na uhalisia wa wakati wa mwandishi. Lugha hii huibuka katika misemo, methali, taswira na tamathali anazotumia mwandishi. Vyote hivi vinafaa viwe vinafahamika na jamii anayoziandikia. Mwandishi pia atadhihirisha mabadiliko katika matumizi ya misamiati kimatamshi na kimaandishi. Mabadiliko katika lugha huweza kuchunguzwa kisinkronia au kidaikoronia jinsi aelezavyo Mgullu (1999). Kutokana na mabadiliko ya msamiati tunaweza kubaini ukweli wa tafsiri ya dhana mbalimbali pamoja na hisia tofautitofauti kuhusiana nayo. Nanyama (2005) anaeleza kuwa lugha ni kipengele muhimu kinachojenga kazi ya fasihi yoyote ile. Lugha ni wenzo wa fasihi ambayo huzalisha sanaa ya fasihi. Umuhimu wa lugha katika fasihi hupatikana katika maana iliyokusudiwa na mwandishi na maana inayoelewaka na msomaji. Hivyo lugha huonekana kama nguzo muhimu katika ujenzi wa kazi ya fasihi. Hapawezi kuwepo fasihi bila lugha ya kuiwasilisha. Lugha ndiyo inayotumika na mwandishi ili kujieleza au kujitambulisha kwa hadhira yake. Naye Chomsky (1990) anasema kuwa lugha hujikita katika misingi ya kijamii, maadili, mapatano na desturi za jamii husika. Halliday na Hassan (1985) wanaeleza kuwa matumizi ya lugha yana muktadha wake mahususi. Hivyo basi, lugha inafaa ichukuliwe kama kielelezo cha uhalisia mintaarafu ya wajibu unaotekelawa na lugha hiyo katika utatuzi wa matatizo ya kimawasiliano katika jamii. Hali hii inashadidiwa na Mukuria (2001) anayesema kuwa lugha hupenya katika mawanda yote ya maisha ya mwanadamu, kiasi cha kufanya isiweze kutenganishwa na jamii.

Habwe na wenzake (2010) wanatueleza kuwa mabadiliko ya kitamaduni huonekana kuitia lugha. Kwa mfano, katika miaka ya hivi karibuni dhana ya kifo imeanza kuchukuliwa kwa mtazamo tofauti. Utasikia badala ya kusema, "Tunaomboleza kifo cha fulani" watu wakisema

"Tunasherehekeea maisha ya fulani". Mtindo wa kucaa nguo nyeupe nao umeibuka ili kuashiria wazo la kusherehekeea. Ufafanuzi huu unatudokezea kwamba dini na athari za mabadiliko ya kitamaduni hutokana na mwngiliano mwngi ambaa umepata kuingia katika matukio ya kimsiba. Badala ya kukata tamaa kwa kucaa nguo nyeusi mazishini, watu wanajipa matumaini kwa kucaa nguo nyeupe maana kule mbinguni alikoenda marehemu kunatarajiwa mema pekee wala siyo mabaya. Ishara ya mema ni weupe unaoashiriwa na nguo nyeupe zivaliwazo na wafiwa. Katika mashairi teule ya Kiswahili utafiti huu uligundua kwamba japo kifo ni swala la kukatisha tamaa na kutia watu huzuni kuu, mwanadamu hakosi tamaa ya kuishi peponi.

Mihimili hii ilitumiwa ili kuthibitisha ni kwa namna ipi tajriba ya mwandishi humtofautisha katika kueleza na kuonyesha msimamo wake kuhusu kifo mbali na mawazo ya jamii yake; ni jinsi gani anakubaliana na jamii yake na kutengana nayo kuhusu kifo. Historia ya jamii ilitumika kuonyesha matukio ya kihistoria jinsi yanavyowiana na tukio la kifo katika maisha halisi. Vielelezo vilitumika ili kubaini ni kwa jinsi gani mazingira hutumika kueleza kifo. Hali hii ilisaidia kuelewa mwandishi anavyotumia mazingira yake ili kujenga taswira ya kifo na kuibua utata wake. Muundo wa kazi nao ulitumika kuthibitisha upekee wa kihisia unaojitokeza katika uwasilishaji wa kifo kwa namna inayokubalika kishairi katika jamii maalum. Muundo katika ushairi huzingatia vipengee vya vina, mizani, kibwagizo na beti. Vipengee hivi huleta utoshelezi au urari unaofaa kwa kuzingatia swala la kifo katika mashairi tuliyoshughulikia katika utafiti wetu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumeangazia maoni ya waandishi mbalimbali ambao wameandika kuhusu dhana ya kifo kwa ujumla. Vilevile tumejaribu kuangazia historia fupi ya ushairi wa Kiswahili ili kuonyesha mashairi teule tuliyoyashughulikia katika utafiti huu. Tumejaribu kuonyesha namna maandishi hayo yanavyohusiana na utafiti huu. Katika kurejelea kazi hizo tulizingatia mada ambazo zinahusiana na utafiti wetu na jinsi mada hizo zimewahi kuandikiwa na watafiti wengine katika ushairi wa Kiswahili.

2.2 Historia fupi ya Ushairi wa Kiswahili

Ushairi wa Kiswahili ni wa kale kama ilivyo lugha yenyewe. Ushairi huu awali ulikuwa ukitungwa na kuhifadhiwa akilini jinsi ushairi wa jamii nyinginezo barani Afrika ulivyokuwa ukifanywa. Hakukuwa na hati za kimaandishi ambazo zingetumika kuhifadhi tungo hizi. Baadaye kuja kwa wageni wa Arabuni na Ulaya kulifanya tungo za ushairi kuanza kuhifadhiwa katika hati za maandishi ya Kiarabu na Kirumi mtawalia. Kwa mujibu wa Mulokozi (1999), ushairi wa Kiswahili huweza kugawika katika awamu za kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Kipindi cha kabla ya ukoloni kina awamu tatu: awamu ya kwanza ni baina ya (k.900-1500M), kipindi hiki kilikuwa na ustawi wa miji ya Waswahili; awamu ya pili ni baina ya (k.1500-1730) ambayo ilikuwa enzi ya utawala wa Mreno na upinzani wa wenyeji dhidi yake; na awamu ya tatu ni baina ya (1730-1890) ambayo ni wakati wa utawala wa Oman na kuasiwiwa

kwa Uislamu mwambao wa Afrika ya Mashariki. Ni katika awamu hii ya tatu ambapo tunakumbana na tenzi mbili kuu tunazozishughulikia katika utafiti huu: *Al-Inkishafi* na *Utenzi wa Mwana Kupona*. Tenzi hizi ziliathiriwa pakubwa na dini ya Kiislamu ambayo ilikuja kukita mizizi na kuingiliana na tamaduni za wenyeji kiasi kwamba kubainisha mpaka baina ya dini na utamaduni wa wenyeji ilikuwa vigumu sana. Waaidha Mulokozi hatupatii awamu nyinginezo za utunzi wa mashairi ya Kiswahili wakati wa na baada ya ukoloni. Awamu hizi zingine tunazipata kwa Kezilahabi (1983) anayeziorodhesha muhula wa urasimi 1728-1885; muhula wa utasa 1885-1945, muhula wa urasimi mpya 1945-1960 na muhula wa usasa 1967-hadi leo.

Katika vipindi hivi vya awali katika ukuaji wa ushairi wa Kiswahili kulikuwa na tungo anuwai za tenzi ambazo pakubwa zilishughulikia maswala ya dini ya Kiislamu kama vile kasida za kumsifu mtume Muhammad (s.a.w) pamoja na zile za kutukuza uislamu. Tenzi hizo ni pamoja na *Utenzi wa Ras-il-Ghuli*, *Hamziyya*, *Inkishafi*, *Utenzi wa Qiyama* miongoni mwa tenzi nyinginezo. Tungo nyinginezo kama vile *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni zile za kutoa sifa za mashujaa wa Uswahilini kama vile Liyongo. Ilmradi tungo hizi zikawa ni kama tungo za kidini. Inadaiwa na watafiti wa ushairi wa Kiswahili kuwa ni Muyaka bin Hajj al-Ghassany ambaye alitoa ushairi wa Kiswahili na kutia sokoni kwa kutungia mada mbalimbali katika kazi zake mbali na maswala ya kidini, (Abdulaziz 1979).

Licha ya hawa wataalamu kutupatia awamu za utunzi wa mashairi ya Kiswahili wanataja kijujuu maudhui ambayo yalishughulikiwa katika awamu hizi tofauti. Pia mjadala wao umezingatia pakubwa muundo wa mashairi hayo pamoja na ukwasi wa lugha ambao ulitumika

ili kuunda tungo hizi. Hawachanganui maudhui hayo kwa kina ili tuelewe ufanifu wa maudhui hayo enzi hizo pamoja na mabadiliko kimaudhui katika ushairi wa Kiswahili kwa ujumla. Utafiti huu unalenga kuchanganua kifo katika mashairi teule ya Kiswahili kwa kuzingatia uhalisia wa kifasihi na wa kimaisha wa dhana hii ya kifo.

2.3 Dhana ya kifo

Dhana ya kifo hutazamwa kwa namna tofauti kwa kutegemea nyanja mbalimbali za kielimu. Mitazamo hii hujibainisha vema katika uwanja wa dini, fasihi na falsafa. Japo kwa upeo mkubwa nyanja hizi hubainisha kuwa kifo ni kinyume cha uhai, lakini kuna utata wa ubainishaji na utenganishaji wa kifo na uhai.

Kwa mujibu wa dini za Kikristo kifo hutazamwa kama tukio la lazima na ni adhabu ambayo Adamu alipewa baada ya kuasi agizo la Mungu na akamuata ibilisi kula tunda lililoharamishwa. Katika Biblia, Agano la Kale, Mungu aliwaamuru Adamu na Hawa wasile matunda ya mti wa kati lakini walipoasi agizo hilo walipewa adhabu ya kifo (Mwanzo 3:19). Baada ya adhabu hii kutolewa kila kiumbe ambaye ni zao la Adamu angepata kukumbana na kifo. Hakuna mwanadamu ambaye ana uwezo wa kuepuka mauti. Hali hii pia husisitizwa katika Qur'an (29:57; 21:35 na 3:185) ambapo tunaelezwa kuwa kila nafsi itapata kuonja mauti. Tangu Mungu kutoa hukumu ya kifo kwa Adamu, wazawa wa Adamu wangali wanakufa na hawana njia ya kukwepa mauti. Lakini kuna maisha baada ya kufa ambapo watu wema watapewa uzima wa milele na wale waovu watatiwa kwenye moto wa jehanamu daima. Yamkini hapa kuwa kuna uhai au kuishi kwa namna nyngine baada ya kuaga dunia.

Mawazo haya ya kidini yanatupatia mwangaza kuhusu kisababishi cha kifo. Maasi dhidi ya Muumba huonekana kama ndiyo chanzo cha mwanadamu kuadhibiwa kufa. Mwanadamu anaonyeshwa kama mnyonge na aliyepungukiwa na uwezo mbele ya mauti. Hata hivyo mawazo haya hayatuonyeshi jitihada anazotia mwanadamu katika mazingira yake ili kupata kufasiri vema dhana ya kifo. Mwanadamu ametia jitihada kubwa katika kuoanisha matukio katika maisha yake na mazingira yake. Katika utafiti huu tumeonyesha namna mazingira yanavyoathiri uwasilishaji wa dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

Miongoni mwa jamii za Kiafrika, kifo ni kitu ambacho kipo na kina sababu zake. Hakuna kifo ambacho hutokea bila sababu maalum. Kila kifo husababishwa na ‘mkono wa mtu’. Hali hii imebainika katika tafiti mbalimbali za wataalamu ambao wameshughulikia swala la kifo katika fasihi simulizi za jamii nyingi za Kiafrika. Watafiti kama vile Finnegan (1970), p’Bitek (1974), Nandwa (1976), Akivaga na Odaga (1982) na Alembi (2001) wakitafitia ushairi simulizi wa jamii mbalimbali za Kiafrika wanathibitisha kuwa kuna imani kuu ya ushirikina kuhusiana na kifo cha yejote yule miongoni mwa wanajamii. Wafu pia huaminika kuwa bado wana nguvu za kuwadhuru au kuwafaa walio hai, kwa hivyo ni muhimu kuwahudumia kwa kutoa kafara na kuwazika kwa heshima. Kulingana na mtazamo huu ni bayana kuwa kufa kwa mwili si mwisho wa maisha kule kuzimuni miongoni mwa Waafrika. Katika jamii hizi za Kiafrika kuna nyimbo nyingi za kuomboleza kifo cha mwenzao. Nyimbo hizi hughaniwa au huimbwa zikiandamana na shughuli nzima ya kuzika. Katika nyimbo hizi sifa za aliyekufa hutajwa, uhusiano wake na mwimbaji (waimbaji) na mara nyingi kisababishi cha kifo pia husemwa kwa njia ya mafumbo. Hali hii hutupatia taswira nzima ya kifo na athari yake kwa wafiiwa. Hata hivyo watafiti hawa walionyesha swala la kifo katika uwanja wa fasihi simulizi lakini hawakuonyesha fasiri ya kifo

katika fasihi andishi. Utafiti wetu ulipata mwanya wa kushughulikia swala hili katika ushairi andishi wa Kiswahili.

Wanasosholojia kama vile Mugambi na Kirima (1976) hutazama kifo kama hatua ya mapito ya maisha ya kila kiumbe hai. Kifo ni awamu ya mapito kutoka duniani hadi katika ulimwengu wa wafu. Kifo ni hatua ya mwisho ambayo roho ya mwanadamu hupitia na kugeuka kutoka umbo dhahiri hadi umbo dhahania au lisilo dhahiri. Maelezo haya ya wanasosholojia huonyesha kuwa kifo ni daraja ya lazima kwa kila kiumbe hai na ni muhimu kuielewa hatua hii kama kiungo cha maisha.

Wanasayansi nao huona kifo kama kule kukoma kupumua kwa kiumbe hai. Endapo kiumbe hai atakoma kupumua na kisha aanze kuoza basi huyo huchukuliwa kama amekufa. Wanasayansi wanatazama kifo kama mwisho wa uhai wala hakuna maisha mengine baada ya kufa. Nao wanaendelea mbele zaidi kumchunguza mtu anayekaribia kufa na kubaini kuwa kuna hatua nane ambazo anayekaribia kufa hupitia kabla ya kujisalimisha mikononi mwa mauti. Morwood (1996) anazitaja hatua hizo toka mwanzo hadi pale mtu anapokufa:

- i. Wakati wa kifo unapokaribia, mwili wako utaanza kuzimia, kwa mfano, kupoteza hamu ya kula na kushindwa kunywa vinywaji.
- ii. Mdomo wako utakauka na utakojoa mara chache sana.
- iii. Wakati kasi ya damu inapopungua mwilini mwako, utaweza kuhisi joto kisha baridi.

- iv. Kupumua kwako kutakosa ukawaida wake huku kila baada ya mpumuo ukikaa tuli kabla ya kupumua tena.
- v. Uwezo wako wa kufikiria utavurugika na kupungua.
- vi. Kila hali ya ukakamavu na ujasiri itapotea.
- vii. Uhusiano na tamaa zitapotea. Wakati huu akili yako itakuwa tupu kuhusiana na tukio lolote la kimaumbile na hali ya kiza itaanza kudhihirika na utupu mfano wa anga lililo wazi bila jua wala mwangaza wowote ule.

Uhusiano na dunia hutoweka na mwangaza wa kuzimu hujongea na kuingia akilini na hapo mtu hufa.

Maelezo haya ya kisayansi yanaonyesha upungufu wa mwanadamu kuweza kubaini kile ambacho hutokea baada ya mtu kufa; hayadhihirishi maandalizi anayokuwa nayo mtu anayekaribia kufa au anapotabiri kifo chake. Vilevile hatuelezwi endapo kuna maisha baada ya kufa ama kama kule kufariki ndiko mwisho wa maisha ya mwanadamu. Hivyo basi ni muhimu kuchunguza maandalizi ya kufa na matukio yanayotokea baada ya kufa kwa mwili wa mwanadamu.

Charity (1966) akizungumzia kifo anafafanua hatua za kufa, namna au hali inayomkumba mtu anayekaribia kufa. Anaeleza kwamba mwanzo kuna kutamauka kunakosababisha toba lakini haileti kamwe msamaha wa maovu aliyotenda mtu huyo. Mawazo haya yanajikita katika

saikolojia ya anayekaribia kufa ambaye kwa kuchelea adhabu katika mauti anaamua kutubu na kuomba msamaha. Maelezo haya yanatudokezea kwamba katika kufa kimwili, roho ndiyo hupewa adhabu ahera. Ili kunusuru roho hii inabidi mwili ulio hai utubu na kuomba maghofira kwa Mungu. Mtaalamu huyu hatuelezi wapi roho zinakoenda baada ya kufa na kupata hukumu. Vilevile hatuelezi iwapo kifo ni hatima ya kila kitu ama ni chanzo cha maisha mapya. Anatuacha tukibaki kujiuliza ni kwa nini roho ndiyo inapata adhabu ahera badala ya mwili ambao unatenda maovu duniani? Hata hivyo anatupatia mwangaza kuhusu maandalizi ya kifo pale anapodokeza kuwa kuna toba inayotolewa na wale wanaokaribia kufa. Mchango huu ni wa kimsingi katika kuelewa kauli au wosia unaotolewa na mzazi kwa mwanawe au maaso ya moyo dhidi ya feli za dunia ili kukwepa adhabu ya mauti kule ahera.

Ni wazi kuwa dhana ya kifo ina fasiri kadhaa kwa kutegemea mkondo wa taaluma husika. Kifo hata hivyo hudhihirika kuwa ni kutoweka kwa uhai katika wakati fulani. Kisababishi cha kifo ni makisio ya wanajamii wanayoyatumia ili kupata kufasiri kinaga ubaga dhana ya kifo na utokeaji wake. Mwanadamu anasadiki kuwa kufariki kuko lakini ni lazima kuwe na sababu mwafaka ya kuegemeza tukio hili la kifo pindi linapomkumba. Mbali na fafanuzi hizi kuhusu dhana ya kifo, utafiti huu uliangazia kifo kama kitu ambacho kipo tu katika fikira za mwanadamu wala hakuna aliywahi kukionja akarejea kusimulia yaliyoko kifoni. Kifo ni hatua ya mapito katika maisha wala si mwanzo ama mwisho wake.

2.4 Chanzo cha kifo na ukubalifu wake

Kifo hutazamwa katika mikabala tofautitofauti katika pande mbalimbali za dunia. Maudhui ya

kifo hujitokeza kwa wingi katika kazi kadhaa za fasihi. Hupewa sitiari na kufungamanishwa na maana mbalimbali, kila mara huonyesha mwisho au mwanzo wa maisha. Wataalamu mbalimbali wametoa fasiri ya kifo kwa namna tofautitofauti huku wakijaribu kuonyesha chanzo chake na vile mwanadamu amekuja kukubali tukio la kifo katika maisha yake.

Mbiti (1969) anaeleza kuwa binadamu amepata kukubali kifo kama sehemu ya maisha yake ila hana mkondo wa kubatili hali hii. Lakini mbali na kukubali hali hii kuwa ni maumbile binadamu bado anahisi kwamba kifo huletwa au husababishwa na kitu ama nguvu fulani mbali na Mungu na maumbile. Pindi mtu afapo watu ni lazima watoe kisababishi cha kifo chake. Kwa kiwango kikubwa watu hutaja uganga ama uchawi, laana ya kijamii, mizimu au roho za wafu ambazo hazikuridhika na namna zilivyonendewa duniani, nguvu za Mungu kuitia mpasuko wa radi na mtu kuenda kinyume na maadili au desturi za kijamii. Utafiti huu unashikilia kuwa kifo ni tukio la kihalisia na huweza kufasiriwa kifasihi ili kulielewa sababu zake na utata unaomkumba mwanadamu pindi anapokumbwa na kifo.

Addinall (1991) na Carnley (1997) wanakubaliana kuwa maovu ndiyo chanzo cha maangamizi ya roho. Wanaeleza kuwa maovu hayo ndiyo humfanya mwanadamu kujaribu kunusuru roho yake kwa kumwabudu Mungu. Kisha wanaeleza kuwa kuna mjadala wa ‘Kufa kwa Mungu’ ulioshamiri na kushika kani katika miaka ya 1960 na hivyo kuzua kupungua kwa imani kwa Mungu hususan mionganini mwa Wakristo. Hata hivyo utafiti huu ulibaini kuwa si maovu pekee ambayo ni chanzo cha mauti. Hii ni kwa sababu hata watendao mazuri na mema pia hufa. Hata watoto ambao hawajazaliwa pia hufa na huogopa kufa. Mawazo haya ni muhimu katika kupanua uelewa kuhusu visababishi vya kifo.

Kwa mujibu wa Kenny (1979), kuna nguvu za kimaumbile ambazo husababisha matukio kama kifo kutokea. Anadai kwamba licha ya mwanadamu kujua kuwa atakufa hawezi kuepukana na mauti yake. Anarejelea Biblia kuthibitisha madai yake kwamba licha ya Yesu Kristo kujua kwamba Judas angemsaliti hakuwa na namna ya kuepuka hali hiyo. Judas naye hakuwa na njia ya kujizuia au kutoroka ila kumsaliti Yesu na kusababisha kifo chake. Hivyo basi anamwona Mungu kama chanzo cha kifo na kila mtu kifo chake tayari kimeandaliwa na kitakachosababisha kifo hicho hakiwezi kuepukika kwa vyovyyote vile.

Kelly (2006) anatueleza kuwa katika Agano Jipya (Biblia), ibilisi analinganishwa na shughuli za mfalme wa mauti katika barua za Petro kwa Wahebrania na Wayudea. Hapa anatudhihirishia kuwa kifo kinasababishwa na ibilisi ambaye tokea kuumbwa kwa dunia alimwasi Muumba na hivyo akatumbukizwa duniani awe mfalme wa maovu na maangamizi. Wanaotenda maovu hatimaye hufa na kuenda katika jehanamu lakini wanaotenda mema licha ya kufa kimwili wapo hai kiroho na watafufuliwa siku ya mwisho kwenda paradiso. Hivyo basi kifo kinaonekana kama kitu ambacho kimeumbwa na ni ufalme uliopewa ibilisi kuutawala. Ufafanuzi huu unaonyesha kuwa kifo ni ufalme unaotawaliwa na shetani na kila anayekufa huingia katika utawala wa shetani. Lakini hatuonyeshwi matukio baada ya kufa katika ufalme huu wa shetani kama tulivyoangazia katika utafiti wetu.

Shorter (1973) anaeleza kwamba kuishi hapa na kwa wakati huu ndio mshikilio madhubuti katika shughuli za kidini za Kiafrika. Kuna msisitizo mdogo wa maswala ya kiroho mbali na maisha ya kimwili. Hamna mwanya baina ya maisha ya kiroho na ya kimwili. Hata baada ya kufa maisha hutazamwa katika umilisi wa mali na mambo yanayoshikika. Hakuna paradiso ya

kutumainiwa wala jehanamu ya kuogofya katika maisha baada ya kufa. Roho ya mwanadamu haitarajii kukombolewa wala kukaa karibu na Mwenyezi Mungu. Mtazamo huu ni wa kidini na kiitikadi na hudhihirisha tofauti za kiimani baina ya makabila ya Kiafrika na tamaduni ngeni za Kikristo na Kiislamu kutoka Ulaya au Magharibi na Bara Asia. Dini hizi mbili zina imani ya kukombolewa kwa roho pindi kiyama kitakapotokea. Tofauti hizi hudhihirika zaidi kiasi kwamba baadhi ya makabila ya Kiafrika kama vile Bemba kutoka Zambia hunong'onezea maiti ujumbe ili aupeleke kuzimuni. Katika jamii nyinginezo kama ya Wachaga kutoka Tanzania kuna mazishi mara mbili kwa mtu aliyekufa. Hapa maiti huzikwa halafu baada ya siku kadhaa kupita hufukuliwa na kuzikwa upya katika sehemu nyingine tofauti. Tendo hili hufanywa ili kumfanya yule nduli wa mauti apoteze njia ya kurudi nyumbani kulikofiya akawaua waliobaki hai. Miiongoni mwa Washona kule Zimbabwe maiti huitwa nyumbani kama hatua ya kufukuza pepo wabaya wa mauti. Hapa tunagundua kwamba mawazo ya mtaalamu huyu yamejifunga katika mazingira ya Waafrika bila ya kutuonyesha mwengiliano wa kitamaduni kutoka nje hususan athari za Ukristo kwa imani za kijadi za Waafrika. Utafiti wetu ulijikita katika uwanja mmoja wa mashairi teule ya Kiswahili ili kupata fasiri bayana ya dhana ya kifo badala ya ujumlishaji uliotolewa na mtaalamu huyu.

Kwa mujibu wa Hussein (1988) katika kazi yake, *Kwenye Ukingo wa Thim*, tamthilia kuhusu jamii ya Waluo, kuna madai kuwa kifo husababishwa na *Chira*. Chira ni mkosi au laana inayomwandama mtu kwa kukosa kufanya mambo jinsi mila na desturi ya jamii inavyohitaji. Anayetenda kinyume na itikadi hizi huandamwa na mikosi pamoja na magonjwa ya kiajabuajabu ambayo hatimaye humuua. Mawazo haya pia yanashikiliwa na Okombo (1983). Ila Okombo anazidi kutueleza kuwa endapo kifo kimejitokeza mara kwa mara katika familia fulani, hususan

kwa mwanamke kupoteza watoto wake wakiwa wadogo, endapo atazaa tena, kuna tambiko linalofanywa ili kumpofusha au kumkanganya malaika wa mauti asirudi kuua katika familia hii. Mtoto huyo azaliwapo hutupwa kando ya njia ili pepo za mauti zisimpate nyumbani. Kisha mtoto huyu huokotwa na yeoyote atakayempata na kumleta nyumbani. Ni imani ambayo ilishitadi katika jamii ya Waluo kwa muda mrefu. Ogolla (1996) pia ana maelezo sawia na Okombo kuhusu jamii ya Waluo nchini Kenya.

Walibora (1996) anaona maisha kama ukungu, lichomozapo jua la mauti hauna budi kutoweka. Ni bayana hapa kwamba kifo ni kama jua ambalo pindi linapochomoza huyeyusha ukungu (maisha) ambao hauwezi kustahimili joto lake. Vitu hivi viwili, jua (kifo) na ukungu (maisha) havitangamani, kimoja kikiwepo kingine hutoweka. Ni kama giza na mwangaza. Uwepo wa giza ni ukosefu wa mwangaza, uwepo wa mwangaza ni kutoweka kwa giza. Walibora hapa anatupatia utata wa kuelewa kifo. Licha ya kumithilisha kifo na jua na maisha na ukungu kuna ugumu wa kuelewa ni kwa nini anatumia vitu hivi ili kufafanua dhana ya kifo. Utafiti huu kwa hivyo ulijaribu kuonyesha namna mazingira ya mwandishi yanavyoathiri ufasiri wake wa matukio fulani katika jamii kama vile tukio la kifo.

2.5 Ukweli wa uwepo wa kifo na hatima ya maisha

Ushairi wa Kiswahili pakubwa umeshughulikiwa katika uchambuzi mbalimbali. Wachambuzi wa awali kama vile Mayoka (1984) na Ruo (1988) pamoja na Kezilahabi (1983) walipata kuzungumzia ufaafu au kutofaa kwa mtindo maalum wa ushairi katika kuelezea maswala anuwai ya kijamii. Almuradi kuna uainishaji wa mashairi kwa kutegemea mada au shughuli za kijamii. Uanishaji huu huonyesha ni wapi na kwa nini shairi fulani hutumika kwa kazi husika. Walakini

uainishaji huu hautupatii uelewa wa kina jinsi mada za kila namna zinavyosukwa na kusawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Mada mojawapo ambayo hutajwa tu katika ushairi wa Kiswahili ni kifo. Kifo hujitokeza katika mashairi mbalimbali ya Kiswahili ila hutajwa tu juujuu na hujumuishwa katika kundi la mashairi ya majonzi au maliwazo kama tunavyoshuhudia katika Nassir (1971) na Mnyampala (1965). Hata mashairi yanayoshughulikia kifo ambayo hutajwa kwa wingi ni mbolezi ambayo ni mashairi ya kisimulizi kama tunavyoona katika Wamitila (2002).

Kifo ni swala ambalo latisha kwa kila mtu. Uwoga wa kifo si swala jipya ulimwenguni. Kifo ni swala la kimsingi katika maisha ya mwanadamu, japokuwa wengi wanazidi kulikwepa. Ndiposa Giddens (1990:85) anasema:

Kwetu sisi kifo ni swala ambalo hupita bila kujadiliwa. Huchukuliwa kimzaha kuwa watu huogopa kufa, na hivyo madaktari na wanajamii hukwepa kuamini kuwa mtu aliye mgonjwa mahututi lazima atakufa.

Kukwepa ukweli wa kifo ni kawaida ya mwanadamu ili kujipa moyo kuwa maisha bado yangalipo na kifo hakina nafasi kumchukua yejote. Ili kuthibitisha hali ya kutokubali kifo, Despelder na Strickland (1998) wanasema kuwa mwanadamu haamini katu uwepo wa kifo na hukiweka katika mkabala wa kisichokuwepo machoni na akilini hakipo. Haya ni maumbile ya mwanadamu mradi yungali hai. Maisha ni matamu na hakuna mtu anayetaka kuota kufa au kufiliwa na mwenzake.

Licha ya kutokubali uwepo wa kifo, utafiti wetu ulionyesha kuwa kifo ni tukio ambalo hukumba

wanajamii na kila uchao ni jambo ambalo hawawezi kulikwepa. Kifo humtatiza mwanadamu huku akiona wenzake wakiathiriwa nacho. Kufa kwa wenzake humpa nafasi ya kujadili sababu za kufa kwao.

Kimmel (1980:494) anathibitisha ukwepaji wa uwepo wa kifo akisema:

Haiyumkini ukataaji wa uhalisi wa kifo katika maisha yaliyojaajali, magonjwa, vita na mauaji mengineyo. Twaweza kuamini kuwa matukio haya yatawakumba wengine lakini si sisi, ama tutashindwa kujijasirisha kuendesha magari, ama kutoka nje ya nyumba zetu...hakuna anayetaka kufa lakini kifo ni lazima.

Maelezo ya mtaalamu huyu yanatubainishia kuwa mwanadamu anaishi kwa hofu ya siku ya kufa kwake. Anapoona wenzake wakifa huingiwa na kihoro na misukosuko tele. Maisha humvutia zaidi kuliko mauti ambayo anajua yatamkumba na kumharibia starehe zake. Lakini hawezi kukiepuka kifo kwa namna yoyote kwani ni kitu ambacho kimekita mizizi kwa kuwa huua watu kupitia ajali, vita, magonjwa na mauaji. Endapo mwanadamu atahofia kuzungumzia swala la kifo basi atahofia hata kuendesha gari.

Kastenbaum (1975) anaonelea kuwa kifo kinaweza kutazamwa kijamii, kuwa watu wamekufa kijamii endapo tumeacha kuwahudumia kama watu na tukaanza kuwatazama kama vitu visivyo na akili na visivyo na hisia. Utu wa binadamu ni kuwahudumia watu wengine na kuwathamini kwa umuhimu wao. Kama tutawafanya wengine wawe watumwa, tutawadhulumu na kuwanyanya basi tutakuwa tumewaumbua na hivyo basi kusababisha kifo chao kijamii. Japokuwa wako hai bila hadhi zao, huko ni sawa na kufa au kutokuwepo kwao. Mtu ni utu. Utu

wake ukiondolewa si mtu tena bali hubaki kuwa kama hayawani. Hayawani ni kiumbe asiye na thamani katika maisha, ni doa kubwa ambalo lafaa kuepukwa kwa kila hali. Russeu (1979) anasadiki uumbuaji huu wa utu wa mwanadamu hutokea pale tunapoanza kuzungumzia mambo kuhusu mtu anayekufa badala ya kuzungumza naye huyo mtu anayekaribia kufa. Hivyo basi kifo kijamii hutokea kabla ya kifo halisi cha mtu binafsi.

Inaelekea kuwa maelezo haya yanaonyesha swala la kifo kama tukio la kidhahania ambalo halishikiki bali huhisika tu. Huu ni mkondo ambaa ni tofauti na ule ambaa tumechukua katika utafiti wetu. Utafiti wetu uligundua kuwa kifo ni swala halisi ambalo hutokea katika maisha ya mwanadamu na huweza kuelezeza katika fasihi.

2.6 Mjadala wa kifo katika fasihi ya Kiswahili

Swala la kifo katika fasihi ya Kiswahili limewahi kujadiliwa na wanazuoni kwa kulitaja tu kwa ujumla wake mionganini mwa maudhui mengine na wakati mwengine kwa kuliangazia katika kazi moja ya sanaa ya jamii au mtunzi fulani. Mawazo mengine hujitokeza katika wasifu wa baadhi ya watunzi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi inadhihirika kuwa swala hili halijadiliwa kwa kina kama tukio la kipekee na la aina yake katika fasihi ya Kiswahili hususan ushairi andishi. Utafiti huu ulinuia kurekebisha hali hiyo kwa kumulika swala hili kwa kina.

Robert (1967) anaona kufa kama ni mapito au ngazi zinazovukwa na maisha ya mwili, roho zinavuka ng'ambo ya pili ambako upeo wa macho hauwezi kufika wala mwito wa mwanadamu hauwezi kusikika. Hapa anadhihirisha kuwa hata baada ya kufa kuna kuishi kwa namna nyiningine, si kwa mwili dhahiri bali kwa roho. Mwili dhahiri hubaki duniani ukazikwa na

kusahaulika sura na matendo yake. Mawazo haya ya Robert ni muhimu kwani yanatupa mwanga wa kutuelekeza kuhusu fasiri ya kifo kwa mujibu wa mtaalamu huyu. Hata hivyo hatuelezi kwa kina jinsi kifo kile kinavyoathiri wafiwa. Maoni yake pia yalijitokeza katika wasifu wala sio ushairi. Utafiti huu nao uliazimia kuchanganua taswira ya kifo ambayo ilitupatia uwezo wa kupata athari yake kama ilivyowasilishwa katika mashairi teule ya Kiswahili.

Turuka (1971) anatueleza mengi kuhusu historia na maendeleo ya mashairi huku akitaja maudhui mbalimbali yazungumzwayo katika mashairi kwa kudokeza ubeti mmoja ama beti chache kuthibitisha hayo. Kuhusu kifo anatutolea ubeti mmoja tu wa shairi la Mnyampala akiomboleza kifo cha mshairi Shaaban Robert. Uchanganuzi wake huu haukuwa pana ili kuangazia mambo mbalimbali kuhusu kifo. Vilevile uchambuzi wake si wa kina kama ambavyo utafiti huu ulivyoangazia swala hili katika mashairi teule ya Kiswahili.

Chiraghdin (1971) anapochambua *Inkishafi* anaeleza kwamba mauti yamekaa kama mtu mshari anayewaacha wenyewe maisha walewelewe na raha za maisha, ndipo anapofyauta mshale wake na kufuma, na jinsi alivyo mkorofî wa shabaha, akifuma hakosi. Kisha anaendelea kufafanua, ‘ajabu ni kwamba daima, na karibu katika mashairi yote mauti huambiwa yanakuja ghafla, licha ya kuwa kila mmoja wetu anajua ni hatima tusiyo na budi nayo, kwa hivyo pengine ingepasa daima kuiweka machoni’. Hapa ni bayana kwamba kifo ni kitu tulicho nacho na kina shari na dhiki tele. La ajabu zaidi ni kwamba kifo hakibagui. Anaendelea kueleza kuwa ikiwa kiko chochote kile chenye katiba ya usawa wa mwanadamu basi ni mauti, kwani mbele yake, mwana wa pazi ni sawa na mwana-duni, tajiri ni sawa na maskini, mjuzi sawa na mjinga. Chiraghdin (1987) anasisitiza mawazo haya kwa kueleza kuwa mtunzi wa *Inkishafi* anaonyesha kuwa dunia siyo

makao ya binadamu, ila ni mapito tu ya kwenda ahera. Hivyo basi wote waliomo duniani watapitia mauti kama njia ya kuwafikisha kule ahera, wote, bila ubaguzi. Utafiti wetu kwa upande mwingine ulilitazama swala la kifo katika tungo teule za mashairi ili kuibuka na mtazamo angavu kuhusu kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

Mlamali (1980) anatuchambulia kifalsafa kuangamia kwa mji wa Pate pamoja na watu wake. Uchambuzi huu ni mzuri na unatuangazia zaidi katika mada ya utafiti huu ili kuchanganua kifo jinsi kinavyowasilishwa katika mashairi teule ya Kiswahili. Mtaalamu huyu alijikita katika utenzi wa *Inkishafi* pekee na kuweka mjadala wake kwenye misingi ya falsafa ya mtunzi wa utenzi huu. Utafiti wetu uliangazia kifo katika uhalisia wake kwa misingi ya historia ya mwandishi pamoja na mazingira yake.

Msami (1982) anatueleza kuwa dunia sio makao yetu ya kudumu, bali sote, maskini na matajiri, tunapita njia hiyo, na iko siku ambayo tukipenda tusipende, tutawacha dunia twende mbele ya hukumu kuu ya Mungu. Maelezo haya yanatudhihirishia kuwa kifo ni hatua ya kumfikia Mungu baada ya mapito haya ya dunia. Mtaalamu huyu anatuelekeza katika ulimwengu wa kesho (ahera) ambao haufikiwi na walio duniani mpaka siku ya mauko wakafika mbele ya hukumu ya haki. Kufa hapa basi ni lazima kwa wote wala hakuna atakayebaki pindi siku ya mwisho itakapofika. Mawazo haya yanajenga falsafa ya kifo katika misingi ya dini ambapo mwanadamu anaonyeshwa kuwa ajiandae kwa hukumu ya matendo yake duniani kule mbinguni. Kisha Msami anaendelea kutueleza kuwa: ‘Mtu asiyewapa wanawe elimu atakuwa awaua kifo cha uhai’. Maana na mawanda ya kifo hapa yamepanuliwa kutoka kwa kifo cha mwili na kuingia katika kifo cha kiakili. Yamkini hapa ni dhahiri kuwa elimu hulinganishwa na maisha na akosaye

elimu ni sawa na aliyekumbwa na kifo maana amepokonywa uzuri wa kuishi na fanaka ya elimu bora. Mtaalamu huyu anatuelekeza katika kubaini aina za vifo, kwamba kuna kufa kwa aina nyingi wala sio tu kufa kwa mwili. Mawazo haya yanatupanulia mtazamo wa kifo na hivyo kuupa nguvu utafiti huu kugundua visababishi vya kifo vinavyotokea katika mashairi teule ya Kiswahili.

Mbaabu (1985), akishughulikia utamaduni wa Waswahili, ameonyesha namna mazishi hufanywa baada ya mtu kufa. Hapa amedhihirisha mwingiliano wa kitamaduni baina ya Uislamu (dini) na Uswahili. MBAABU ameonyesha baadhi ya itikadi na imani za Waswahili kuhusiana na kifo. Imani mojawapo ni kwamba 'bundi akilia juu ya nyumba anatangaza kifo'. Imani hii ipo na inadhihirika katika baadhi ya kazi za watunzi wa Uswahilini kama vile Mohamed (1980; 1988). Lakini mtaalamu huyu hatuelezi ni kipi wanachofanya wanajamii kifo kinapokuja. Hatuelezi shughuli ama mambo wayafanyayo ili kukabiliana na kifo. Hali kadhalika mawazo yake yamejikita tu katika jumuiya ya Waswahili pekee katika imani na itikadi zao, tofauti na mkondo ambao utafiti huu ulichukua kuchunguza kifo katika mashairi teule ya Kiswahili huku ukijua kwamba watunzi wa ushairi wa Kiswahili hutuangazia namna sanaa inavyoweza kutumiwa ili kuangazia matukio katika jamii kwa duru ya wakati.

Shariff (1988) amefafanua tungo mbalimbali za Waswahili katika uwanja wa ushairi. Pia ametupatia nafasi na majukumu ya tenzi. Hata hivyo maudhui katika tungo hizi hayajajadiliwa kwa undani ila yametajwa hapa na pale pasi na uchambuzi wa kina uliowekwa kwenye misingi ya kinadharia. Kuhusu kifo, mtaalamu huyu ametaja mashairi ya majonzi yanayojitokeza katika mashairi mengi ya Kiswahili pasi na kujikita kwa kina katika swala la kifo. Amejumuisha kifo

katika maudhui ya majonzi ambayo ni ya jumla sana. Mtaalamu huyu aliangazia pakubwa historia na maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Huu ni mwanya ambao utafiti wetu unalenga kuziba kwa kuchambua uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili kupitia misingi ya nadharia ya uhalisia.

Wataalamu Gibbe (1990), Madumulla na Khamis (1989) na Khatib (1985), licha ya kuwa wameshughulikia tenzi maarufu za Kiswahili, wamechambua kwa kina usanifu na ukamilifu wa tenzi hizo katika matumizi ya lugha katika kuchora maudhui. Ijapokuwa tenzi zimezumgumzia kifo, maudhui haya hayajaangaziwa kwa kina na wataalamu hawa. Utafiti wetu ulilenga kuangazia kwa mapana na marefu tukio hili la kifo kama wanavyowasilisha watunzi wa mashairi teule ya Kiswahili.

Njozi (1992) licha ya kwamba anajadili utenzi ulioandikwa kwa Kiswahili, mjadala wenyewe upo katika Kiingereza. Mtaalamu huyu anatusimulia mawazo hasi na chanya kuhusu nafasi ya *Utenzi wa Mwana Kupona* katika ukombozi wa mwanamke. Hatupatii lolote kuhusiana na maudhui ya kifo japo kifo kimesimuliwa pakubwa katika utenzi huu. Utafiti wetu unashikilia kuwa kifo ni swala nyeti katika utungaji wa utenzi huu ambao ni kama wosia wa mama kwa mwanawe. Mtunzi wa utenzi huu, Mwanakupona, alipoona afya yake imeanza kudorora na muda wake wa kuishi kukaribia kufa, alimtungia bintiye utenzi huu kama wosia kwake. Ni kutokana na dalili ya kuona kuwa kifo chake kinakaribia akaamua kutunga utenzi huu (Mulokozi 1999). Hivyo basi ni muhimu kulichanganua swala hili ili kupata kuelewa kifo kama msingi wa msukumo wa kuandikwa kwa utenzi huu.

Njogu (1997), akichambua riwaya za visiwani Zanzibar, anatuelezea mapinduzi yaliyotokea visiwani humo kama yanavyosimuliwa na waandishi wa riwaya hizo. Pia anatuonyesha matukio ya kifo kutokana na mapinduzi hayo. Hata hivyo hayajadili kwa misingi ya nadharia ya uhalisia kama tulivyofanya katika utafiti wetu. Halikadhalika utafiti wake ulijikita katika riwaya maalum za visiwani Zanzibar. Utafiti wake huu unatuangazia mwanga wa kupata kuchambua kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

Wafula (1999) anatueleza kwa usahili dhima ya ushairi katika kuongoza umma kutekeleza mapinduzi katika jumuiya ya *Kilio cha Haki*. Yeye haingii ndani katika uchambuzi wa mashairi ambayo ndiyo yaliyotumika katika ujenzi wa tamthilia hii. Mashairi haya yanaonyesha majonzi na masikitiko pamoja na ukiwa unaoletwa na mauti. Wahusika wa tamthilia hii ambao walishikwa na mhemko wa kujikomboa wanaonyesha kuwa wako radhi kufa. Mateso na mahangaiko wanayoyapata na misiba imejengwa na kuwasilishwa kishairi lakini swala hili la matumizi ya mashairi ya misiba katika tamthilia hii halijaangaziwa. Utafiti wetu ulichunguza tukio la kifo katika mashairi teule ya Kiswahili kama taaluma huru.

Jambo moja ambalo fasihi hutuwezesha kuelewa ni kuwa, kifo humaanisha vitu tofauti kwa watu tofauti katika nyakati mbalimbali. Dhana ya kifo katika fasihi ni pana na ina fasiri nyingi mionganoni mwa wanajamii. Kifo pia ni swala halisia la kimaisha na mwanadamu hana uwezo wa kuepuka kifo pindi wakati wake ukifika. Uhalisia wa kifo hututisha na hivyo kutufanya tuenze kukwepa uhalisi huu kwa kujipa moyo wa uwepo wa maisha baada ya kifo na kutokuwepo kwa kifo cha milele bali maisha ya kudumu baada ya kufa. Kila mara mwanadamu hujipumbaza kwa kufikiria kuwa kifo chake bado kiko mbali lakini anasikitika pakubwa pindi anapofiya na

mwandani wake. Hapo ndipo anapoanza kufikiria namna ya kujinusuru ili asije akapigwa na kumbo la kifo ambalo ni bayana kuwa hawezi kulikwepa

2.7 Hitimisho

Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa ni bayana kuwa swala la kifo ni tata na limeshughulikiwa kwa upeo wa chini katika ushairi wa Kiswahili. Hivyo basi utafiti huu uliazimia kuliangaza hili swala kwa kina kwa kuliegemeza kwenye misingi ya nadharia ya uhalisia. Halikadhalika utafiti huu utajikita katika mashairi teule ya Kiswahili ili kutoa mtazamo mpana kuhusu dhana ya kifo namna washairi hawa wanavyoiwasilisha. Dhana ya kifo haina maana moja maalum. Maana hubainishwa kutegemea taaluma mbalimbali.

SURA YA TATU

NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

Katika sura hii tumetoa maelezo kuhusu utaratibu wa utafiti huu. Tumeeleza muundo wa utafiti, njia ya utafiti, usampuliishaji, mbinu za ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data.

3.1 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ulijikita katika muundo wa kiuchanguzi wa matini. Muundo huu hujikita katika kujibu maswali kama vile wapi, jinsi gani, nani na lini? Muundo huu ultumika kwa sababu husaidia katika kupata majibu yanayoafiki uchanganuzi wa kimatini kama tulivyofanya katika utafiti wetu.

3.2 Njia ya utafiti

Ili kufikia malengo ya utafiti huu, njia ya maktaba ilitumika. Utafiti maktabani ulifanywa kwa kusoma, kudurusu, kuchanganua na kutathmini maandishi mbalimbali yanayozungumzia suala la utafiti. Njia ya kipekuzi pia ilijumuishwa ili kusaidia katika kutalii kwa kina mashairi yaliyoteuliwa katika utafiti wetu. Njia hii ni nzuri katika kueleza swala la kimaumbile kama kifo ambalo liko nje ya uwezo wa mwanadamu kama anavyoeleza Krathwohl (1993). Mtafiti alilazimika kuzuru maktaba ya vyuo vikuu na maktaba za umma. Kupitia njia hii mtafiti aliweza kukusanya data inayofaa na inayolenga kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Njia ya maktaba pamoja na upekuzi pia zilihusu kusoma kwa kina mashairi mengi ya Kiswahili na kuchagua mashairi yanayozungumzia kifo. Usomaji wa mashairi haya ulitoa msingi mwafaka wa kuhakiki

uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Ili kuweza kupata maelezo ya ziada mtafiti alisoma majarida, vitabu na makala iliyo na maelezo kuhusu kifo. Mtando pia ulitumika ili kupata maelezo ya ziada kuimarisha utafiti huu. Data zote zilizopatikana zilichanganuliwa kwa kurejelea madhumuni ya utafiti kuchanganua kwa uwazi dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

3.3 Kikundi Lengwa

Utafiti huu ulilenga mashairi teule ya Kiswahili ambayo ni *Inkishafi, Utenzi wa Mwana Kupona* na shairi la ‘Usiniuwe’ kutoka katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Diwani hizi zote zinazungumzia swala la kifo kwa mapana na mrefu. Shairi la ‘Usiniuwe’ katika Sauti ya Dhiki pia limesukwa kwa ufaafu zaidi katika kuwasilisha dhana ya kifo.

3.4 Uteuzi wa sampuli

Kuna mashairi mengi yanayozungumzia dhana ya kifo katika viwango mbalimbali. Lakini utafiti huu uliangazia usampulishaji wa kimakusudi wa tenzi mbili na shairi moja ambalo linazungumzia kifo ili kusaidia katika utimizaji wa madhumuni na malengo ya utafiti. Kama wanavyoeleza Mwanje (2001) na Kombo na Tromp (2006) kuwa usampulishaji wa kimakusudi huzingatia na kuteua kile ambacho kina sifa zinazolengwa na utafiti, tuliyateua mashairi ambayo yaliafikiana na madhumuni ya utafiti wetu. Usampulishaji huu ulijumuisha tenzi mbili ambazo ni *Inkishafi* na *Utenzi wa Mwana Kupona* na shairi moja ‘Usiniuwe’ kutoka diwani ya *Sauti ya Dhiki*, hili ndilo shairi pekee ambalo linazungumzia kifo katika diwani hii. Tingo hizi zilichaguliwa kwa misingi kuwa zina upeo wa juu wa lugha na fani za utunzi wa mashairi kwani

ni tungo zinazoakisi urasimi. Tenzi hizi mbili ziliteuliwa kutokana na upekee wa mitindo yao ambayo imekwepa kusimulia maswala ya kishujaa kama utenzi wa *Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* na *Utenzi wa Ras l'Ghuli*. Shairi lililoteuliwa pia ni refu kwani lina beti ishirini na tisa na hivyo kutoa uwanja mzuri wa kuwasilisha dhana tata kama kifo. Mashairi haya pia yanachukua vina sawia katika kibwagizo au bahari. Vina hivi vinajenga vema dhana ya kifo katika mashairi haya kwa kuonyesha hali ya mwanadamu kukata tamaa ya kuishi na kujisalimisha kwa kifo.

3.5 Mbinu za ukusanyaji wa data

Utafiti huu kimsingi ulikuwa wa kimaktaba. Usomaji na uchanganuzi wa matini ulifanywa. Ulianza na usomaji kimsingi wa matini yaliyopo maktabani na yanayozungumzia dhana ya kifo. Kwa hali hii utafiti huu uliweza kupata mwangaza kuhusiana na dhana ya kifo. Usomaji wa matini haya ulihusisha unakili wa mashairi yaliyoteuliwa kwa shughuli ya kutimiza malengo ya utafiti. Hoja muhimu kuhusu mashairi haya zilinakiliwa.

3.6 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data

Uchanganuzi wa data ulijikita katika mashairi teule ya Kiswahili ili kubaini uhalisia wa kifasihi na uhalisia wa kimaisha kuhusiana na dhana ya kifo kama wanavyowasilisha watunzi wa mashairi haya yaliyoteuliwa katika Kiswahili. Data zilizokusanywa ziliwekwa pamoja kwa kuzingatia maswali na malengo ya utafiti. Kipengee cha lugha kilitumika kutuongoza katika kung'amua uteuzi wa misamiati ambayo yanajenga taswira mbalimbali za kifo katika mashairi

yaliyoteuliwa. Mazingira ya mtunzi pia yaliteweza kuelewa mchango wa tajriba ya mwandishi pamoja na vielelezo vilivyotumika ili kuibua visababishi vyatano na utata unaoibuka katika ufasiri wa dhana ya kifo. Kwa hali hii uhalsia wa fasihi na uhalsia wa kimaisha uliweza kubainika. Usomaji wa matini teule na mengine yanayohusiana nayo pamoja na uchanganuzi wa kina ulifanywa ili kujenga msingi wa uchanganuzi wa kithamano. Uhariri wa data ulifanywa kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa ni sahihi, kamilifu na zinakubalika. Hatimaye data zilijumlishwa pamoja kwa njia ya jedwali iliyorahisisha utoaji wa matokeo kuhusiana na suala la utafiti huu. Waaidha tulijumuisha pia mawazo ya Truex (1996) ambaye anathibitisha kwamba njia ya uchanganuzi matini ni muhimu kwa utafiti wetu kwani inatupatia nafasi ya kuhakiki kwa makini vipengele vyatano kimazingira na muktadha namna vinavyojitokeza katika sanaa husika. Njia hii ilisaidia utafiti huu kudhihirisha umuhimu wake na hivyo maelezo mwafaka kuhusu swala la utafiti yaliweza kutolewa na malengo ya utafiti kutekelezwa kikamilifu.

SURA YA NNE

MAWANDA YA KIFO KATIKA MASHAIRI TEULE YA KISWAHILI

4.1 Utangulizi

Sura hii imejaribu kuyajibu maswali ya utafiti wetu ili kutimiza madhumuni yetu ambayo yalilenga kuchanganua taswira ya kifo, visababishi vyakifo na utata unaojitokeza katika fasiri ya dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Tumetangulia kuangalia muhtasari wa diwani tulizoziteua katika utafiti wetu ili kutoa mwangaza juu ya diwani hizi. Hii ni kwa sababu kuna machapisho tofauti ya diwani hizi haswa zile za tenzi zilizoteuliwa ambayo hudhifiri tofauti za idadi ya beti katika mkusanyiko wa utenzi fulani. Kwa mfano, utenzi wa *Inkishafi* hudaiwa kuwa na beti sabini na saba au sabini na tisa. Mulokozi (1999) anadai kuwa tenzi hizi zina athari ya lafudhi za wakusanyaji wao. Hata hivyo ilitubidi tutumie machapisho ya tenzi za hivi karibuni ambayo tuliweza kuyapata maktabani. Imebainika kuwa namna kifo kinavyosukwa na kuwasilishwa katika mashairi ya Kiswahili ni ya kipekee na hivyo hutupatia picha mbalimbali za kifo namna wanavyowasilisha watanzi wa mashairi teule ya Kiswahili. Tuligundua kuwa kifo ni kitu cha kutisha, hakipendwi, kinatamausha, ni faradhi, humkumba kila kiumbe, ni kazi ya ibilisi, hakibagui, kina upweke na sio mwisho wa maisha. Mazingira ya mtunzi pia humsaidia katika kujenga taswira ya kifo. Hali hii hujitokeza katika wakati, dini au utamaduni, elimu na lugha.

Sura hii vilevile imeangazia utata unaoibuka katika fasiri ya dhana ya kifo huku ikionyesha namna uhai na kifo vinavyoingiliana kiasi kwamba kunaibuka ugumu wa kubaini mwanzo na mwisho wa kila mojawapo. Kifo na uhai ni mfano wa roho na kiumbe, vinategemeana na

kukamilishana. Bila uhai hakuna kifo, na bila kifo basi uhai hauna maana yoyote kwetu. Kifo ni kinyume cha uhai, na uhai ni kinyume cha kifo. Huu ndio utata unaomkumba mwanadamu maishani. Ili kuelewa utata huu mwanadamu huwasilisha mawazo yake kisanii ili kujipa uwezo wa kung'amua na kujaliza maana ya maisha. Katika utafiti wetu wa mashairi teule ya Kiswahili tuligundua kuwa utata wa ufasiri wa kifo hujitokeza katika mambo yahusianayo na kifo na mwisho au mwanzo wa maisha. Haya hujitokeza katika mambo kama vile adhabu na kuzawadiwa peponi, mazungumzo na Mungu, utabaka, ufufuo au kuzaliwa upya, uteuzi wa misamiati na mwanzo wa maisha. Vilevile sura hii imeangazia visababishi vyta kifo ambavyo tulibaini kuwa ni Mungu, shetani na mtu kwa mtu.

La ajabu ni kwamba licha ya ukweli wa kuwepo kwa kifo, mwanadamu hakati tamaa ya kuishi, ameshika kani kujiruzuku ili aishi na apate raha duniani. Akumbwapo na kifo huwa anashtuka na kushikwa na majonzi huku akiona kuwa kifo kinamwonea na kumdhulumu bila ya kiasi. Anaona kuwa maisha ni matamu na kifo ni adui wa maisha hayo matamu. Kifo ni mshindani mkuu wa maisha na hujigamba kwa kuwaliza walio na maisha ambao wamejaa tadi na inda kiasi cha kusahau kuwa haya maisha yanaisha kweli na kifo kuchukua usukani.

Kifo kinajitokeza kama kiumbe hai. Kina uwezo wa kuchukua na kuangamiza maisha. Akili ya mwanadamu haichoki kujisaili maswali sampuli kwa sampuli kuhusu kifo ambacho hakipendwi lakini kimeshika kani kushindana na maisha. Kifo kinajidhihiri kama nduli mkubwa mwenye uwezo wa kutenda mengi nje ya uwezo wa maisha.

4.2 Diwani teule za ushairi wa Kiswahili

Sehemu hii inatoa ufanuzi mwafaka kuhusiana na diwani teule za tungo zilizoshughulikiwa katika utafiti huu. Kwa kila mojawapo tumeonyesha lini na wapi ilipata kutungwa na kuchapishwa. Diwani hizo ni pamoja na *Inkishafi*, *Utenzi wa Mwana Kupona* na *Sauti ya Dhiki* ambayo ndani yake tulichagua shairi moja la ‘Usiniwe’.

4.2.1 Inkishafi

Utenzi wa *Inkishafi* ni miongoni mwa tenzi za zamani za Kiswahili. Kwa mujibu wa Mulokozi (1999) kuna madai kuwa utenzi huu ulitokana na tungo za Kiswahili za zamani ziitwazo ‘Qala Shair al-Muhadhar’ na ‘Ayuha al-Maghururi’. Nakala ya zamani zaidi ya utenzi huu ni ya 1853 (Hichens 1972). Baadhi ya wataalamu ambao wameshughulikia utenzi huu ni Taylor (1950), Hichens (1972), Allen (1945), Harries (1962), Allen (1977), Knappert (1979) na Mlamali (1980). Gibbe (1994) na Shitemi (1997) wamewahi kuiandikia tasnifu lakini wote hawa hawakushughulikia swala la kifo linalotawala katika utenzi huu mzima.

Mulokozi (1999) anadai kuwa utenzi wa *Inkishafi* ndio utenzi maarufu zaidi katika tungo za tenzi za Kiswahili kutokana na upeo wa lugha yake na mkondo wa usimulizi wake ambao ni uzungumzi nafsi. Utensi wa Inkishafi ni utungo wa kidini unaovuka mipaka ya dini moja. Pia umaarufu wake unatokana na kule kukwepa mtindo wa tenzi kuzungumzia maswala ya mashujaa na mambo yahusianayo na utawala na siasa. Utensi huu unatokana na neno la Kiarabu ‘inkishaf’ lenye maana ya ‘uzinduzi’ au ‘ufunuo’ wa moyo. Hichens (1972) anasema kuwa inkishafi humaanisha ‘kujifunua kwa nafsi ya mtu kwa nafsi yenyewe’, ilhali Jahadhmy (1975) anadai kuwa inamaanisha ‘kufichua’ naye Allen (1977) anasema kuwa ni ‘kujiangalia upya’ au

‘kujifunua’. Inabainika kuwa inkishafi ni tafakari ya mtu na moyo wake. Uzinduo wake ulijikita katika kuanguka kwa mji wa Pate ambao ulikuwa maarufu katika mwambao wa Afrika Mashariki. Hivyo basi ni zao halisi la historia ya Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1999), mgogoro mkuu uliozaa utenzi huu ni kule kuanguka kwa ustawii wa miji ya Waswahili katika mwambao wa Afrika Mashariki kulikosababishwa na uvamizi wa wageni kutoka Ureno (k. 1500-1700) na baadaye Oman (kuanzia 1700). Wavamizi hawa walisababisha kuanguka kwa miji hii kutokana na vita vya mara kwa mara na pia kuitawala kiimla. Yamkini mtunzi wa *Inkishafi* alishuhudia kipindi cha mwisho cha kuanguka kwa mji wa Pate na kumwathiri kuisawiri hali yake kishairi katika utenzi huu ili kutoa nasaha kwa moyo wake.

Mulokozi anazidi kueleza kuwa, kuna madai kuwa utenzi wa *Inkishafi* haukukamilika na beti mbili zilizomalizia utenzi huu ni nyongeza ya kazi ya mtunzi mwingine. Hii ni kwa sababu mtunzi alidhamiria kututungia kidani lakini anafikia beti 77 na pia majina yote ya Mungu hayajatajwa ili yatimie 99 jinsi tuyajuavyo katika dini ya Kiislamu. Endapo haukukamilika basi tunaweza kukisia kuwa mtunzi alifariki kabla ya kumaliza utunzi wake ama baadhi ya beti za mwisho zilipotea. Watetezi wa hoja ya kuwa *Inkishafi* haikukamilika wanadai kuwa maneno “koja” na “kifungo” katika ubeti wa 7 na 8 yana maana ya tasbihi, ambayo aghalabu huwa ni punje za shanga 99. Hivyo mtunzi alikusudia kutunga beti 99. Vilevile wanaongeza kuwa utenzi huu mwishoni hauna beti zinazotaja jina la mtunzi, kumtukuza Mungu na kumwombea Mtume Muhamad kama ilivyo kawaida, na huo ni ushahidi kuwa utenzi haukukamilika. Mlamali (1980) anapinga hoja zinazotolewa kuhusu kutokamilika kwa utenzi wa *Inkishafi* kama wanavyodai

baadhi ya wataalamu. Anadai kuwa neno “kifungo” si lazima liwe na maana sawa na “tasbihi”, linaweza kuhusu kidani chochote tu, na kumtaja Mungu ama Mtume katika utenzi ni mila tu, si lazima.

Utenzi huu ilitungwa na Sayyid Abdallah Bin Ali Bin Nasiri ambaye anakadiria kuishi baina ya 1720-1820 (Hichens 1972). Naye Chiraghdin (1987) anakadiria kuwa mtunzi huyu aliishi baina ya 1718-1815. Ni bayana kuwa mtunzi huyu aliishi katika karne ya 19. Mtunzi huyu inasemekana kuwa alikuwa na uhusiano na Sayyid Idarus aliyetunga Hamziyya (Hichens 1972). Mbali na *Inkishafi* alitunga pia *Takhmisa ya Liyongo au Wajiwaji*. Mtunzi huyu alitokana na ukoo wa malenga farisi wa Kiswahili wenye asili ya Hadhramaut kule Yemen. Katika utafiti wetu tumetumia nakala ya utenzi wa *Inkishafi* iliyokusanywa na Mlamali (1980) na Mulokozi (1999).

4.2.2 Utensi wa Mwana Kupona

Utenzi huu ilitungwa na Mwana Kupona Binti Mshamu kwa ajili ya binti yake aliyejulikana kama Mwana Hashima Binti Mataka katika mwaka wa 1275H (1858M). Utensi huu pia umetumiwa sana katika asasi za unyago miongoni mwa Waswahili kwani umejikita katika mawaiha kwa mwanamke ili kumpa mwongozo wa vile anavyofaa kuishi na mumewe katika ndoa.

Mwana Kupona Binti Mshamu Nabhani alizaliwa Pate mwaka wa 1810. Mwaka wa 1836 aliolewa na Bwana Muhammadi Is-Haq Bin Mbarak (k. 1799-1856) aliyejulikana kwa jina la Shee Mataka. Shee Mataka alikuwa mtawala wa Siu na mpinzani mkubwa wa utawala wa Sultan

wa Zanzibar. Mwana Kupona na Shee Mataka walifanikiwa kupata watoto wawili: Mwana Hashima Binti Mataka (1841-1933) aliyetungiwa utenzi huu, na Muhammadi Bin Shee Mataka baina ya miaka ya (1856-1858). Mwana Hashima aliolewa mara mbili na alizaa watoto wawili ambao pia waliishi Lamu. Alifariki mwaka wa 1933.

Mulokozi (1999) anadai kuwa inasemekana Mwana Kupona aliutunga utenzi huu akiwa mgonjwa wa maradhi ya tumbo la uzazi. Alihisi kuwa asingepona, hivyo akaamua kuutunga utenzi huu ili uwe ni wosia kwa binti yake ambaye angebaki bila uongozi wa mama. Mwana Kupona hakupona, alifariki mwaka wa 1860, miaka miwili baada ya kutunga utenzi huu.

Utenzi huu uliwahi kuchapishwa na Hichens (1934), Harries (1962), Allen (1971) na Amina Abubakar Sheikh na Ahmad Sheikh Nabhany (1972) na Jahadhmy (1975). Mjadala mkubwa kuhusu utenzi huu kwa muda mrefu umehusisha wataalamu wa fasihi ya Kiswahili wakiangalia udunishaji wa mwanamke na kufaa au kutofaa kwa utenzi huu katika enzi zetu. Baadhi ya wataalamu hao ni Mulokozi (1982) na Ndulute (1988) ambao wote wanaona kuwa ni utenzi unaoendeleza kasumba ya waume kuwadunisha wake zao na hivyo kumdhilishwa mwanamke kwa ujumla. Wenyе mtazamo kinzani nao ni kama Njozi (1992) na Mbele (1985) wanaoutazama utenzi huu kama mwongozo mwema wa kitamaduni unaomkuza mwanamke na kumdhilishwa mwanamume. Gibbe (1993) naye anachukua mkondo wastani wa mitazamo ya wataalamu wote hao. Kama ilivyojitokeza katika *Inkishafi*, hapa pia swala la kifo halijapewa mwangaza na wataalamu walioutafitia utenzi huu licha ya kuwa limezungumziwa pakubwa na mtunzi wake. Utafiti wetu uliteua nakala ya utenzi huu uliokusanywa na Mulokozi (1999) ili kuwa chanzo cha data yetu. Hii ni kwa sababu beti za nakala hii zimekamilika beti zake.

4.2.3 Sauti ya Dhiki

Diwani hii iliandikwa kizuizini na mtunzi Abdilatif Abdalla na kuchapishwa na shirika la uchapishaji la Oxford mwaka 1973. Mtunzi Abdilatif Abdalla alizaliwa mwaka wa 1946 Mji wa Kale (Mombasa) katika mtaa wa Kuze. Alisoma Faza (Rasini), kisiwa kilicho karibu na mji wa Lamu kabla kuja baadaye kumaliza masomo yake ya msingi katika eneo la Takaungu.

Abdilatif Abdalla aliwahi kufungwa (1969-72) kutokana na msimamo wake wa kisiasa dhidi ya serikali ya rais wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya. Alisingiziwa kuchochea watu dhidi ya utawala wa Kenyatta kutokana na kuchapishwa na kusambazwa kwa makala yake ilioitwa: ‘Kenya, twendapi?’ Alipelekwa katika jela ya Shimo la Tewa na baadaye Kamiti na kule jelani ndiko alikotunga *Sauti ya Dhiki*. Mashairi yaliyomo yanadhihirisha dhiki kuu aliyokuwa nayo kifungoni. Mojawapo ya mashairi hayo ‘Usiniuwe’, lilitewa kushughulikiwa katika utafiti huu kwani ndilo pekee linazungumzia kifo tena kwa kina na upeo wa juu. Shairi hili pia linazungumzia kifo kwa urefu na lina kina cha ‘ya’ katika kibwagizo chake kinachooana na kina cha tenzi za *Inkishafī* na *Utenzi wa Mwana Kupona* ambazo tuliteua kushughulikia katika utafiti wetu. Kina hiki kinawasilisha vema hisia za uchungu na upweke wa kifo kwa mwanadamu. Yale mashairi mengine yanazungumzia maswala mengine kuhusu dhiki, upweke na mateso ya mtunzi kizuizini na kuonyesha matumaini yake ya kujumuika na watu wa familia yake na marafiki kwa ujumla.

Utangulizi wa diwani hizi zote unadhihirisha kuwa watunzi wote hawa wanahusiana kimazingira japo wametengwa kihistoria na kiwakati. Wote hawa ni Waswahili kindakindaki na waliwahi kuishi katika visiwa vya kaskazini mwa Kenya vinavyodaiwa na Chiraghdi na Mnyampala

(1977) kuwa chimbuko la Kiswahili na ushairi wake. Tungo zao zimetumia lahaja ya Kiamu na Kimvita ambazo ni lahaja kuu za Kiswahili na zilizotumika pakubwa katika utunzi wa mashairi. Vilevile wametumia mazingira halisia walimokulia ili kuzungumzia kifo. Tungo zao zote zina kina kinachofanana katika kibwagizo, kwani ni kina cha irabu au nusu irabu ‘ya’, ‘ye’, ‘wa’ na ‘a’ na hudokeza kule kutamauka au kukata tamaa kutokana na kifo au ugumu wa kuishi. Vina vya nusu irabu na irabu hutamkika kwa sauti hafifu, havina nguvu wala mrindimo bali vina unyoofu na ulaini wa kutumia pumzi chache wakati wa kuvitamka. Hali hii ni sawa sawa na mpumuo wa mtu anayekaribia kufa au aliyekata tamaa kwa kuzongwa na matatizo mengi ambayo ameshindwa kuyatatu. Kuhusu matamshi ya sauti na silabi zilizo na irabu, Mgullu (1999) anatueleza kuwa silabi wazi ni zile silabi ambazo huishia na irabu. Inaaminika kuwa matamshi ya irabu huwa hayakatiki kwa haraka kama yale ya konsonanti, na kwa hali kama hiyo silabi wazi huonekana kama ipo huru au wazi zaidi kwa sababu wakati wa kuitamka haikatizwi ghafla. Wakati wa kutamka irabu hewa huwa haizuliwi au kubanwa mahali popote. Kwa kawaida matamshi ya konsonanti hayaendelei kama yale ya irabu. Hukatika ghafla. Hivyo basi utokeaji wa silabi za irabu na nusu irabu kama vina vya mashairi tuliyoyateua huonyesha mwingiliano mwafaka wa uteuzi wa vina hivi na maudhui ya kifo ambayo yamewasilishwa kama kitu kilicho na upweke na kinachowatia watu huzuni kubwa.

Mulokozi (1989) anapochambua shairi la *Amina* la Shaaban Robert kuhusu swala la vina na maudhui katika shairi anasema,

Uteuzi wa vina labda unahusiana na maudhui ya shairi kuhusu kifo, na kusudi la mtunzi kulilia mpenzi wake. Hii ni kwa sababu kina cha kati ‘nga’ kinachotumika katika ubeti wa 1 na 3, na pia katika kibwagizo, kinatoa mlion wa sauti ya kuomboleza...kadhalika

kina cha ‘a’ kinachotokea mwishoni mwa mistari yote, na kinachotanguliwa na irabu/konsonanti laini (glides) za e, i, u, w...kinatoa mlion wa majonzi, wa maombolezo, hasa tunapolisoma au kuliimba hili shairi kwa sauti.

Utafiti huu ulibaini kuwa uteuzi wa misamiati maalum katika uwasilishaji wa dhana ya kifo huibua vina vinavyodokeza taswira anuwai ya kifo. Vina vyatia irabu na nusu irabu ndivyo vinajitokeza pakubwa katika vibwagizo vyatia mashairi yaliyoteuliwa na vinatoa mlion wa masikitiko na hofu ya mwanadamu dhidi ya kifo.

4.3 Taswira ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili

Dhana ya taswira imefafanuliwa kwa namna mbalimbali na wataalam wa fasihi. Senkoro (1982) anafafanua taswira kama mkusanyiko wa picha mbalimbali ziundwazo kwa maelezo ya wasanii katika fasihi; ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa kutumia ishara.

Senkoro anaangalia taswira kama picha zinazojitokeza kuitia maelezo ya msanii. Kila msanii ana njia tofauti atumiayo kueleza kitu kilekile tofauti na msanii mwingine. Hivyo taswira mbalimbali zitaibuka kutokana na maelezo tofauti ya msanii.

Allen (1971) naye anasema kwamba anatazama taswira kama ishara ya maneno yatumiwayo kuwasilisha kile kinachodhamiriwa na msanii. Anasema kuwa:

Maneno ya kiishara wakati mwingine hutumiwa kuwasilisha vitu ambavyo haviwezi kuelezeza bayana. Maneno haya hudokeza maana badala ya kueleza maana ya kinachoashiriwa. Maneno haya huvuta makini ya msomaji au msikilizaji. Mwandishi

hutumia lugha ya kiishara kwa kuwa hana namna nyingine ya kujieleza kwa uwazi zaidi ili apate kuelewaka.

Cuddon (1979) kwa upande mwingine anasema:

Taswira zote si lazima imaanishe picha ya akilini...kwanza, tunaweza kutofautisha kati ya (picha) halisi, (picha) ya kutambulika, na (picha) ya kidhana...Taswira nyingi (lakini si zote) zinaletwa na lugha ya kitamathali, kama vile katika sitiari, tashbiha, majazi, tanakali za sauti na taashira au menotumia. Taswira inaweza kuonekana..., kunusika..., kugusika..., kusikika..., kuonjeka..., kuwazika... au kufikirika..., na kujongeeka.

Vuzo (1999) anafafanua taswira kama:

Hali ya kuandika kazi kwa ufundu kiasi kwamba aliyeandika anajenga picha fulani akilini mwa msomaji.

Madumulla (2009) anadai kuwa:

Taswira ni sawa na picha. Akimnukuu Harthorn (1965) anasema kuwa kwa kawaida picha zinabainishwa na sifa halisi kuliko maana dhahania; kwa kawaida, picha zina sifa za kihisia zaidi kuliko ishara – zinaitisha kwa bayana kabisa akilini taswira za vionjo, harufu, mguso, sauti na muonekano wa vitu vilivyorejelewa.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa taswira hujitokeza kama picha, ishara inayosimamia maana ya kitu kile kinachorejelewa, hujengwa kutokana na maelezo ya mtunzi wa kazi fulani ya sanaa na huweza kugundulika kuitia akili na hisi nyinginezo za mwanadamu. Hisi hizi ambazo

zinamsaidia mwanadamu kugundua taswira fulani hutupatia aina za taswira ambazo ni pamoja na taswira za maono (picha ya kuwaza au kufikiria), mnuso (picha ya kunusa), mguso (picha za kugusa), usikivu (picha ya kusikia), mwonjo (picha ya kuonja). Kazi ya aina fulani ya fasihi huweza kuwa na aina zote au baadhi ya taswira hizi kwa viwango mbalimbali. Uzuri na udhaifu wa taswira mojawapo hutegemea maelezo ya mtunzi mmoja hadi mwingine na pia utanzu mmoja wa fasihi hadi utanzu mwingine.

Katika sehemu hii tumeangazia picha ya kifo tunayowasilishiwa katika mashairi teule ya Kiswahili. Kifo kimechorwa kwa njia mbalimbali katika mashairi teule ya Kiswahili. Taswira hii inabainika kuwa ni dhoruba ya kifo, kifo kinatamausha, uchungu wa mauti, kifo ni hatima ya kila kiumbe, upweke wa kifo, kifo si mwisho wa maisha na ukatili wa mauti. Usawiri wa kifo pia hujikita katika mazingira ya mtunzi ambayo hujitokeza katika vipengee vya wakati, dini au utamaduni na lugha.

4.3.1 Dhoruba ya kifo

Mwanadamu heshi woga. Woga wa dhara lolote maishani hutokana na kule kuamini kuwa atakufa. Kifo cha mwenzake kinamtia hofu kwa kujua kuwa hakuna taarifa wala wakati wala njia moja mahususi ya kufariki. Kifo huja kama mwizi na kumpoka uhai wake bila onyo. Huja kwa dhamira ya kunyakua na kutoweka na kitu chenye thamani kwa mwanadamu. Kitu chenyewe ni ghali na kikienda hakina badala yake. Maisha yana thamani ya juu kushinda lulu na dhahabu ama chimbo za yakuti au almasi ambazo mwanadamu huthamini na kuenzi kama vitu vinavyoonyesha ukwasi na starehe za maisha. Mtunzi wa *Inkishafi* anadhihiri dhoruba ya kifo akisema:

22. **Tandi la mauti likawakota**

Wakauma zanda na kuiyuta

Na dunia yao ikawasuta

Ichamba: safari! Muniukiye

Neno ‘*tandi*’ ni tanzi linalooashiria kunyonga. Kunyonga ni kipigo kikali na labda cha ghafla linaloonyesha ukatili kwa kiumbe. Kisha tunaambiwa kuwa ‘*wakauma zanda na kuiyuta*’, yaani wakapata taabu nyingi za kusikitisha. Dunia ikawasuta na kuwakejeli ili kuwaonyesha kuwa wao si kitu bali ni viumbe dhaifu! Yumkini tukio la kuanguka kwa mji wa Pate lilimtatiza mtunzi wa shairi hili kwani alishuhudia jinsi mji huu ambao ulikuwa umenawiri unaangamia na kuanguka. Hatima ya mji huu ni kufa kwa watu wake wote ambao walijulikana kwa wingi wa milki na ukwasi waliosheheni. Lakini kifo kilipokuja hakikubagua tajiri wala maskini, watawala wala watawaliwa, wote waliangamia. Maisha ya mwanadamu kila kuchao kuna tukio la kufa kwa matajiri na maskini sawia. Kifo hakina ubaguzi wala huruma. Hali hii ya mauti inatisha kiasi cha kumfanya kiumbe alie na kusihi mauti yasije yakamchukua ghafla. Katika shairi la ‘Usiniuwe’ kutoka *Sauti ya Dhiki* mtunzi anatupatia picha ya mtoto aliye tumboni mwa mamake akililia mauti yampe nafasi aishi:

29. Mauti! Nihurumiya, Mauti! ‘Sinitukuwe,

Lipi nilokukoseya? Hatuna vita mi nawe,

Toba! Nisikitikiya, nisalimisha na wewe,

Magoti nakupigiya, simsikize mamangu.

Taswira hisi au mguso inajengwa hapa katika ubeti huu. Matumizi ya alama ya hisi (!) baada ya neno ‘*mauti*’ huonyesha ule woga dhidi ya kifo na pia ule mpigo wa kitu wenye nguvu zaidi.

Vile vile tunapata kubaini uchungu wa mauti kwani huja kama kipigo kwa mwanadamu. Kifo kinatisha na kinamtia kihoro mtoto ambaye hajazaliwa. Kifo kinapokuja kinapiga kwa nguvu na kutatiza fikira za mwanadamu. Katika uhalisia wa maisha watu mara nyingi wanaweka mikakati ya kujikinga dhidi ya kifo. Kama kuna chochote ambacho huweza kusababisha kifo, mwanadamu hujitahidi kukikwepa kwa kila hali.

Kutokana na kusadiki kuwa kifo ni kitu ambacho hakina wakati wake maalum, mwanadamu hujiandaa kukabiliana na kifo kwa kuwaachia waliobaki wosia wenyewe nguvu na himizo kutenda wema. Mwanadamu ameishi akiona wenzake wakifa na hivyo kuona ni vema kuishi kwa udugu huku akijibari na maovu ambayo huleta maangamizi kwa roho. Mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* anamuusia binti yake kuhusu kifo hivi:

10. Penda nikupe kifungo,

Kizuri kisicho ongo,

Uvae katika shingo,

Utaona manufaa.

11. Yangu utakaposhika,

Mwanangu hutosumbuka,

Duniani utavuka,

Na akhera utakiya.

12. La kwanda kamata dini,

Faradhi usiikhini,

Na suna ikimkini,

Ni wajibu kuitiya.

*13. Pili uwa na adabu,
Na ulimi wa thawabu,
Uwe kitu mahabubu,
Kulla utakapongiya.*

*14. La tatu uwa sadiki,
Ushikalo ulithiki,
Mtu asoshika haki,
Sandamane naye ndiya.*

Mwana Kupona alikuwa katika mazingira ya dini ya Kiislamu na akaathiriwa na mafunzo yake kuhusu maisha ambayo aliamua kumuusia binti yake kufuata kikamilifu ili aishi vema duniani na ahera. Anasisitiza mambo ya kushika dini yakiwa ni pamoja na kuswali na kumhimidi Mungu na mitume, adabu na kutenda haki huku mtu akijitenga na wasiopenda haki. Dini hapa huwasilisha matumaini ya mwanadamu badala ya kukata tamaa ya kuishi duniani na akhera.

4.3.2 Kifo kinatamausha

Nenola-Kallio (1982) anasema kwamba kifo ni kitu ambacho mwanadamu hana budi kukabiliana nacho na kukikubali, kujiimarisha nacho na kupata maana yake. Wakati mwingine ni kitu kizuri badala ya maisha yaliyojaa shida na dhiki tupu. Jinsi tunavyomwona mhusika Martha, *Kwenye Ukingo wa Thim (uk. 12)* akisema:

Martha: Unavyotuona hapa, sisi ni maskini. Ndiyo maisha ya mwanamke. Unapoteza mume. Unapoteza maisha. Unapoteza kila kitu.

Kutokana na mateso anayokumbana nayo, mhusika huyu (Martha) anaona kuwa kifo ni afueni zaidi kuliko maisha ambayo yanampa dhiki chungu nzima. Anazidi kusema hivi katika uk. 26

Martha: Kweli kuna wakati hata mimi natamani ningekuwa maiti, simo katika maisha, nikaepukane na ujinga huu.

Kutokana na kauli ya mhusika huyu, kifo huwa kama dawa ya kumwepusha na kumpozu mtu machungu yanayoletwa na maisha. Maisha huonekana kama chanzo cha dhiki wala hamna la kufurahia. Kifo basi kikaonekana kama mfariji mwema kwa mtu mwenye dhiki.

Katika kazi nyingi za Kezilahabi inadaiwa kuwa wahusika wake wamekataa tamaa kwa kukosa kuona maana ya kuishi duniani mlimojaa dhiki na masumbuko kila wakati na kila mahali. Tunamwona mhusika Kazimoto katika *Kichwamaji* akijiua kwa kukosa matumaini ya kuishi. Vilevile anajisaili maswali mengi kuhusu maisha na maana yake na anapokosa kupata jibu mwafaka anaamua kuondoa uhai wake. Utamaushi huu wa wahusika wa Kezilahabi ni tofauti na utamaushi ambao tunaangazia katika mashairi teule ya Kiswahili. Katika mashairi haya tunakumbana na tahadhari anayopewa mwanadamu kutoshiriki dunia kiasi cha kusahau kuwa maisha haya yana mapito tu wala hayadumu na kuyashiriki ni kujitafutia maangamizi. Mwanadamu anapewa kiwango au mpaka wa kuishi na kushiriki mambo ya dunia asije

akajisahau. Huu ni mpaka ambao unamfunga na kumnyima uhuru wake wa kuishi bila woga wa kifo. Kifo kinapewa nafasi kubwa kumkumbusha ule ufupi wa maisha na ukosefu wa utamu wake duniani kwa watu wakwasi na maskini kwa pamoja.

Matumaini ya kuishi ni kule kuona mambo yakinyooka. Mambo yanapoanza kwenda sambejambe mwanadamu hukata tamaa ya maisha. Kifo ndicho kitu kinachomtamausha mwanadamu kuishi raha mustarehe duniani na hivyo kujivekea mpaka wa starehe ili amkumbuke muumba wake na maisha ya kesho ahera. Tunaambiwa hivi katika *Inkishafi*:

13. Hunu ulimwengu bahari tesi,

Una matumbawe na mangi maasi,

Aurakibuo juwa ni mwasi,

Kwa kulla khasara ukhasiriye.

Ubovu wa dunia husisitizwa na msanii huyu kwa kuwa maisha ya mwanadamu ni humu duniani. Dunia haina maana yoyote kama hakuna binadamu waishimo. Duniani ni watu kama asemavyo Abdalla (1983). Dunia inasawiriwa kama kitu kilichovurugika ‘*bahari tesi*’ na aifuataye mambo yake hukumbwa na hasara nyingi zaidi. Mwanadamu akiasi njia ya haki na nyofu ya kumtii Mungu na mitume wake basi kifo ndicho kitu kinachomngoja. Mtunzi huyu anaonyesha kuelewa mazingira ya baharini kikamilifu ndiposa akamithilisha maisha na mchafuko wa bahari. Katika bahari kuna wakati ambao upemo umetulia na hali ni shwari na huvutia sana. Lakini wakati mwingine kuna vurugu na shida nyingi kwa kuwa kimbunga hupuliza kwa nguvu na kuharibu ule utulivu ambao mwanadamu anapenda apate kuishi ndani yake. Mithili ya maisha ya kawaida ni kuwa wakati wa utulivu mwanadamu hujistarehesha na kujipumbaza kwa anasa za dunia huku

akijihisi raha mstarehe. Hali hii humfanya ajisahau kwa mambo ya dunia. Wakati wa mashaka hali huwa si shwari tena na hivyo inakuwa sawa na bahari tesi ambayo imevurugika kwa kimbunga kikali na kuharibu starehe za wasafiri na wanyama baharini humo. Kisha mtunzi huyu anaendelea kushadidia ubovu wa dunia akisema:

19. Dunia ni jifa siikarabu,

Haipendi mtu ila kilabu,

I hali gani ewe labibu,

Kuwania na mbwa hutukizwaye.

Dunia haipendelei mtu yejote yule na kiumbe kuparamia kwa nguvu ni kujitafutia aibu kwani mwanadamu hubaki kama mbwa (kilabu) anayetapika nyongo akarudi kuiramba. Mwanadamu kwa hivyo anajikuta kuwa hawezi kufurahia ya dunia kikamilifu ili asije akakosa mema ya kesho ahera. Kuishi duniani kunamtamausha kwani kuna mengi ya kufurahisha ela anaarifiwa kuwa yatamtia kwenye maangamizi ya milele endapo atashabihiana nayo na kukosa kujirudi mapema ili amfuate Muumba wa yote. Mwanadamu anatahadharishwa asiwe mbwa asiye na fikira, anayetapika nyongo akarudi kuiramba. Mwanadamu asiwe na tabia ya kung'ang'ania vitu vya dunia ambavyo viro katika mapito. Maisha ya dunia hayadumu bali yapo kwa muda mfupi usio bayana. Mtunzi wa *Inkishafi* anazidi kumtahadharisha mwanadamu dhidi ya ubovu wa dunia na namna inavyokatisha tamaa kwa kukumbusha moyo wake juu ya walioshiriki dunia lakini hatima yao ikawa ni mauti:

21. Wangapi dunia waipitewo,

Wakataladhudhi kwa shani lawo,

Ikawasumbika zitala zawo,

Wakanguka zanda wazumiye.

22. **Tandi la mauti likawakuta,**
Wakauma zanda wa kuiyuta,
Na dunia yao ikawasuta,
Ichamba safari munipukiye.

Katika ubeti wa 22 hapo juu, mtunzi anasawiri ubovu wa dunia kwa kutuonyesha hatima ya maisha ya mwanadamu kuwa ni mauti, ‘**Tandi la mauti likawakuta**’ na maisha ni safari ambayo haihitaji cheleo, ‘*Ichamba safari munipukiye.*’ Ubovu wa dunia amba ni makao ya wanadamu kuishi kwa raha huwakatishia tamaa ya kuishi. Mwanadamu maisha yake yamo duniani na kule ahera ni matumaini tu anayojipa kuwa maisha yatakuwa mema kwa kutegemea vile atakavyoishi duniani.

4.3.3 Uchungu wa mauti

Maisha ni matamu lakini mafupi. Mwanadamu katu hapendi kufa na hufanya kila juhudhi ili apate kukwepa kufa. Endapo ni ugonjwa ataenda hospitalini ili apate matibabu au pengine ataenda kwa mganga amgange na kumpa hirizi ili kujikinga na mabaya yoyote maishani. Kutokana na kuchukia kifo, maisha hupendwa kwa dhati na kila mtu. Kifo nacho hujidhihiri kama kitu kinachotia uchungu na hofu kwa mwanadamu. Ni taswira ya ukiwa na majonzi ambayo humkumba mwanadamu pindi anaposhuhudia mauti. Hapa tunamsikia mtoto katika ‘Usiniuwe’ kutoka kwa *Sauti ya Dhiki* akisema kwa uchungu:

27. *Uhai! Nakuliliya, wewe ndiye upendwaye,*
Uhai! Huna ubaya, yupi akutukiyaye?
A! Uhai niombeya, mamaangu sema naye,

Pengine atasikiya, asiniuwe mamangu.

28. *Nawe Haki nisemeya, kwa ya dhati matamshi,*
Sema na kuniombeya, nihururumiwe niishi,
Mamangu anioneya, anioneya bilashi,
A! Haki nihukumiya, asiniuwe mamangu.

Hakuna anayechukia kuishi kama asemavyo mtoto katika beti hizo ‘Uhai! Nakuliliya, wewe ndiye upendwaye, Uhai! Huna ubaya, yupi akutukukiyaye?’ Mtoto huyu kwa kuuliza swali la balagha hapa ni kule kusisitiza kuwa kuishi kunapendeza kila mja na hakuna yejote yule ambaye ana hiari ya kunyimwa nafasi ya kuishi hata kidogo. Mtoto huyu anazidi kuomba ‘Haki’ kusema na mamaye ili apewe nafasi ya kuishi kwani kuishi ni haki ya kila mtu na anaamini kuwa haki ikitendeka naye pia atapata nafasi ya kuishi. Hata katiba ya Kenya na mataifa mengine ya dunia husisitiza kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na hakuna mtu yejote anayeruhusiwa kumtoa uhai mwenzake. Kifo kinaleta machungu na majonzi kwa wafiwa. Mtunzi wa shairi kutokana na uchungu wa kufungwa jela na kunyimwa uhuru wake analilia uhuru wa kuishi nje ya jela. Yaonekana kuwa mle jelani mlikuwa na vitisho vya kuuawa na huku wale waliotaka kumuua mfungwa wakiwa wana tamaa ya kuzidi kuishi kwa amani kwa kumwondoa huyu mfungwa ambaye kwao ni kikwazo katika maisha yao.

Mtunzi anatumia mbinu ya tashhisu au uhaishaji hapa ili kutuelekeza katika mpaka wa uchukivu wa kifo na mapenzi ya maisha aliyo nayo mwanadamu. Ndiyo maana hata mtoto huyu ambaye yungali tumboni mwa mamake anawenza kuzungumza na ‘Uhai’ na ‘Haki’ ili apewe nafasi aishi,

hataki wala hapendi kufa. Mtu mwingine aweza kuona kuwa mtunzi ametia chumvi lakini ndio uhalisi wa maisha. Kukubali kufa si laiki ya kiumbe yelete. Hata akiwa mgonjwa mahututi akiona moto ukiwaka na kuja mahali aliko, atajikaza na kutoroka mbio ili aokoe maisha yake.

Katika *Utenzi wa Mwana Kupona*, Mwana Kupona anamkumbusha bintiye yale majonzi ambayo yalimkupata pindi mumewe alipoaga. Kifo cha mumewe kilimpa uchungu mwingi na kamwe hajapata kutulia kutokana na uchungu huo wa ukiwa. Anakumbuka mapenzi mema waliyokuwa nayo wakati alipoolewa na mumewe hadi alipokufa:

52. Naliowa na babako,

Kwa furaha na ziteko,

Tusondoleane mbeko,

Siku zote twaloka 'a

53. Siku moyo tusitete,

Ovu langu asipate,

Na lake lisinikute,

Hata akakhitarwa.

Lakini wakati alipokufa huzuni ilimshika na kamwe hajasahau mapenzi hayo. Kifo hiki kinamtia huzuni na upweke na ameshindwa kukoma kulia. Anatuonyesha uchungu wake katika beti zifuatazo:

54. Yalipokuya faradhi,

Kanikariria radhi,

Kashukuru kafawidhi,

Moyo wangu katushiya

55. *Tangu hapo hata yeyo,*
Siyanyamaa kiliyo,
Nikumbukapo pumbayo,
Na wingi wa mazoeya.

Naye mtunzi wa Inkishafi anasawiri mauti kwa waovu kuwa ni mateso na dhiki tele. Katika ubeti ufuatao anasema:

67. *Siku ya maini ndani kuwaka,*
Na paa za watu kupapatuka,
Ukimbiliepi pa kukushika,
Mbonya malijaa nitagamiye.

Maini kuwaka ni ishara ya adhabu kali ambayo ina machungu makuu. Waovu wataungulika ndani kwa ndani wala hakuna mahali pa kukimbilia, ‘*Ukimbiliepi pa kukushika.*’

4.3.4 Kifo ni hatima ya kila kiumbe

Ajabu ya kifo ni kuwa kinamkumba kila kiumbe; mwanadamu na wanyama pamoja na matendo yao. Ajabu zaidi ni kuwa mwanadamu hahisi uchungu wowote kuhusu kifo cha wanyama au mifugo ambao hufa au labda yeye mwenyewe huwaua kwa ajili ya mlo. Lau angekuwa na huruma au machungu nao, hangeshiriki kuwaua kwa vyovyote vile. Hata mazishi hawafanyii! Pengine ni jamii ya Wahindi ambao wana imani kuwa kila kiumbe mwenye damu ana uchungu

na hivyo asiuliwe kwa ajili ya mlo ndio pekee wana huruma na viumbe hawa. Labda viumbe hawa wana uchungu! Twasema labda kwa sababu kuna viumbe wengine wasiotokwa na damu kama vile kumbikumbi ambao wanaliwa na hawatoi sauti wanapouawa. Ajabu kubwa zaidi ni kuwa mwanadamu anajipenda kupindukia. Kifo cha mwenzake wakati mwingine humfariji au anachangia katika mauaji yake. Ndiyo maana wanaunda silaha hatari ya kujilinda dhidi ya maadui (wanadamu wengine). Lakini kifo hatimaye huwakumba wote. Kama Heidegger (1962) anavyotwambia kuwa kifo kipo na kila kiumbe ana kifo chake tofauti na mwingine. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* mtunzi wake naye anasema kuwa sote tutakufa wala hakuna atakayesalia:

6. Mwana Adamu si kitu,

Na ulimwengu si wetu,

Walau hakuna mtu,

Ambao atasaliya.

Katika vitabu vitakatifu tunaambiwa kuwa kila mtu ataaga dunia. Katika Biblia na Qur'an tunaambiwa kuwa baada ya Adamu na Hawa kumwasi Mungu, walipewa hukumu kuwa wote watataabika duniani ili kujikimu na hatimaye watakufa. Hata Yesu na Muhammad (s.a.w) ambao wanafuatwa na waumini wa Kikristo na Kiislamu mtawalia, waliaga dunia. Kifo kinapokuja hakimbagui yejote hata akiwa mkwasi au maskini, kiongozi au mfuasi. Hivi ndivyo mtunzi wa *Inkishafi* anavyotusawiria akirejelea watawala wa Pate pamoja na watumwa wao ambao wote waliangamia:

32. Hakuwa mtume Sulaimani,

Maliki wa insi na ajinani,

*Walimfuteye ukamukhini,
Akiwa mwingine humtendaye.*

*33. Watoto wangapi uwawenewo,
Ukawayakini kupona kwavo,
Sasa nyumba kati ziwatetewo,
Katika luhudi iwafundiye.*

*34. Uwene wangapi watu wakwasi,
Walo wakiwa kama shamasi,
Wa muluku zana za adharusi,
Dhahabu na fedha wakhiziniye.*

*35. Malimwengu yote yatwatiile,
Na dunia yao iwaokele,
Wachenda zitwa zao zilele,
Mato mafumbuzi wayafumbiye.*

Mtunzi huyu anatuonyesha namna kifo kinavyomkumba kila kiumbe. Mtume Suleimani na watu wengine wakwasi waliokuwa waking'aa kama juu 'Walo wakiwa kama shamasi' kwa kumiliki dhahabu na kuheshimiwa na watu wote walikufa. Mtunzi huyu anazidi kushadidia akisema:

*45. Sasa walaliye mji shubiri,
Pasipo zuliya wala jodori,*

*Ikawa miwili kutaathari,
Dhiki ya kaburi iwakusiye.*

Kiumbe afapo huacha kila kitu duniani na hurudi bure kaburini jinsi alivyokuja duniani. Kama asemavyo mtunzi huyu katika ubeti huo, ‘*Sasa walaliye mji shubiri, Pasipo zuliya wala jodori*’. Ikabaki dhiki ya kaburi kuathiri mwili wa marehemu hao. Huu ni uhalisia wa maisha ya mwanadamu. Yamkini watunzi wa mashairi haya walipata kushuhudia kifo cha wenzao na pia mafunzo ya dini yao yaliwahimiza kubaini hatima ya mja kuwa ni kifo. Mtunzi wa *Inkishafi* kutokana na tajriba yake ya kushuhudia kuangamia kwa Dola ya Pate, anatumia historia ya mji huu kutuwasilishia kifo kama kiungo cha maisha ya mwanadamu. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* msisitizo ni huohuo na umejengwa kwenye msingi wa dini.

4.3.5 Upweke wa kifo

Kwa mujibu wa Sivananda (1997), kifo kina uchungu kwa mpenda anasa za dunia. Hii ni kwa sababu akikumbana na kifo huona uchungu wa kutengana na mazuri yaliyokuwa yakimfurahisha na kuenda katika upweke wa ukimya na unyamavu usiokuwa na sauti wala kelele zozote za ngoma, wanyama, watu, wadudu wala maumbile. Mtunzi wa *Inkishafi* anatusawiria mji wa Pate jinsi ulivyonawiri na kisha ukapata kuanguka. Mji huu ambao ulisheheni shughuli nyingi sasa umberaki pweke baada ya wakaazi wake kufariki. Watumwa wake wa kike na wa kiume waliokuwa wakiwfanyia mabwana zao kazi usiku na mchana sasa hawapo tena. Watawala waliokuwa na vijakazi wa kuwashudumia walitoweka pia. Makasri ya kifalme yakageuka mahame ya kukaliwa na ndege. Popo wananging’inia juu ya dari. Ni taswira ya hali mbovu na

upweke ulioshamiri na kuchukua usukani wa pilikapilika zilizokuwepo awali. Ubeti huu wa *Inkishafi* unashadidia hali hii:

49. Nyumba zao mbake ziwele tame,

Makinda ya popo iyu wengeme,

Husikii hisi wala ukeme,

Zitanda matandu walitandiye.

Nyumba inayozungumziwa katika ubeti huu ilikuwa nzuri na yenye nuru ‘mbake’ lakini sasa ni magofu ‘ziwele tame’. Hapa nyumba yenye nuru ni kama mwanadamu aliye hai na mwenye siha yake ambaye baada ya kipindi kidogo ule mwili uliokuwa na siha nzuri umegeuka maiti ghafla baada ya mauti kumkumba kiumbe. Pindi nyumba hii ilipohamwa kukawa na kimya ila ndege kama popo ndiye anayepatikana humo. Ni ishara ya upweke maana popo huwa hawapendi palipo na kelele wala mwangaza bali penye ukimya na kiza. Kisha mwandishi anazidi kushadidia upweke wa kifo katika ubeti unaofuatia akisema:

50. Madaka ya nyumba ya zisahani,

Sasa walaliye wana wa nyuni,

Bumu hukoroma kati nyumbani,

Zisiji na kotwe waikaliye.

Bundi ‘bumu’ anapewa nafasi ya kuonyesha upweke na shari ya mauti. Bundi ni ndege ambaye huhuishwa na kisirani na matukio mabovu. Katika imani ya jamii nyingi za Kiafrika, ndege aitwaye bundi hunasibishwa na ukiwa na mauti. Mbaabu (1991) na Mlamali (1980) wanakubaliana kuwa bundi ni ndege anayechukuliwa kusimamia hali ya masikitiko na msiba. Mbaabu kwa mfano anadai kuwa mionganini mwa jamii ya Waswahili kuna itikadi kuwa bundi

akilia kwenye paa basi mtu atakufa katika nyumba hiyo. Ahmed (1988) akiashiria hatima mbaya wa mhusika Mvita anatupa ishara ya bundi ambaye anaonekana karibu na nyumbani kwao kabla ya kifo kumkumba. Mtunzi wa Inkishafi anatuonyesha kuwa tajriba yake na historia ya jamii yake imemwathiri katika kuelewa na kufasiri kifo. Uhalisia wa mazingira yake umeitikadi katika kumnasibisha bundi na mauti na ndivyo hivyo anavyotusawiria.

Mwandishi Walibora (1996) anatupatia picha sawia ya mazingira ya upweke wa kifo tunapokumbana na mhusika wake Kongowea Mswahili. Mhusika huyu anapoenda kuonana na Mzee Kazikwisha kama alivyomwagiza wakutane, anakuta mji uliojiinamia jii kuashiria kifo. Mazingira ya mji huu yamesawiriwa kama ifuatavyo:

Nikaingia chumbani mwa Mzee Kazikwisha...nilipoingia chumbani nikakumbana na harufu kali. Kundi la mijipanya likatoka kitandani na kuparamia ukuta na kutokomea. Nzi walilialia. Moyo wangu karibu upasuke kwa yale niliyoyaona. Mzee yule alikuwa maiti. Babangu alikuwa tayari marehemu. Nzi walikuwa waking'ong'a uhondo katika maiti ile iliyokuwa tayari imeanza kuoza. Alikuwa amenyooka kitandani kama ambaye alikuwa akilala. Pengine kufa kwake ilikuwa heri hiyo. Wakati maisha yalipoamua kumwia magumu, kifo kilikuwa aula zaidi.

Mzee Kazikwisha hakuwa na wa kumhudumia ila mijipanya na nzi ambao ndio walikuja kusherehekea maiti yake. Maisha hayakumpa afueni yoyote maana alikosa mtu wa kumsaidia hadi kifo chake.

Mtunzi wa *Inkishafi* mbali na bundi na nyuni wanaolalia kwenye mahame anafikia kilele cha ukiwa na upweke wa mauti pale anapotoka ndani ya nyumba na kutumulikia mazingira ya nje ya nyumba iliyobaki mahame akisema:

53. Ziwanda za nyumba ziwele mwitu,

Ungi wa matuka na kutukutu,

Milango ya ndia yatisha mtu,

Kwa kete na kiza kilifundiye.

Nje ya nyumba hii kuna mwitu ambao umemea na kujenga magugu, ‘*Ziwanda za nyumba ziwele mwitu, Ungi wa matuka na kutukutu*,’ hali ambayo inampa mtu kitisho na wasiwasi mwingi, ‘*Milango ya ndia yatisha mtu, Kwa kete na kiza kilifundiye*.’

Mwana Kupona naye anapomuuusia bintiye anakumbuka upweke uliomkumba baada ya mumewe kufariki. Kifo hiki japo kilimtia majonzi, alibaki na upweke wingi. Hali hii ndiyo inayomfanya kulia akikumbuka mazowea na mahusiano mazuri aliyokuwa nayo na mumewe:

54. Yalipokuya faradhi,

Kanikariria radhi,

Kashukuru kafawidhi,

Moyo wangu katushiya.

55. Tangu hapo hata yeyo,

Siyanyamaa kiliyo,

Nikumbukapo pumbayo,

Na wingi wa mazoeaya.

4.3.6 Kifo si mwisho wa maisha

Wataalamu wengi wanaonyesha kuwa kifo si mwisho wa maisha. Mawazo yao yanaoana pakubwa na imani za takriban dini zote ulimwenguni, za Kiafrika zikiwemo. Huwa tunaambiya kuwa tukiishi vema duniani na ahera pia tutaishi hivyo. Wataalam kama Mbiti (1969) na Sivananda (1997) wanakubaliana kuwa kifo si mwisho wa maisha. Kifo ni mwanzo wa maisha katika awamu nyingine mbali na upeo wa macho ya mwanadamu. Upo huu wa maisha baada ya kufa ndio wakati mwingine huitwa transfizikia. Inaonyesha kuwa hata baada ya kufa kimwili kuna uhai mwingine kule ahera. Katika jamii mbalimbali za Kiafrika, kifo si mwisho wa uhai maana wale wahenga bado wanahudumiwa kwa kutambikiwa au majina yao, watoto wanaozaliwa hupewa ili kuwakumbuka na kuendeleza kule kuishi kwao katika akili za wanajamii. Alembi (2001) akitafitia jamii ya Abanyore anathibitisha kauli hii akisema kuwa watoto wanaozaliwa wakati au baada ya watu fulani kufa hupewa majina ya hao waliokufa na mazishi hufanywa kwa heshima kubwa ili mfu asipate kuwatatiza walio hai endapo watakosa kumhudumia vema. Mtunzi wa *Inkishafi* na *Utenzi wa Mwana Kupona* wanathibitisha hali ya maisha kuwepo baada ya kufa wakisema kuwa bora tuishi kwa kutenda mema ili kesho ahera tupate thawabu. Katika *Inkishafi* mtunzi wake anasema:

70. Na malipwa yao wadhilimuwa,

Si dhahabu timbe si ya kufuwa,

Fedha hawatwai na wangapowa,

Ila hasanti ni malipwaye.

71. Aso hasanati wala thawabu,

Hufungwa kitaya kama rikabu,

Akatwekwa dhambi za maghusubu,

Akambiwa haya mtukuliye.

Walokuwa wakiwadhulumu watu duniani waliweza kutumia fedha au madini ya thamani ya juu kama dhahabu ili kufidia hao kama wameshtakiwa. Lakini hali hii imegeuka mbinguni kwani waliodhulumiwa hulipwa mema pekee kama asemavyo mshairi huyu katika maneno ya beti hizi, ‘*Ila hasanti ni malipwaye*’ ilhali waovu wanapata taabu na masumbuko kwa uovu wao: ‘*Aso hasanati wala thawabu, Hufungwa kitaya kama rikabu, Akatwekwa dhambi za maghusubu, Akambiwa haya mtukuliye.*’ Kuna imani na msemo wa Waswahili kuwa malipo ni hapahapa duniani, ahera yenda hesabu. Siku ya kiyama inaaminika kuwa matendo ya mtu ndiyo yatahesabiwa ili apewe thawabu au adhabu zake. Imani hii ndiyo ilisawiriwa hapa kisanaa.

Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* tunaambiwa:

74. Nimekupa duniani,

Watunde uwahizini,

Unipe kesho peponi,

Mbee za Tumwa Nabiya’

75. Wangalie kwa huruma,

Uwongoze ndia njema,

Uwepulie na tama,

Za akhera na duniya.

Kisha anazidi kueleza:

95. Somani mite ya nganu,

Mtii waume wenu,

Musipatwe na zitunu,

Za akhera na duniya.

Katika beti hizi Mwana Kupona anaonyesha kuwa matendo mazuri ya mtu humwokoa dhidi ya maangamizi ya roho. Anahimiza matendo mazuri jinsi dini inavyosisitiza ili mja apate kuishi salama duniani na kesho ahera afufuliwe ili aishi maisha ya milele. Hapa ni bayana kuwa kifo si mwisho wa maisha bali ni mwanzo wa kuishi kwa namna nyingine kule ahera. Ndani ya mauti kuna maisha na ndani ya maisha kuna mauti.

Mtunzi wa ‘Usiniuwe’ katika *Sauti ya Dhiki* anaona kuwa maovu ya mtu ndiyo humsababishia maangamizi. Kwake haki ikitendeka basi kifo hakina nafasi ya kuja kumchukua kiumbe. Kupitia mtoto tumboni mwa mamake anasema:

28. Nawe Haki nisemeya, kwa ya dhati matamshi,

Sema na kuniombeya, nihururumiwe niishi,

Mamangu anioneya, anioneya bilashi,

A! Haki nihukumiya, asiniuwe mamangu.

Haki inahimizwa kumkanya mama asimuue kwa makosa ambayo hajatenda. Mamake anaonekana kuwa anamwonea tu wala hana hatia yoyote ya kustahili kufa. Yamkini mtoto anaona kifo kwenye mizani ya maovu, kwamba mwovu adhabu yake ni kifo na mwema thawabu yake ni kuishi, ‘A! Haki nihukumiya, asiniuwe mamangu.’

4.3.7 Ukatili wa mauti

Kufa si sahili. Wakati wa kufa huwa kuna mapambano makali baina ya maisha na kifo. Maisha yakidai kuzidi kutawala ilhali kifo kikikakawana kuchukua usukani. Kifo kama mwanamapinduzi huja kwa fujo na vishindo hadi pale maisha yanapolegea yakidhani vita vimeisha, kifo ghafla hutoka na roho ya kiumbe. Mlamali (1980:25) akifasiri *Inkishafi* anasema hivi:

Hivyo ndivyo aonavyo mwenye *Inkishafi* fungamano lilivyo baina ya mauti na maisha. Yaani mauti yamekaa kama mtu mshari anayewaacha wenyewe maisha walewelewe na raha za maisha, ndipo anapofyatua mshale wake na kufuma, na jinsi alivyo mkorofii wa shabaha, akifuma hakosi.

Mawazo yake haya ni ukweli wa maisha na tunaweza kuyathibitisha na ubeti ufuatao kutoka katika utenzi wa *Inkishafi*:

24. Mvi wa manaya ukawafuma,

Akatumbukia katika nyama,

Nasiwe mwatami mwenye kwatama,

Amwamba ni ani yalikuwaye.

Sajili ya usasini imetumika kudhihirisha kuwa kifo ni kama mwindaji ambaye yu mbioni kuchukua kile ambacho kina nia nacho. Pia huwinda kwa ukatili mkubwa wa kufuma kwa mishale yenye ncha kali na kikilenga hakikosi shabaha. Sajili hii pia ni ya vitani ambayo ianonyesha kuwa kuna mapambano makali baina ya uhai na mauti.

Mbele ya kifo kiumbe hana budi kusalimu amri ili apate kuchukuliwa na kifo. Hii ni kwa sababu kifo kina ujibari na nguvu tele na wakati wake ukifika kiumbe hawezi kuahirisha ama kujiongeza muda wa kuishi. Hakuna mkataba wa maelewano wala maagano yoyote kati ya kiumbe na mauti. Mauti huja kama mwizi na kumpoka kiumbe uhai wake bila indhari. Mtunzi wa *Inkishafi* anazidi kueleza hali hii katika ubeti ufuatao:

25. Wakazisalimu umri zawo,

Hadimu ladhati achenda nawo,

Pasi mkohozi akohowawo,

Au mwenye kwenda asiridhiye

Mtunzi wa ‘Usiniuwe’ katika *Sauti ya Dhiki* kutokana na dhiki ya kifungo katika jela na mateso mengi aliyoyapata anahofia maisha yake ambayo anaweza kupokonywa wakati wowote. Enzi yake alipokuwa kifungoni kuna wafungwa wengi ambao waliuawa au waliotoweke bila kujulikana walikoenda. Ukatili huu wa kuuawa na utawala ambao ulifaa kumpa ulinzi na kumhakikishia usalama wake unampa hofu nyingi kifungoni. Kwa kutumia mhusika mtoto ambaye yungali tumboni mwa mamake anayehisi kuwa atauawa analia hivi:

11. Bado sijamalizika, halijesha umbo langu,

Sitakwisha kwa haraka, zitapita siku tungu,

Huna haki kunipoka, uhai ni haki yangu,

Niwata ‘takamilika, mamangu nihurumiya.

Mtunzi huyu anatumia kauli ‘*Huna haki kunipoka, uhai ni haki yangu*’ katika ubeti huu ili kuthibitisha ukatili wa kutoa uhai. ‘Kupoka’ ni kunyakua kitu kwa ghafla bila kuarifu, ni

kunyang'anya kwa nguvu, kung'oka na kitu. Kifo kinasawiriwa kama kitu katili ambacho kinanyakua uhai wa mtu na kumwacha kiumbe bila uhai tena.

4.4 Mazingira katika usawiri wa kifo

Mtunzi wa kazi ya sanaa huumba kazi yake katika mandhari mahususi. Hata kazi ambazo hutazamwa kama za mazingaombwe au za kufikirika hujengwa katika mandhari maalum akilini mwa msanii. Hii ndiyo maana kazi yoyote ile ya fasihi huweza kufasirika katika mazingira fulani duniani. Mazingira ni jukwaa la matendo ya sanaa anayosuka mtunzi ili kuweza kuumba wahusika wake na matendo yao. Huweza kuwa dhahiri au dhahania. Ili kazi ya sanaa ifuzu ni lazima mtunzi ang'amue mazingira yake vilivyo na kuelewa kila kiungo cha mazingira yake kisha kutumia viungo hivyo kufanikisha ujenzi wa maudhui na fani ya kazi yake. Mazingira ya mtunzi hujumuisha vipengee vya wakati, dini au utamaduni na lugha.

Cuddon (1979) anafafanua mazingira kuwa ni wapi na lini katika hadithi au tamthiliya. Mandhari ni mahali katika mazingira ya wakati fulani. Mahali na wakati husaidia kubainisha muktadha. Na muktadha husaidia kubainisha utamaduni wa jamii husika, ikiwa kwa dhana ya utamaduni tutakuwa na maana kwamba ni mwakiso wa maisha ya jamii fulani katika ujumla wake.

Maelezo haya yanatubainishia kuwa mazingira hujumuisha vipengee vya wakati, utamaduni, na lugha. Utamaduni huwa ni jumla ya mambo yote yanayosawiri jamii fulani kwa njia ya kipekee na inayoibua ubainishaji ulio wazi toka jamii moja hadi nyingine. Mazingira katika tamthilia au riwaya hubainika vema katika jukwaa la matendo au maonyesho ilhali katika ushairi hubainishwa na maneno anayoteua msanii ili kuwasilisha matendo ya wahusika wake. Uteuzi wa

mazingira au mandhari ya kufana husaidia pia katika uwasilishaji wa ujumbe wa mshairi kwa hadhira yake. Kwa kurejelea mashairi teule tuliyoyashughulikia katika utafiti wetu, mazingira yanemetumika kuibua utamaduni wa watanzi na itikadi au imani yao juu ya kifo. Vipengee vya tajriba ya mwandishi na utamaduni wa jamii vimetusaidia kubaini namna mazingira ya mtunzi yanavyojidhiri katika uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

4.4.1 Wakati

Kazi ya sanaa ni chimbuko la historia, ni tukio la wakati maalum. Mtunzi mara nyingi hujenga sanaa yake kutokana na kile ambacho kimewahi kumkumba au kilichompata mwingine akapata kusikia au kushuhudia. Hali hii ndiyo tunakumbana nayo katika *Inkishafi* ambapo mtunzi wake alipata kuishi na kushuhudia kukua na kuangamia kwa Dola ya Pate. Kutokana na kushuhudia kwake vile watawala wa Pate walivyokuwa wakiwatumia watumwa na wengine na kisha kuja kuangamia kwao, mtunzi huyu akatumia mazingira hayo ya Pate ya karne ya 19 na kutusimulia kuanguka kwake katika taswira ya kifo. Mtunzi anaanza kutujengea mazingira ya dunia pana na mapito yake akisema:

21. Wangapi dunia waipitewo,

Wakataladhudhi kwa shani lawo,

Ikawasumbika zitala zawo,

Wakanguka zanda waziumiye.

Kisha anaendelea kujibainisha na mazingira yake yaliyomchochea kuandika utenzi huu akisema:

59. Wapi wa Kiungu wayaza kumbi,

Na mashekhe mema wake Ki-Sarambi,

*Walaliye nyumba za vumbivumbi,
Ziunda za miti ziwaaliye.*

*60. Wa wapi ziuli wa Pate Yunga,
Wenye nyuso ali zenyе mianga,
Wangiziye nyumba za tangatanga,
Daula na ezi iwaushiye.*

*61. Kwali na mabwana na mawaziri,
Wenda na makundi ya asikari,
Watamiwe nati za makaburi,
Pingu za mauti ziwafundiye.*

Mazingira ya Pate katika enzi zake za kunawiri imetumika hapa huku mtunzi akirejelea watawala wake na makaazi yao. Mtunzi anatutajia mitaa ya Kiungu na Sarambi ambayo ilikuwa ya watu wakwasi na wanaojipata kiuchumi. Hili ni jambo halisia kwa kuwa watu wakwasi mara nyingi huishi katika mitaa tofauti na wachochole au wasiojiweza. Lakini leo hao wakuu wa Pate wamekwishaaga, ‘*Walaliye nyumba za vumbivumbi*’, na tayari wamezikwa, ‘*Ziunda za miti ziwaaliye*.’ Hawa walikuwa masultani wenye hadhi ya juu kwani nyumba walizoishi zilikuwa makasri yaliyojaa anasa tupu. Mtunzi anasema hayo katika kauli yake ‘*wakataladhudhi kwa shani lawo*’, yaani wakashiriki anasa na wakaona raha nyingi. Lakini mauti yalipofika ngome yao haikuwa imara ili kuwakinga dhidi ya maangamizi makuu yaliyowafuma ghafla bila tahadhari yoyote. Mtunzi anashangaa kwa kutoweka kwao, ‘*Wa wapi ziuli wa Pate Yunga*,

Wenye nyuso ali zenyе mianga'. Kumbe hao watu maarufu wa Pate walishaaga dunia. Walikufa wote, mabwana na mawaziri pamoja na askari waliokuwa wakiwalinda. Sasa wamo makaburini ambamo hawawezi kujikomboa kwani wamezikwa na mauti yamewakaba vivilvyo, '*Watamiwe nati za makaburi, Pingu za mauti ziwafundiye*'. Kifo kilipofika kiliwakaba bila saburi na hakuna mwenye nafasi ya kujikomboa dhidi ya mauti.

Tunamwona mtunzi wa *Inkishafi* akiuliza kuwepo kwa watu ambao walikuwa maarufu kule Pate. Yaonekana hawapo tena, wamekwishaangamia. Ndiposa anashangaa akiuliza wa '*wapi ziuli wa Pate Yunga*'. Beti hizi za *Inkishafi* ambazo zinauliza kuwepo au kutokuwepo kwa watu mashuhuri kwa kutumia kifungu *wapi* au *wa wapi* katika ubeti wa 59 na 60 zinasomeka sawa na beti za *Utenzi wa Pambazuko la Afrika* ambapo tunampata mtunzi wake akitumia vifungu *yuwapi* na *yuko wapi* akiashiria kifo cha ukoloni barani Afrika. Wakoloni wa Ulaya na Arabia walikuwa maarufu sana kiuchumi, kisiasa na kijamii wakati wa utawala wao barani Afrika. Kigezo cha ustaarabu kilikuwa chao na chochote kilichokuwa asilia ya Mwfrika kilidunishwa kwa kila hali. Lakini hatimaye tawala hizi ziliporomoka na kutoweka baada ya Afrika kujikomboa kutoka kwenye minyororo na pingu zao. Mtunzi wa utenzi huu anasherehekeea kuangamia na kutokomea kwa wakoloni ambao walishitadi na kushika kani kukandamiza nchi za Kiafrika. Anataja dola hizo ambazo zilitawala Afrika kwa ukiritimba lakini hii leo zimeshindwa. Kushindwa kwa dola hizi za Ulaya na Arabia kunatokea sawa sawa na kuangamia kwa mji wa Pate na utawala wake. Huu ni uhalisia wa kiwakati na kimazingira unaosawiriwa kifasihi. Tajriba ya mwandishi huyu nayo inajitokeza pale aliposhuhudia ukoloni kujikita na kisha kuangamia. Hali hii ni sawa na mtunzi wa *Inkishafi* ambaye alishuhudia au alipata kusimuliwa kuanguka kwa Dola ya Pate. Mtunzi wa *Utenzi wa Pambazuko la Afrika* anatumia tashdidi

kuthibitisha kuangamia au kufa kwa ukoloni barani Afrika akitaja kila nchi iliyotawala Afrika kwa kiburi na jinsi leo hii imeshindwa. Beti zake zifuatazo zinadokeza hali hiyo:

Yuko wapi Mngereza?

Afrika loiweza,

Hayupo ameteleza,

Ulaya amerejeya.

Yuwapi Mtaliana?

Lokuwa akijiona,

Na akijitapa sana,

Afrika kaiachiya.

Yuwapi Mjarumani?

Kwa ukali namba wani,

Na viboko mikononi,

Watu kimsujudiya.

Yuwapi Mfaransa?

Maarufu wa kutesa,

Ameshapigwa msasa,

Mate anatumezeya.

Yuwapi naye Mdachi?

*Kwa ukali kama kuchi,
Ameshapigwa muchi,
Naye ametokomeya.*

*Yuwapi nayo Mmanga?
Ni bingwa kwa zake panga,
Ameshindwa kutuvunga,
Karejeya Arabiya.*

*Yuwapi Mbelgiji?
Kwa ulafi ndiye gwiji,
Kaihama yetu miji,
Karudi liko tokeya.*

*Yuwapi jimbi Mrenu?
Kuupata tu upenu
Kutoka na usununu
Mtutu kaukimbiya.*

*Yuwapi Msipania?
Alokwa kapania
Nchi kujifaidia
Hataki kuturejeya.*

Takriri ya kuulizia wapi walipo hawa watawala ni ishara ya kuonyesha kuwa wameshatoweka ulingoni mwa utawala. Utawala wao uliokuwa maarufu kama utawala wa Pate umeporomoka na kuangamia, kilichobaki ni kumbukumbu. Hii ni taswira ya kuimarike au kukua na kufa kwa binadamu. Kuna wakati mtu huwa na afya na siha nzuri ya kuenzika na kutamanika lakini ni kipindi ambacho hakidumu milele. Baada ya mtu mfupi mtu huangamia.

Mtunzi wa ‘Usiniuwe’ katika *Sauti ya Dhiki* naye anatumia mazingira ya ‘tumboni mwa mamake’ akizungumzia kifo. Haya ni mandhari dhahania kwa misingi ya ufasiri wa juujuu lakini tukimrejelea mtunzi na maisha yake tunabaini kuwa alikuwa akitumia mazingira halisi, ‘tumbo’ kumaanisha jela alimokuwa amefungwa. Hivyo basi kilio hiki ambacho tunakishuhudia cha mtoto kumlilia mamaye asipate kumuua ni kilio cha raia mwema ambaye anaomba utawala wa nchi yake usimhukumu kifo. Kilio hiki kinajibainisha wazi katika beti zifuatazo:

10. Na hilo pande la damu, likakaa kwa salama,

Likingoja yake zamu, aloiweka Karima,

Zamuye ilipotimu, nikawa nofu la nyama,

Basi usinihukumu, mamangu nihurumiya.

11. Bado sijamalizika, halijesha umbo langu,

Sitakwisha kwa haraka, zitapita siku tungu,

Huna haki kunipoka, uhai ni haki yangu,

Niwata ‘takamilika, mamangu nihurumiya.

12. Huna haki kuniuwa, japo sijakamilika,

Huna haki kunitowa, kabla siku kufika,

Niwata nipate kuwa, mimi mwenyewe ‘tatoka,

Mama wata kuniuwa, mamangu nihurumiya.

Neno ‘usinihukumu’ na mafungu ‘zitapita siku tungu’, na ‘kabla siku kufika’ hudhihirisha kifo kama tukio ambalo huja wakati fulani. Kila mja ana muda aliopewa kuishi kabla kufa kwake. Ufahamu huu ndio unamfanya huyu mtoto kumlilia mamake ampe fursa aishi kwanza wala asimtoe tumboni mapema asije akafa bila ya kuishi maisha aliyopangiwa duniani. Wakati mwingine endapo mtoto atakufa kabla au wakati wa kuzaliwa kwake utasikia baadhi ya watu wakidai kuwa, ‘hakuumbwa kuishi’.

Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* tunamwona mtunzi akitunga kazi hii wakati akiona kuwa maisha yake yanakaribia mwisho kutokana na ugonjwa uliomkabili. Mulokozi (1999) anadai kuwa Mwana Kupona aliutunga utungo huu akiwa mgonjwa wa tumbo la uzazi na alipobaini kuwa alikuwa na nafasi finyu ya kupona. Mwana Kupona anatuonyesha hali yake ya kuugua katika ubeti ufuatao:

2. Maradhi yamenishika,

Hata yametimu mwaka,

Sijapata kutamuka,

Neno lema kukwambiya

Katika ubeti huo anaonyesha kuwa ameishi na binti yake kwa muda mrefu lakini hakuwahi kumshauri njia ipi ya kuishi kwa wema na watu wengine ili akifa aende peponi. Maradhi

yalipokuwa yamemzidi akazinduka kuona kuwa maisha yake yanaelekeea ukingoni na muda ambao alikuwa amesalia nao ulikuwa mfupi. Kama mama mzazi aliyeishi na kushuhudia mengi akaona kuwa ni wakati wake mwafaka wa kumshauri bintiye. Kifo kinapomkabili kiumbe humzindua na kumwonyesha njia ya kufuata katika matekelezo ya majukumu yake. Kisha anamwonyesha bintiye kuwa kunafika wakati ambapo kila kiumbe ambaye yu hai ataangamia maana dunia ni mapito kwetu sisi wanadamu. Hivi ndivyo asemavyo katika ubeti ufuatao:

6. Mwana Adamu si kitu,

Na ulimwengu si wetu,

Walau hakuna mtu,

Ambao atasaliya.

4.4.2 Dini au utamaduni

Dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya Mungu na binadamu au ni njia ya kuhusiana na Mungu kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981)

Mulokozi (1999) anasema kuwa Waswahili ni Waafrika, hata kama wamechanganyika na watu wengine kutoka nje ya bara hili. Waafrika wanazo mila na desturi zao za jadi kuhusu mahusiano ya watu katika ndoa na maisha kwa jumla ambazzo huwafundisha watoto wao.

Sengo (1995) akiandikia itikadi za jamii ya Waswahili kule Msimbati anasema kuwa:

Wakazi wa eneo hili wanasadiki kuwa Uislamu uko, Ukristo uko lakini kuna mambo mengine ambayo kidogo ni ya kimila, kwa hakika kuyaepuka ni vigumu...tambiko hizi za Msimbati zinaelekeea kuwa ni sehemu ya uganga. Kama dhana, tambiko ni dhana

maarufu katika pwani yote ya Uswahilini. ...jadi ya pwani na visiwani, karibu zote, zinatumia hirizi moja ama nyagine. Hirizi kwa maana ya kinga ni pamoja na dua, Sura au Aya ya kinga, kipande cha karatasi au kombe la kula ama kunywa, dawa ya kula utotoni, au cha ngozi, kucha au nywele n.k. Ni itikadi iliyoshamiri kiasi kwamba haimkiniki kudhani kuwa yuko mtu ambaye hajikingi kwa dua, sura ama aya za Qur'an, dhidi ya nyoka, dawa za kivuvi, n.k. ...kote kuliko itikadi hii, inakubalika kuwa ni shir-k cubwa kwa yejote kuamini moja kwa moja kwamba hirizi kama hirizi au hata hao malaika au majini wanaohusishwa nazo wana uwezo na nguvu zozote. Tegemeo pekee ni Mungu tu.

Mugambi na Kirima (1976) nao wanasisitiza kwamba licha ya Waafrika kupata dini kama vile ukristo kutoka nje, bado wanadumisha mila na desturi zao. Wanasema kuwa Mwaafrika hubaki Mwaafrika hata akibatizwa na kuwa mkristo kwa kufuata mila ambazo zilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mila hizi na desturi za Kiafrika ndizo nguzo zao ambazo wanaingia nazo katika dini zao na bado huwaathiri kimawazo na kimatendo katika shughuli za kila siku. Imani za Kiafrika husawiri mtazamo wao kuhusu maisha na kifo.

Ni vigumu kutenganisha dini na utamaduni wa jamii. Katika mwambao wa Afrika Mashariki, kwa mfano, dini ya Kiislamu na utamaduni wa wenyeji vimeshikana kwa kiasi kikubwa. Wakati wa utawala wa Waarabu wa Omani, sultan wa Zanzibar alijumuisha maeneo yote ya mwambao wa Afrika Mashariki katika milki yake. Ni wakati huu ambapo dini ya Kiislamu ilipata kuenea zaidi ndani na nje ya pwani ya Afrika Mashariki. Misikiti mingi na vyuo vyta mafunzo ya dini ya Kiislamu vilijengwa. Wenyeji wa mwambao walislamu kwa wingi na kujumuisha dini na

utamaduni wao katika tangamano moja. Utawala wa kisultan ulikuja kupokelewa katika miji mingi ya pwani. Miji iliyojiimarisha kiuchumi na kisiasa hatimaye ikawa na masultan wao. Mojawapo ya miji hiyo ni mji wa Pate ambao ulikuwa maarufu kutokana na kukua kwake kisiasa na kiuchumi. Mji huu ulifuata utawala wa kisultani ambao uliwaruhusu matajiri kuwa na watumwa. Matajiri hao walitawala kwa udhalimu mkuu na wakashiriki anasa za dunia kiasi kwamba walikuja wakasahau kuwa mtu ni utu. Udhalimu huu ulikuja kufika kikomo siku ya kufa kwao. Mtunzi wa *Inkishafi* alishuhudia kuanguka kwa utawala huu na udhalimu wake kwa umma ndiposa akatunga utenzi huu kuuasa moyo wake ili ujurudi kwa kuacha madhalimu na kumhimidi Mungu. Mtunzi anaushawishi moyo wake kwenda sijida akisema:

*30. Ewe moyo enda **sijida** yake,*

Hela tafadhali unabihike,

Shetani rajimi asikuteke,

Kesho kakuona kuwa kamaye.

Sujudu ama sijida ni mtindo wa kuomba katika dini ya Kiislamu ambapo mtu anapiga goti na kuinamisha uso wake mchangani. Hii ni ishara ya kunyenyeka kwa mwanadamu mbele ya Mungu wake. Mtunzi anauasa moyo wake ili usipatwe na maangamizi kwa kupotoshwa na shetani, ‘*Hela tafadhali unabihike, Shetani rajimi asikuteke.*’

Mlamali (1980) akirejelea mawazo ya Al-Ghazali kuhusu dhana ya sijida au sujudu anasema:

Sujudu ndiyo daraja kubwa kabisa ya kunyenyeka, kwani kati ya mengine inarejesha kiungo azizi kabisa-uso-kwenye asili yake...inarejesha ‘tanzu shinani’...na maana ya kurudisha ‘tanzu shinani’ ni hii: asili ya mwanadamu ni udongo, na pale anapoweka

kipaji cha uso wake chini ni kitendo cha nje kinachodhihiri dhati ya ndani. Ni thibitisho kwa mja la Umola wa Mola, na ni thibitisho kwa mja la uja wake.

Ubeti huu unaotaja sijida ndio unamkumbusha kiumbe asili yake na hivyo kumhimiza anyenyeknee mbele ya Muumba wake. Mwanadamu aliumbwa kutokana na udongo na afapo mwili wake utazikwa udongoni. Kitakachonusurika ni roho ya mwanadamu na ndiyo maana mtunzi huyu wa *Inkishafi* anahimiza moyo wake kusujudu kwa Mola wake.

Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* mtunzi wake ambaye alikuwa akiishi katika kasri la kifalme anamuusia binti yake asitangamane na watumwa maana katika utamaduni wao watumwa walikuwa watu wa daraja ya chini ambao hawakuwa na haki ya kujumuika pamoja na watawala wao katika shughuli nyingi za kimaisha. Anamwambia bintiye hivi:

20. Sitangamane na watuma,

Illa mwida wa khuduma,

Watakuvutia tama,

Labuda nimekwambiya.

21. Sandamane na wayinga,

Wasoyua kuitunga,

Ziumbe wasio changa,

Wata kuwakurubiya.

Lakini vilevile anampa ushauri wa mambo ya kuzingatia ili pindi atakapokufa asipatwe na taabu ya jehanamu bali apate mema ya peponi. Beti zifuatazo zinathibitisha hayo:

22. Mama pulika maneno,

Kiumbe ni radhi tano,

Ndipo apate usono,

Wa akhera na duniya.

23. Nda Mngu na mtumewe,

Baba na mama wayuwe,

Ya tano nda mumewe,

Mno imekaririwa.

24. Na awe radhi mumeyo,

Siku zote mkaayo,

Siku mukhitariwayo,

Awe radhi mekuwiya.

25. Na ufapo wewe mbeye,

Radhi yake izengeye,

Wende uitukuziye,

Ndipo upatapo ndiya.

26. Na siku ufuliwayo,

Nadhari nda mumeyo,

Taulizwa atakayo,

Ndilo takalotendewa.

27. Kipenda wende peponi,

Utapekwa dalihini,

Kinena wende motoni,

Huna budi utatiwa.

Haya mafunzo kuhusu kifo na siku ya ufufuo ni mapokezi ya kidini na utamaduni. Dini ya Kiislamu inafunza kuwa wanawake wako chini ya mamlaka ya waume zao lakini swala hili la waume kuwa na mamlaka juu ya mahali wake zao wanapaswa kuwekwa peponi ni kazi ya mtunzi. Huenda Mwana Kupona alimtaka bintiye awe mnyenyeketu zaidi ndiposa akatia chumvi kuhusu mamlaka ya mwanamume. Kwa mujibu wa Timammy na Swaleh (2013) mafunzo haya ya kidini na kitamaduni yamekuja kupokelewa na kuingizwa katika utamaduni wa Waswahili na ikawa itikadi za unyagoni ambazo mabinti hufunzwa kabla ya arusi zao.

Jamii zote ulimwenguni zina malezi tofauti tofauti kwa kutegemea uana. Imani za kijamii hupitishwa kwa watoto kwa kuzingatia jinsia zao na hivyo kuathiri imani yao. Kutoka kizazi kimoja hadi kingine mafunzo haya hupitishwa kwa watoto kuptitia wazee wao. Hali hii ndiyo inayomfanya mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* kumtungia bintiye wosia huu katika umbo la tenzi ili amshauri na kumwelekeza kwenye misingi ya jamii yake kama yeche alivyolelewa. Anasema hivi kwa bintiye:

*8. Twaa nikupe **hirizi**,*

Uifungeto kwa uzi,

Uipe na taazizi,

Upate kuiangaliya.

Anazidi kumwelekeza hivi:

52. Naliowa na babako,

Kwa furaha na ziteko,

Tusondoleane mbeko,

Siku zote twaloka'a.

53. Siku moya tusitete,

Ovu langu asipate,

Na lake lisinikute,

Hata akakhitariwa.

54. Yalipokuya faradhi,

Kanikariria radhi,

Kashukuru kafawidhi,

Moyo wangu katushiya.

Neno '*hirizi*' limetumiwa hapa kushuhudia kuwa kulikuwa na imani za uganga katika jamii ya mtunzi. Hirizi ni kinga dhidi ya mabaya ambayo yaweza kumkumba mtu. Japokuwa Waswahili hukisiwa kuwa wengi wao ni waislamu, baadhi ya itikadi zao na tamaduni zao huegemea zile

itikadi ya jamii mbalimbali za Kiafrika. Hii ni kwa sababu Waswahili ni Waafrika. Chiraghdin na Mnyampala (1977) wanasema:

Utamaduni wa Kiswahili chimbuko lake ni mwambao wa Afrika Mashariki. Ukichukua tawi lolote la mila na utamaduni wake utaona kuwa shina lake ni Afrika. Ukichukua matanga ya Kiswahili, harusi, malezi, itikadi, ukiyalinganisha na ya Kiarabu utaona kuwa ada zao ni tofauti. Utamaduni wa Kiswahili, mazingira yake hasa ni ile sehemu ya nchi iliyopakana na maji ya pwani.

Mulokozi (1999) pia anakubaliana na mawazo ya Chiraghin na Mnyampala (1977) kwa kusema:

Waswahili ni Waafrika, hata kama wamechanganyika na watu wengine kutoka nje ya bara hili. Waafrika wanazo mila na desturi zao za jadi kuhusu mahusiano ya watu katika ndoa na maisha kwa jumla ambazo huwafundisha watoto wao.

Naye Massamba (2002) anasisitiza jambo hili kwa kusema:

Hapa ni muhimu kusisitiza kwamba Uislamu uliwakuta wenyeji (Waswahili) na lugha yao (Kiswahili) na kamwe haukuleta Kiswahili. Tunasisitiza hili kwa sababu kuna baadhi ya watu wenye fikira potofu wanaodhani kwamba Uislamu ndio ulioleta Kiswahili, na kwamba Kiswahili hakiwezi kutenganishwa na Uislamu. Fikira hizo potofu ndizo pia zinawafanya watu wa aina hiyohiyo washindwe kutofautisha Uislamu na Uarabu, kama ambavyo kuna baadhi ya watu wasioelewa wanavyoshindwa kutofautisha Ukristo na Uzungu.

Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa, baadhi ya itikadi za Kiafrika kama vile dhana ya uchawi na imani kuhusu hirizi kumkinga mtu dhidi ya maangamizi ilisisitizwa. Hii ndiyo maana Mwana Kupona anamsisitizia binti kuwa wosia anaompa ni hirizi, yaani kinga ya maovu dhidi ya maangamizi. Mwanakupona anamkusudia mwanawe mema kuitia wosia huu anaompa. Endapo atafuata wosia huu kikamilifu basi atapata kinga dhidi ya maovu yanayomwandama. Kisha beti tatu tulizozinakili hapo huonyesha namna mabinti walikuwa wanalelewa na hawakupaswa kwenda kinyume na waume zao kwani hata katika kifo mume bado ni kiongozi na siku ya ufuluo ye ye ndiye ataulizwa mahali anapostahili kuwekwa mke wake. Kama beti zifuatazo zinavyofafanua:

26. Na siku ufuliwayo,

Nadhari nda mumeyo,

Taulizwa atakayo,

Ndilo takalotendewa.

27. Kipenda wende peponi,

Utapekwa dalihini,

Kinena wende motoni,

Huna budi utatiwa.

Mawazo haya ya mtunzi kuhusu kifo na mahusiano baina ya mume na mke hutokana na malezi na mafunzo aliyopewa na ndiyo hayo anampitishia mwanawe. Yamkini mafunzo ya kidini na kitamaduni yanashikana hapa katika kumweka mwanamume mbele kitabaka huku mwanamke

akiwa chini ya mamlaka ya mumewe. Hata katika mauti siku ya ufuluo Mungu atamuuliza mume mahali pa kumweka mkewe.

Utafiti huu uling'amua kuwa, utamaduni wa jamii ya mwandishi na mazingira huchangia pakubwa katika usawiri wa dhana ya kifo.

4.4.3 Lughha na mauti

Chimerah na Njogu (1998) wanasema kuwa fasihi ni sanaa ya lughha. Ili msanii apate kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira kwa njia inayofaa lazima atumie lughha itakayosawiri mawazo yake vema. Lakini lughha pia huwa na sajili zake kwa kutegemea uwanda wa matumizi na uelewa wa mtunzi. Mtunzi wa *Inkishafi* anateua lughha yake mwafaka kuoana na Pate ya wakati wake. Ni lughha ambayo huonekana kuwa ngumu kutokana na mabadiliko ya wakati lakini imewafiki vilivyo usimulizi wake. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* mtunzi anatumia lughha sahili na anaeweka wazi kwa sababu mwenyewe amekiri kuwa si mtunzi bali ni mtu anayetoa tu mawaidha yake kishairi. Katika *Inkishafi* tunakumbana na Kiswahili cha kale kilicho na ukwasi mkubwa wa msamiati. Mtunzi wa utenzi huu naye ni mshairi na ametokana na ukoo wa malenga farisi wa ushairi wa Kiswahili. Katika shairi la ‘Usiniuwe’ katika *Sauti ya Dhiki* tunapata lahaja ya Kimvita ikitumiwa na mtunzi huyu kutokana na uelewa wake wa lahaja hii vema. Beti hizi za *Inkishafi* zinadokeza ukomavu wa mtunzi katika utanzu wa ushairi akisema:

13. Hunu ulimwengu bahari tesi,

Una matumbawe na mangi maasi,

Aurakibuo juwa ni mwasi,

Kwa kulla khasara ukhasiriye.

*14. Ni kama kisima kisicho ombe,
Kwenye mtapaa mwana wa ng'ombe,
Endao kwegema humta pembe,
Asipate katu kunwa maiye.*

Mtunzi huyu anaelewa mazingira ya bahari namna inavyojaa na kupwa huku ikivuruga ushwari wa usafiri. Akamithilisha ulimwengu na bahari akisema, '*Hunu ulimwengu bahari tesi*'. Yaani ulimwengu umejaa vituko vingi na anayeuanadama hafaalu kamwe kuona raha maana utampiga kumbo, '*Endao kwegema humta pembe*' kisha '*Asipate katu kunwa maiye*' na mwisho wao ni kukumbana na mauti:

*22. Tandi la mauti likawakuta,
Wakauma zanda wa kuiyuta,
Na dunia yao ikawasuta,
Ichamba safari munipukiye.*

Walipoaga dunia milki yao ikaharibika na kupoteza uzuri wake:

*45. Sasa walaliye moyo shubiri,
Pasipo zulyia wala jodori,
Ikawa miwili kutaathari,
Dhiki ya kaburi iwakusiye.*

Uteuzi wa maneno '*jodori*' na '*kutaathari*' ambayo ni ya kilahaja na Kiarabu mtawalia umeleta urari wa vina na mizani huku maneno haya yakijenga taswira ya kifo kikamilifu katika upweke

na mateso makuu. Maneno haya kwa kawaida yangekuwa kama yafuatayo na yangekosa urari wa vina na mizani:

Kipate/Kiarabu	Kiswahili Sanifu
Jodori	Godoro
Kutaathari	Kuathirika

Katika shairi la ‘Usiniuwe’ katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*, matumizi ya lahaja ya Kimvita yamemwezesha mtunzi wake kuteua kina cha ‘ya’ katika kibwagizo chake. Kina hiki kinadhihirisha taswira ya kutamauka au ukosefu wa nguvu mbele ya mamlaka makuu kwani ni silabi huru ya nusu irabu na irabu inayotamkwa bila nguvu nyingi. Mtoto tumboni mwa mamake akilia asiuwawe anaonyesha unyonge huo kama tunavyoshuhudia katika beti zifuatazo:

1. Mama nimekukosani? Nambiya nami nijuwe

Nimetenda jambo gani, ovu liso mfanowe?

Lazima hiyo nda nini, ushikayo uniuwe?

Hebu iwa na imani, mamangu nihurumiya.

Kisha katika beti tatu za mwisho kina hiki cha ‘ya’ kinaonyesha kule kutamauka kwa mtoto tumboni mwa mamake huku akisihi kwa unyonge aachiwe uhai wake azidi kuishi. Beti hizi zinaonyesha hali hiyo hivi:

27. Uhai! Nakuliliya, wewe ndiye upendwaye,

Uhai! Huna ubaya, yupi akutukiyaye?

A! Uhai niombeya, mamaangu sema naye,

Pengine atasikiya, asiniuwe mamangu.

28. Nawe Haki nisemeya, kwa ya dhati matamshi,

Sema na kuniombe ya, nihururumiwe niishi,

Mamangu anioneya, anioneya bilashi,

A! Haki nihukumi ya, asiniuwe mamangu.

29. Mauti! Nihurumi ya, Mauti! ‘Sinitukuwe,

Lipi nilokukose ya? Hatuna vita mi nawe,

Toba! Nisikitiki ya, nisalimisha na wewe,

Magoti nakupigi ya, simsikize mamangu.

Uteuzi wa misamiati katika ushairi humsaidia mshairi kudhihirisha taswira nyingi na tofautitofauti. Kutohana na mifano mbalimbali tuliyotoa, taswira ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili ni ya namna tofauti tofauti.

4.5 Visababishi vya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili

Tukio la kifo mionganii mwa wanajamii mbalimbali kote ulimwenguni hutazamwa kama jambo lisilo la kawaida na daima hutafutiwa chanzo au kisababishi. Mionganii mwa wanajamii wa Kiafrika hudaiwa kuwa kila kifo mara nyingi hutokana na mkono wa mtu. Alembi (2001) anasema kuwa mionganii mwa jamii ya Abanyore hata kama inajulikana kuwa mtu amekufa

kutokana na malaria bado kuna madai kuwa ugonjwa huo umeletwa na mtu ambaye ama ni mchawi au alifanya kitendo kisichofaa. Alimradi kila kitu kina sababu zake nje ya nguvu za kawaida za kimaumbile. Mvua ikikosa kunyesha wakati mwafaka na kukatokea ukame, huwa kunaelezwa kuwa Mungu amekasirika au kuna mmoja wa wanajamii aliyekufuru. Kukinyesha mvua na mafuriko yakaja, hufasiriwa kuwa tendo fulani la wanajamii limesababisha hayo. Hii ndiyo hali inayotokea pindi kifo kinapobisha hodi mlangoni na kumchukua mmoja wa wanajamii. Kifo si kifo bali kina sababu maalum ya kutokea kwake. Mashairi teule ya Kiswahili yamesheheni uhalisia huu wa maisha kuwa kifo kina kisababishi fulani. Kutokana na mila na itikadi zilizowakuza washairi tuliwashughulikia, kifo hutokana na Mungu, shetani na mtu mwenyewe.

4.5.1 Mungu

M'Ngaruthi (2008) anaeleza kuwa nyimbo za kidini huimbwa zinazolenga kuwafahamisha waliobaki kuwa kifo si ajali bali ni mapenzi ya Mungu. Pia huwashauri juu ya maisha baada ya kifo.

Mungu ni muumba wa yote na ana uwezo wa kuumbua kiumbe wake pindi akiona kuwa ni nafuu kufanya hivyo. Mungu habagui wakati wa kuua kwani ni adhabu ambayo alitoa kwa kila kizazi cha Adamu. Haya ni mafunzo ambayo yamejikita katika dini za Kiislamu na Kikristo. Mafunzo haya husisitiza kuwa mwanadamu ni kiumbe ambaye yuko katika mapito ya maisha yake duniani na anahimizwa kutopenda dunia maana si makao yake ya kudumu. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* tunaarifiwa kuwa Mungu ndiye anaamua lini apate kumchukua kiumbe wake. Ubeti ufuatao unathibitisha madai hayo:

67. Kwani yote tunenayo,

Mwana adamu ni puwo,

Mola ndiye awezawo,

Kupoteza na kongowa.

Ubeti huu una mawazo sawa na ule wa *Utenzi wa Qiyama* unaosema:

14. Mwando wake fahamuni,

Atakapo Rahamani,

Kutondowa duniani,

Awaliye tawambiya.

Mungu anasawiriwa kama muweza wa kumpa kiumbe uhai na kuutoa uhai huo pindi anaporidhia. Hivyo basi mwanadamu anafaa ajitahidi kutubu dhambi zake kwa Muumba ili apate kusamehewa. Mwana Kupona anzidi kutoa toba yake kwa Mungu hivi:

78. Nondolea ndwee mbovu,

Yaloningia kwa nguvu,

Dhambi zangu na maovu,

Ya Rabbi nighofiriya.

79. Kwetu yangawa mazito,

Kwako wewe ni matoto,

Nepulia uvukuto,

Unepuke mara moyo.

Wakati kifo kinapotokea katika jamii mbalimbali, itikadi na imani iliyopo ni kuwa Mungu ndiye ameleta kifo. Okombo (1983) akiandika kuhusu jamii ya Waluo kupitia mhusika wake Okune, anasema kuwa watu humwomba Mungu amrehemu aliyefariki ili alale pema peponi. Wanaamini kuwa huko peponi ndiyo makao ya watu wote waliotangulia kufa na waliobaki duniani. Duniani mwanadamu husawiriwa kama msafiri ambaye baada ya muda fulani atatoweka akifikia ukingo wa safari yake.

Mwanadamu pindi afapo hupewa malipo na Mungu kulingana na matendo yake duniani. Wale waliowadhulumu wenzao watalipwa kwa dhuluma zao na wale waliotenda mema watalipwa kwa wema wao. Mtunzi wa *Inkishafi* anatwambia hayo katika beti zifuatazo:

69. Namua na huyo menidhilimu,

Kwa hukumu yako iliyo nyumu,

Mungu Jabari akahukumu,

Amtendeleo ampalipiye.

70. Na malipwa yao wadhillimuwa,

Si dhahabu timbe si ya kufuwa,

Fedha hawatwai na wangapowa,

Ila hasanti ni malipwaye.

71. Aso hasanati wala thawabu,

Hufungwa kitaya kama rikabu,

Akatwekwa dhambi za maghusubu,

Akambiwa haya mtukuliye.

Mungu ndiye anatoa hukumu kwa waja wake, ‘*Mungu jabari akahukumu*’. Hukumu kwa mwovu ni, ‘*Hufungwa kitaya kama rikabu*,’ kisha aliyemdhulumu mwenzake akaambiwa akipungukiwa na mema ya kulipa mwenzake basi maovu ya yule mdhulumiwa anaongezewa yeze dhali, ‘*Akatwekwa dhambi za maghusubu, Akambiwa haya mtukuliye*’.

Hata mtoto tumboni mwa mamake anahisi kuwa kila mwanadamu amepangiwa siku zake za kuishi duniani na Mungu wake. Anahisi kuwa Mungu ndiye ana uwezo wa kumhukumu mja kwa kumtoa uhai lakini mwanadamu mwingine hana ruhusa hiyo. Hii ndiyo inamfanya anamkataza mamake kumuua kama asemavyo katika shairi la ‘Usiniwe’ katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* akimwambia mamake hivi:

*10. Na hilo pande la damu, likakaa kwa salama,
Likingoja yake zamu, aloiweka Karima,
Zamuye ilipotimu, nikawa nofu la nyama,
Basi usinihukumu, mamangu nihurumiya.*

Katika ubeti huo mtunzi anabaini kuwa kila mja ana siku zake ambazo Mungu amemtengenai ili apate kuishi, ‘*Likingoja yake zamu, aloiweka Karima*’ na mja hana nafasi ya kumharibia mwenzake siku zake za kuishi, ‘basi usinihukumu.’ Ni Mungu ambaye ana ufahamu wa lini na wapi mtu atapata kufariki maana hiyo idadi ya siku ameshazipanga kuanzia siku ya kuzaliwa hadi siku ya kufariki.

4.5.2 Shetani

Shetani amechukuliwa katika ngano za makabila mbalimbali kama mwenye nguvu na uwezo wa kusababisha mauti. Katika simulizi za jamii za Wabukusu, inaaminika kuwa shetani ni mwovu na mwenye uwezo wa kuua mwanadamu. Hali hii ndiyo tunakumbana nayo katika jamii ya Waluo, mkoani Nyanza. Mhusika mmoja katika Okombo (1983) kuhusu kifo cha mke mwenza wake ajulikanaye kwa jina la Nyar Abayo anapotoa rambirambi zake anaona kuwa kifo cha mke mwenzake ni kazi ya shetani. Anasema hivi:

Uk.17. Nimeshangaa sana kutokana na kazi na nguvu za shetani ambaye amemchukua Nyar Abayo.

Shetani ni adui mkubwa wa Mungu. Yeye alitupwa duniani baada ya kumwasi Mungu na hivyo akapata mamlaka ya kuitawala. Mafunzo haya yapo katika Biblia na Qur'an. Imani za jamii mbalimbali za Kiafrika pia huonyesha kuwa shetani ni adui wa Mungu na kila mara hujaribu kumpotosha mwanadamu kwa kumwingiza katika maovu ambayo yanavutia lakini yenye maangamizi kwa kiumbe. Mwanadamu kwa hivyo huhimizwa kutomwandama shetani maana ni mlaanifu na mwangamizi mkubwa. Hivyo shetani hufanya kila juhudhi ili kupata wafuasi wengi kwa kuwafanya waasi mienendo mema ya Mungu na mwishowe akawatia kwenye maangamizi. Mtunzi wa *Inkishafi* anatueleza hivi kumhusu shetani na uangamizaji wake:

30. Ewe moyo enda sijida yake,

Hela tafadhali unabihike,

Shetani rajimi asikuteke,

Kesho kakuona kuwa kamaye.

Ili moyo ujinusuru ni bora kumrudia Mungu ili mwovu shetani asije akauchukua kwa kuufisha maana shetani kalaaniwa ‘*shetani rajimi*’. Anayemfuata shetani mwishowe hulingana naye, ‘*Shetani rajimi asikuteke, kesho kakuona kuwa kamaye*’. Maisha halisia pia huonyesha hali kama hii kwa kuwa mtu anayetembea na mwovu mara nyingi huwa mwovu pia kwa kuiga na kutenda. Mtoto wa nyoka ni nyoka.

Naye mtunzi wa ‘Usiniwe’ katika *Sauti ya Dhiki* kuititia sauti ya mtoto akilalamika dhidi ya kuuawa anasema:

*13. Kunipa ulikubali, uhai tangu kitambo,
Kabla sijawaswili, humuno ndani mwa tumbo,
Sasa niya ‘mebadili, wataka geuza mambo,
Usiwe sawa na nduli, mamangu nihurumiya.*

Hapa muuaji anamithilishwa na nduli (shetani) ambaye kazi yake ni kuua na kuangamiza roho za watu. Ubeti huu unasawiana na mawazo ya Beieldelman (1963) anayeeleza kuwa katika jamii ya Wakaguru kule Tanzania kuna imani kubwa kuhusu uwezo wa shetani kusababisha kifo cha mtu. Mtoto katika ubeti tulionakili hasemi kuwa mama yake ni shetani bali anammithilisha na shetani. Inaashiria kuwa shetani ni mwangamizaji. Hii ndiyo sababu anamwambia mamake, ‘**Usiwe sawa na nduli, mamangu nihurumiya.**’ Neno nduli ni kisawe cha shetani au mwovu na mwangamizaji. Mamake ambaye anakakawana kumuavya anaonekama kuwa na roho mbaya kama shetani ambaye kiumbe tumboni mwa mama anahisi ni mwovu na mwangamizaji.

4.5.3 Mtu kwa mtu

Jamii nyingi za Kiafrika huwa hazisadiki kuwa kifo huweza kutokea bila ya ‘mkono wa mtu’ kuwepo. Kila kifo cha mwanajamii hutokana na mtu mwingine. Wakati wa mazishi nyimbo za mbolezi hutumika kukashifu huyu muuaji. M’Ngaruthi (2008) anadai kuwa mbolezi ni nyimbo ambazo huimbwa kuomboleza mtu aliyefariki. Katika baadhi ya tamaduni, nyimbo hizi hazitumiki tu kuomboleza bali kulalamikia asili ya kifo hicho. Inaweza kudaiwa kupitia nyimbo kuwa marehemu alirogwa, kuuawa kwa kuumizwa na mtu au mnyama. Baadhi ya nyimbo hutumika kumlaani yejote aliyejusishwa na kifo hicho. Hata hivyo, si mabaya tu yanayotajwa katika nyimbo hizi. Baadhi yake hutungwa kumsifu marehemu kwa wema alioutenda akiwa hai na kuwatolea changamoto waliobaki kuwa wauige wema wake.

Alembi (2001) akitafitia jamii ya Abanyore na Sangree (1966) akitafitia jamii ya Tiriki ambazo ni za Kibantu wanakubaliana kuwa katika jamii hizi hakuna kifo kinachokuja bila sababu hata kama mtu amezeeka sana. Kila kifo katika jamii hizi husababishwa na ‘mkono wa mtu’. Japo mwanadamu anajua kuwa siku moja atakufa, hajui ni lini na ni wakati upi kifo chake kitampata. Vilevile hajui ni kitu kipi kitasababisha kifo chake. Mara nyingi tokeo la kifo hutazamwa kama limechangiwa na mtu hata kama si kwa uganga au urogi. Kwa mfano, dereva wa gari la abiria akipata ajali na kuangamiza kila mtu, pengine abaki hai atahukumiwa kwa kuua. Asipobaki hai watu watamlamu kwa kuendesha gari kwa kasi au kutozingatia masharti ya uendeshaji wa magari barabarani. Hata kama gari litakuwa bovu bado lawama zitamwandama kwa kutotengeneza gari kabla ya kulipeleka barabarani. Alembi (2001) akitafitia mashairi ya mbolezi katika jamii ya Abanyore, anaeleza kuwa katika jamii hii kifo mara nyingi huaminika kuwa husababishwa na watu waovu. Watu hawa hudaiwa kuwa mara nyingi ni wachawi. Katika

maombolezo ya watu ambao hushukiwa kuwa hawa wachawi wamechangia katika kifo chao huwa kuna onyo katika mbolezi kwa washukiwa wa uchawi na mauaji ya marehemu anayeombolezwa. Wachawi hawa huonywa kuwa hawatanusurika maana wao pia watakufa siku moja. Alembi (2001:77) anatupatia mfano wa mbolezi inayotumiwa kuwakanya hao washukiwa wa mauaji kama hivi:

Omwana wa Anjichi

Mwana wa Anjichi

Ukholle mbwena?

Umenifanyia nini hii?

Sese wa Anjichi

Sese wa Anjichi

Ukholle mbwena

Umenifanyia nini hii?

Nangwe mbwena?

Ni nini itakuja kunipata?

Nandeletenge khulusina bane?

Nitaegemea nini?

Omwana wa Anjichi

Mwana wa Anjichi

Ukholle mbwena

Umenifanyia nini hii?

Ye, ye, ye, ye

Ye, ye, ye, ye

Murebe Emuhaya

Ulizia Emuhaya

Murebe Emuhaya

Ulizia Emuhaya

Tsia murebe Oluhano Emuhaya eh

Ulizia chifu Oluhano kule Emuhaya

Omwana wanje wandatola bululu bane

Mwanangu niliyempata kwa uchungu

Rebanga Anjichi waikhole mbwena

Nakuuliza Anjichi ulinifanyia nini?

Ye, ye, ye, ye

Ye, ye, ye, ye

Sindi nomulembe bana befwe

Sina amani watu wangu

<i>Otemba oboye mukoloba ye, ye</i>	<i>Otemba aliyasema jana ye, ye</i>
<i>Inyumba esimbanga</i>	<i>Nyumba ya vivu</i>
<i>Khuliakana iyo</i>	<i>Tutakutana huko</i>
<i>Inyumba esimbanga ye, ye</i>	<i>Nyumba ya vivu</i>
<i>Inyumba esimbanga ye!</i>	<i>Nyumba ya vivu!</i>

Katika shairi hili, '*Inyumba esimbanga*' imerudiwarudiwa kuonyesha kuwa ni mtu fulani ndiye aliyesababisha kifo cha Anjichi. Lakini huyo mtu anaonywa kuwa mambo aliyoyatenda hayajaisha maana hata naye atakiona cha mtema kuni, '*Khuliakana iyo*'. Muuaji huyu anajulikana mionganoni mwa wanajamii hii japo hatajwi kwa jina. Hii ndiyo maana watu wanaambiwa waulizie kule Maseno na Emuhaya, '*Murebe Emuseno... Murebe Emuhaya*'. Hata chifu wa eneo moja kule Emuhaya anamjua huyu muuaji wa Anjichi, '*Tsia murebe Oluhano Emuhaya eh*'. Kwa hivyo huyu muuaji hasingiziwi maana anajulikana kotekote katika eneo hili. Hili tukio la watu kushukiwa kuwauwa watu wengine kwa njia za kichawi au nyinginezo lipo katika maisha halisia.

Hali tunayokumbana nayo katika mashairi teule ya Kiswahili ni tofauti na mbolezi tuliyotoa hapo juu japo kisababishi cha kifo ni kilekile. Katika mbolezi muuaji hushukiwa kutumia nguvu za kichawi katika kumuua *Omwana wa Anjichi* tofauti na mashairi tuliyoteua ambayo huonyesha kuwa mtu ndiye anayesababisha kifo cha mwenzake lakini bila ya kutumia nguvu za kichawi. Badala yake anakusudia kuua kwa kuavya. Katika shairi la 'Usiniwe' kutoka *Sauti ya Dhiki* mtoto tumboni mwa mamake anamlamu kwa kusudi la kutaka kumwavya na kumnyima haki ya

kuishi. Anamwona mamake kuwa ana mamlaka juu ya kifo na hivyo anamsihi asimuue kwa kosa lisilo lake:

8. Ni manii tone moja, la maji madhalilifu,

Tone lililojituja, kutoka maji machafu,

Ndicho chanzo changu kuja, na bado ndiya ni ndefu,

S'anze sasa kunifuja, mamangu nihurumiya.

9. Tone lilipoanguka, mahalipe maalumu,

Hapo likahifadhika, kungoja muda utimu,

Kisha likabadilika, nikawa pande la damu,

Wata roho kunipoka, mamangu nihurumiya.

10. Na hilo pande la damu, likakaa kwa salama,

Likingoja yake zamu, aloiweka Karima,

Zamuye ilipotimu, nikawa nofu la nyama,

Basi usinihukumu, mamangu nihurumiya.

16. Kama hunitaki mama, piya waniuliyani?

*Nakuomba nikisema: **usiniuwe tumboni,***

Mama nizaa salama, kisha nitupa ndiyani,

Mja alo na huruma, an'okote kunileya.

Mauaji haya yanakisiwa kuwa na sababu mbili kuu; mwanzo ni kutokana na aibu na kuogopa kusemwa na watu. Mtunzi anatuambia hivi:

24. *Kwamba waicha aibu, na makanwani kutiwa,*

Hizino ndizo sababu, za kutaka kuniuwa?

Haya yasingekuswibu, ungelitunga muruwa,

Mwenyewe uliharibu, mamangu nihurumiya.

Pili ni kutaka heshima au kutafuta kustahikiwa mionganoni mwa watu:

25. *Kutaka ustahiki, na kuitaka hishima,*

Hakuwezi kupa haki, kuniuwa wangu mama,

Na ovu lako kubaki, litabakiya lazima,

Hilo halizamishiki, mamangu nihurumiya.

Huenda mama anayekusudia kumwavya mtoto wake alipata mimba hiyo kwa njia ambayo si nzuri. Pengine ni mimba ambayo ililetwa na kushiriki mapenzi kiholelaholela. Mimba kama hizi zina madhara mengi kama asemavyo Nyanje (2009) katika ubeti ufuatao:

Aidha nawaarifu, katika hii shajara

Ambaani uzinifu, una adha na madhara

Nangoja siku ya ufu, siku ya kwenda akhera

Mojawapo ya madhara ya uzinifu ni kuwaan mzini fu anaweza kupata mimba bila mipango na hivyo mwenye mimba akaunda dhamira ya kumwavya mtoto tumboni mwake. Wakati mwingine uzinifu huweza kueneza magonjwa ya zinaa.

Kama ilivyo jamii nyingi za Kiafrika kifo kina sababu zake na muuaji huwa na analolikusudia kama tulivvosawiriwa katika beti hizo. Muuaji wakati mwingine huua kutokana na wivu na wakati mwingine huua ili apate sifa au heshima mionganii mwa wanajamii. Sifa hizo ni pamoja na kuogopwa kuwa fulani ni katili na haogopi chochote hata kuua. Nyingine ni kupata kuheshimiwa na watu kama asemavyo mshairi '***Kutaka ustahiki, na kuitaka hishima.***'

4.6 Utata wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili

Fasiri ya dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili hujitokeza kuwa ni kitu kigumu ambacho kina sura anuwai na hupokelewa kwa namna mbalimbali mionganii mwa wanajamii. Utata huu hujitokeza katika kuelewa mwanzo na mwisho wa maisha, maisha baada ya kifo, uteuzi wa msamiati katika kulizungumzia swala la kifo pamoja na uwezo wa kuzungumza na Mungu katika ufu.

Ni vigumu kung'amua lini na wapi kifo huanza na maisha huisha. Hii ni kwa sababu wataalamu wengi waliolitafitia swala la kifo katika jamii mbalimbali wanadai kuwa kwa mujibu wa jamii hizo, waliokufa bado wana uwezo wa kurudi wakawadhuru walio hai. Kwa mfano, Mbiti (1969) anasema kuwa katika jamii za Kiafrika kifo si mwisho wa maisha bali ni mwanzo wa kuishi kwa namna nyingine. Mawazo haya yanashadidiwa na Alembi (2001) akitafitia jamii za Abanyore nchini Kenya. Katika mauti kuna mengi yanayodaiwa kuendelea kana kwamba kungali kuna uhai. Wakati mwingine kuna mengi ambayo hudiwa kuendelea katika mauti kama vile adhabu na kuzawadiwa peponi, mazungumzo na Mungu, utabaka na kutobainika mwanzo na mwisho wa maisha.

4.6.1 Adhabu na kuzawadiwa peponi

Imani za dini mbalimbali ulimwenguni hudokeza kuwa kuna siku ya kiyama ambayo wafu watafufuliwa. Wabaya watapewa adhabu na wazuri watazawadiwa. Kwa mujibu wa Mbiti (1969) imani za wakristo ni kufufuliwa siku ya mwisho wa dunia na kuenda mbinguni kuishi na Mungu huku waasi wakipelekwa katika moto wa milele. Dini ya Kiislamu vilevile inashikilia kuwa kuna adhabu baada ya kufa kwa wale watendao maovu huku wema wakizawadiwa. Mafunzo haya ya Kiislamu yanashadidiwa na Qur'an inayotueleza kuwa kuna kuzawadiwa kwa wema huku wanaume waliofuata sharia wakipewa huruleini sabini. Walioasi watatupwa kwenye moto wa daima. Imani hii ya Kiislamu ndiyo nguzo ya mawazo ambayo yanajitokeza kuhusu swala la kifo katika mashairi teule yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Sivananda (1997) imani ya dini ya Kihindi huonyesha kuwa kuna kuzaliwa upya kwa kiumbe kwa kutegemea matendo yake katika maisha ya awali kabla ya kifo. Aliyeishi maisha mema huzaliwa katika tabaka la juu baada ya kufa kwake ilhali aliyeishi maisha ya vurugu tupu huzaliwa katika tabaka la chini. Hali hii huendelea daima na hivyo kudhihirisha kuwa maisha na kifo havina mwisho ila ni mabadiliko ya kiwakati.

Katika mashairi teule tuliyoyashughulikia tunakumbana na hali hii ya kuwepo kwa adhabu baada ya kufa. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* mtunzi anapomshauri bintiye namna ya kuishi duniani akijiandaa kwa maisha ya ahera anasema hivi:

73. Ya Allahu wangu wana,

Nimekupa ni amana,

Watunde Mola Rabbana,

Siwate kuwangaliya.

74. Nimekupa duniani,

Watunde uwahizini,

Unipe kesho peponi,

Mbee za Tumwa Nabiya'

Mtunzi wa shairi hili anamwomba Mungu apate kumtunuku mema kesho katika ahera. Hii ni wazi kuwa katika ahera kuna kuzawadiwa na kuadhibiwa kulingana na matendo ya mtu. Ndiposa mtunzi huyu akasema, '*Nimekupa duniani... Unipe kesho peponi*'. Yaani amamtunza bintiye kwa kumwelekeza kwa njia ya Mungu na kesho pindi afapo apate kuzawadiwa kule peponi.

Katika *Inkishafi* mtunzi hutuambia kuwa kuna adhabu ya moto kwa waasi kule mbinguni. Anatueleza aina ya mioto ambayo itatumika katika kuwaadhibu wale waovu ambaowalimwasi Mungu. Anatuambia mambo haya katika beti zifuatazo:

74. Kuna na hawiya pulika sana,

Ni moto mkali hau makina,

Asi angiapo hula kitana,

Huona pumuzi zimsiziye.

75. Moto wa sairi ufahamuto,

Ni moto mkali katika nyoto,

Ni mngi wa moshi na mitukuto,

Na majoka na pili waikaliye.

76. *Na moto wa ladha nao pulika,*

Moto ukitiwa mara huwaka,

Huona manofu yakikwambuka,

Waona ziungo ziungushiye.

77. *Fahamia tena sio Hutama,*

Motowe muwashi na kunguruma,

Huvunda mifupa hupisha nyama,

Bongo na wasakha limshushiye.

Kuna mioto ya hawiya, sairi, ladha na hutama ambayo itakuwa adhabu kwa waasi. Hii ni mionganini mwa mioto inayotajwa katika Qur'an ambayo kwa ujumla ni nar, ladha, saqara, saira, hutama, jahima na darkul-asfal. Inadhihirika hapa ni kuwa hata katika mauti kuna uhai, ndiyo maana kuna adhabu kwa waasi. Kama hakungekuwa na uhai ni jinsi gani wafu wangepewa adhabu? Licha ya hayo mwanadamu hushauriwa aishi vema ndipo apate mema peponi. Mtunzi huyu anazidi kutuambia hivi:

78. *Sasa takhitimu tatia tama,*

Atakofuata na kuyandama,

Tapata khatima na mwisho mwema,

Rabbi twakuomba tujaaliye.

Mtu anayesikiza aambiwalo haishii na majuto. Mtunzi wetu huyu anahimiza watu wafuate mashauri yaliyo mema ili wasipatwe na majuto ya kutiwa motoni bali wawe na mwisho mwema uliojaa shangwe na raha tupu.

4.6.2 Mazungumzo na Mungu

Katika kazi nyingi za fasihi tunaona mahali ambapo mhusika au wahusika baada ya kifo wanawekwa mkabala na Mungu kujadiliana. Kazi ambazo zina sifa hii ni pamoja na *Rosa Mistika* (1980), *Amezidi* (1990) na *Visiki* (1983). Katika riwaya ya *Rosa Mistika* tunashuhudia mazungumzo baina ya Rosa na Mungu baada ya Rosa kujiua. Mungu anapomuuliza kuwa ni kwa nini aliamua kujiua, Rosa anamwarifu kuwa ulimwengu ulimlea vibaya na babake ndiye alimlea visivyo. Tamthilia ya *Amezidi* nayo inatupatia picha ya mazungumzo baina ya Ame na Zidi pale ambapo Zidi ametangulia kufa naye Ame yuko duniani wakijadiliana. Haya ni mazungumzo baina ya kuzimu na dunia. Tamthilia ya *Visiki* nayo inatupatia picha ya wananchi amba walichochewa na Bi Tamaa na Bwana Ndovu, wakapigana na kuuana. Siku ya kiyama ilipofika walienda mbele ya Mungu kushtaki uchochezi wa hawa watu wawili, Bi Tamaa na Bwana Ndovu. Katika ushairi wa Kiswahili pia hali hii inajitokeza katika mashairi teule ambayo tumeyateua kwa utafiti wetu. Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* tunaarifiwa kuwa siku ya kiyama kuna kuulizwa maswali ili mume apate kutoa maamuzi mahali mkewe anastahili kuwekwa:

26. Na siku ufuliwayo,

Nadhari nda mumeyo,

Taulizwa atakayo,

Ndilo takalotendewa.

27. Kipenda wende peponi,

Utapekwa dalihini,

Kinena wende motoni,

Huna budi utatiwa.

Hapa inaonyesha kuwa hata katika mauti mja ana uwezo wa kuamua atakayo. Huyu mume ambaye ataulizwa wapi pa kuweka mkewe alikwishaaga dunia lakini peponi yuko hai. Akiamua mkewe atiwe jehanamu atatiwa; akiamua apelekwe peponi, atapelekwa. Hii inadhihirisha kuwa maisha yangalipo ndani ya mauti, kwa maana anayeweza kuulizwa atakacho ni mtu mwenye uhai na masikio ya kusikia. Kama kifo kingekuwa kinamaliza maisha kabisa basi hakungekuwa na maswali ya kuulizwa. Huu ni uhalisia wa kisanaa maana katika maisha ya kawaida hatumtarajii mfu kupata kunena. Ni uhalisia mazingaombwe. Wakati mwengine katika maisha ya kawaida kuna watu ambao wamewahi kudai kukutana na wapendwa wao ambao waliaga dunia kitambo lakini walirejea kutoa ujumbe kutoka kuzimuni. Haya ni madai ambayo ni magumu kuthibitika kisayansi kwani wafu hao wanaorejea kwa walio hai huja kwa mtu mahususi na ni mtu yuyo huyo aliyerejelewa ndiye ana uwezo wa kuwaona wafu hao ambao huitwa mizimu.

Shairi la ‘Usiniuwe’ katika *Sauti ya Dhiki* linatupatia mazungumzo ya mtoto ambaye hajazaliwa akisihi uhai, mauti na haki kumpa nafasi asije akauliwa. Hali hii inazua utata wa kuelewa ni nani ana uwezo wa kuzungumza; mfu au kiumbe hai. Mazungumzo haya yanaonyesha mkabala wa karibu baina ya uhai na mauti na pia kiumbe. Tunashuhudia haya katika beti zifuatazo:

27. Uhai! Nakuliliya, wewe ndiye upendwaye,

Uhai! Huna ubaya, yupi akutukiyaye?

A! Uhai niombeya, mamaangu sema naye,

Pengine atasikiya, asiniuwe mamangu.

28. *Nawe Haki nisemeya, kwa ya dhati matamshi,*

Sema na kuniombeya, nihururumiwe niishi,

Mamangu anioneya, anioneya bilashi,

A! Haki nihukumiya, asiniuwe mamangu.

29. *Mauti! Nihurumiya, Mauti! ‘Sinitukuwe,*

Lipi nilokukoseya? Hatuna vita mi nawe,

Toba! Nisikitikiya, nisalimisha na wewe,

Magoti nakupigiya, simsikize mamangu.

Mazungumzo haya pia tunashuhudia katika shairi hili lote ambapo mtoto anamsihi mamake asimuue. Hatumwoni mtoto huyu akimsihi Mungu bali anasihi vitu vya kimaumbile kama haki, uhai na mauti kumtetea. Pengine hivi vinavyosihwa vinawakilisha Uungu maana vyote vimeumbwa na Mungu.

4.6.3 Utabaka

Maisha ya mwanadamu duniani yamejengwa katika misingi ya utabaka. Kuna tabaka la juu la watawala na matajiri na tabaka la chini la maskini na watawaliwa. Mila na itikadi za jamii mbalimbali za dunia huonyesha kuwa wanawake wako chini ya mamlaka ya wanaume. Wanawake huonekana kuwa wanyonge ambao kwa vyovyote vile wanatarajiwa kufuata amri ya waume zao. Lakini mafunzo ya dini yanaeleza kuwa pindi tutakapokufa tutakuwa sawa mbele ya

Mungu. Vilevile dini ya Kiislamu inaeleza kuwa siku ya kiyama wanaume bado watakuwa katika daraja ya juu huku wanawake wakiwa katika daraja ya chini. Hali hii ni kinyume cha mtazamo wa Msami (1982) anayeona kifo kama kitu kilicho na katiba ya usawa kwani kinawauwa wote, matajiri kwa maskini, wake kwa waume na wanyonge kwa wenyewe nguvu. Mashairi teule ya Kiswahili yanadhihirisha kuwa hata katika mauti kuna utabaka. Kifo ni tukio ambalo bado linaendeleza yale yaliyokuwepo wakati wa uhai wa mwanadamu maana tunajua kwamba swala la utabaka ni maumbile ya mwanadamu na lina asasi yake kwenye misingi ya uchumi ya wanajamii. Yamkini kuwa hata katika kifo kuna utabaka pia na hivyo kwenda kinyume cha yale asemayo Msami (1982) kuwa kifo husawazisha wanadamu. Wanawake hubaki chini ya mamlaka ya wanaume kama mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* anavyotuambia katika beti zifuatazo:

24. Na awe radhi mumeyo,

Siku zote mkaayo,

Siku mukhitariwayo,

Awe radhi mekuwiya.

25. Na ufapo wewe mbeye,

Radhi yake izengeye,

Wende uitukuziye,

Ndipo upatapo ndiya.

26. Na siku ufuliwayo,

Nadhari nda mumeyo,

*Taulizwa atakayo,
Ndilo takalotendewa.*

*27. Kipenda wende peponi,
Utapekwa dalihini,
Kinena wende motoni,
Huna budi utatiwa.*

Hata katika mauti mume huulizwa wapi pa kupelekwa mkewe. Tatizo kuu ni kuwa endapo huyu mume mwenyewe amehukumiwa adhabu ya moto ilhali mke wake aliishi vema na anafaa aende peponi, atakubali vipi apelekwe peponi naye abaki motoni? Ikiwa alikuwa na kisasi na mkewe, hali itakuwa vipi katika maamuzi atakayotoa? Yaonekana kuwa hata sanaa haisaidii kumkomboa mwanamke dhidi ya udhalilishwaji wa maisha halisi na maisha ya kisanaa. Mwanamke daima anawekwa chini ya mamlaka ya mwanamume.

Timammy (2013) anasema kuwa hoja hii ya mume kuwa na mamlaka juu ya mkewe siku ya kiyama imetiliwa chuku na mtunzi kwani si mafunzo ya Kiislamu na kamwe haingiliani na hali ya Upweke wa Mungu (Allah). Hii ni lugha ya ishara. Kwa kuwa Mwana Kupona alimpenda bintiye sana akaamua kumuusia kutimiza mambo ya kidini na majukumu ya mwanamke kwa mumewe kwa kila njia awezayo. Timammy anazidi kueleza kuwa katika Uislamu maswala ya kidini na kidunia yana maingiliano makubwa, moja hujenga jenzake na jingine hukamilisha jenzake. Mema ya mtu duniani hulipwa kwa rehema ya Allah na kupelekwa peponi.

Mtunzi wa *Inkishafi* naye anadhihirisha kuwa wale ambao walikuwa wakwasi na watawala, katika kifo wanapata adhabu kupindukia kwani nyumba zao nzuri walizokuwa wanakalia sasa zimeshukia daraja ya chini:

45. Sasa walaliye mji shubiri,

Pasipo zulyia wala jodori,

Ikawa miwili kutaathari,

Dhiki ya kaburi iwakusiye.

46. Zitukuta zao hutawanyika,

Usaha na damu hawa itika,

Pua na makanwa bombwe hushuka,

Haiba na sura zigeushiye.

47. Wasiriye wote kula kwa dudi,

Na kuwatafuna zao jisadi,

Na mtwa na tungu huwafisidi,

Na nyoka na nge wawatatiye.

Ni kana kwamba waliolewa katika anasa za dunia pamoja na milki yao ya kidunia, siku ya kufa kwao watashukia mali yao ikipotea ghafla. Wingi wa mali unakuwa chanzo cha wingi wa maovu. Katika Biblia tunaambiwa kuwa ni rahisi kwa ngamia kuingia kwenye tundu la sindano kuliko tajiri kuingia mbinguni. Utajiri huja na kiburi na udhalimu na ndiyo maana unashutumiwa kuwa ni njia ya kuingia motoni. Matajiri waliozoea kula anasa duniani, siku ya kufa kwao watapatwa na uchungu huku mazuri na matamu waliyozoea yakigeuka kuwa shubiri.

Watataabika kaburini kwa dhiki kuu pasina afueni yoyote. Wakwasi waliokuwa katika tabaka la juu sasa wameshushwa hadhi katika mauti na wanapata mateso kupindukia kiasi cha kupambana na nyoka, ‘*Na nyoka na nge wawatatiye*’.

4.6.4 Mwanzo na mwisho wa maisha

Swali la ni lini maisha huanza na wapi huisha limemtatiza mwanadamu kwa muda mrefu. Hili swalii bado litamtatiza mwanadamu kwa muda mrefu zaidi. Hata katiba nyingi za mataifa mbalimbali duniani hukumbwa na shida ya kutetea maisha ya watu na haki zao. Swala la uavyaji mimba hukumbwa na mirengo miwili ya kuliunga na kulipinga. Wanaoliunga mkono swala la uavyaji mimba hudai kuwa wakati mwingine mwanamke ameshika mimba kwa kunajisiwa au bila kuipangia na hivyo anafaa kuruhusiwa kuitoa mimba hiyo ili apate uhuru katika nafsi yake. Wanasyansi nao huangalia kuavya mimba kuwa endapo ile mimba huweza kumtatiza mwanamke kiafya basi anafaa apewe nafasi ya kuitoa ili ajinusuru maisha na afya yake. Lakini kuna upande ambao unashikilia kuwa kuavya mimba ni kinyume cha haki ya binadamu kwani kunamnyima yule mtoto asiye na hatia nafasi ya kuishi kama wanadamu wengine. Vilevile wanaonelea kuwa kule kuavya mimba ni kuua roho changa na huko ni kwenda kinyume na maadili ya dini ambazo hufunza kuwa kuua ni dhambi. Tatizo ni kubaini ni lini maisha huanza tumboni mwa mama na kumwezesha yule mtoto kuhisi chochote. Mtunzi wa ‘Usiniuwe’ katika *Sauti ya Dhiki* anatupatia picha ya mtoto ambaye yuko katika mjadala na mamake huku akimsihi asimuue, ampe nafasi aishi kama wengine duniani:

15. Ngoja! Usinisongowe, niweka mama niweka,

Niweka hadi nikuwe, halafu ndipo ‘tatoka,

*Kama hunitaki wewe, ulimwengu wanitaka,
Mwanayo usiniuwe, mamangu nihurumiya.*

16. Kama hunitaki mama, piya waniuliyani?

*Nakuomba nikisema: usiniuwe tumboni,
Mama nizaa salama, kisha nitupa ndiyani,
Mja alo na huruma, an'okote kunileya.*

Kauli za ‘*Ngoja! Usinisongowe, Niweka hadi nikuwe*’, na ‘*usiniuwe tumboni*’ zinasisitiza dhati ya huyu mtoto tumboni kuhisi kuwa uavyaji mimba ni ukatili na hivyo hafai kuuawa kabla ya kuishi. Tunamwona yu tumboni lakini anao uwezo wa kuhisi kifo. Kifo kina nafasi ya kuua hata kiumbe ambaye hajazaliwa na kupata kuishi! Mtunzi huyu anatujengea taswira ya kutisha ya kifo hata kwa kiumbe ambaye bado hajazaliwa. Kifo kinaweza kuhisika hata na mtoto tumboni mwa mamake. Tunashindwa kujua ni jinsi gani mtoto huyu ambaye hajazaliwa ana uwezo wa kuhisi tishio la kifo. Maisha ni kama yanaanza mapema hata kabla ya kiumbe ‘kuishi’. Katika Biblia kitabu cha Jeremia 1:4 Jeremia anasema kuwa ‘Neno la Mungu lilinijia, likiniambia, kabla nikuweke tumboni mwa mamako, nilikujua, na kabla ya kutoka tumboni mwa mamako, nilishakuchagua uwe mtume wangu.’ Katika kitabu cha Mwanzo, tunaelezwa kuwa hapo mwanzo kulikuwa na neno na neno lilikuwa na Mungu na vitu vyote vilumbwa kutokana na yeye. Hivyo basi inakuwa muhali kung’amua lini na wapi maisha huanza kwa mwanadamu. Baada ya kuishi kuna kifo na chochote kilichoumbwa na kupewa uhai kitakufa pia. Baada ya kufa kuna ufufuo wa wafu. Kama tunavyoona katika *Utenzi wa Mwana Kupona* akimkumbusha bintiye maisha kule peponi:

26. Na siku ufuliwayo,

Nadhari nda mumeyo,

Taulizwa atakayo,

Ndilo takalotendewa.

Wafu watafufuliwa na kila mmoja atapata kuishi upya. Hayo maisha baada ya kufufuliwa ndiyo hatuyajui yanaishia wapi. Wale tuambiwalo kuwa watatiwa motoni, watacaa huko milele na katika hali gani? Mashairi ya teule ya Kiswahili kama mafunzo ya dini za Kiislamu na Kikristo yanakosa kutuonyesha haya maisha baada ya kufa jinsi yalivyo. Tunaambiwa tu kuwa wema wataishi peponi milele huku waovu wakiadhibiwa motoni milele. Hivyo basi mwanadamu anabaki katika hali ya matarajio ya kuishi milele bila kujua ni kwa namna gani.

4.6.6 Hitimisho

Sehemu hii imeshughulikia muhtasari wa waandishi wa mashairi teule tuliyotafitia. Imebainika kuwa maandishi haya ni chimbuko asilia na halisi katika matukio na mazingira ya waandishi hao walioathiriwa na mazingira yao katika kulizungumzia swala la kifo. Uwasilishaji wa kifo katika tungo hizi umetupatia sura anuwai ya kifo. Kifo huonekana kama tukio la kutisha, la kutamausha, humkumba kila kiumbe, hakibagui, kina upweke na sio mwisho wa maisha. Halikadhalika mazingira ya mtunzi humsaidia katika usawiri wa kazi yake. Mawanda mapana ya mazingira yamejitokeza katika wakati, dini au utamaduni na lugha.

Tumeangalia pia visababishi vya kifo na tukabaini kuwa ni vitatu; Mungu, shetani na mtu (binadamu mwenyewe). Imebainika kuwa binadamu yuko radhi kumuua mwenzake ili apate

heshima. Mauaji haya huweza kuwa kwa nia ya kuhifadhi jina au kutokana na misukumo ya jamii. Vilevile katika sura hii tumejadili utata unaoibuka katika uwasilishaji wa dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Utata huu upo katika ufasiri wa adhabu na kuzawadiwa peponi, mazungumzo na Mungu, utabaka na mwanzo na mwisho wa maisha.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa tasnifu nzima kwa kuangazia yote ambayo tumeshughulikia katika utafiti huu. Tumetoa taamuli kuhusiana na madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti na nadharia ambayo tulijumuisha ili kutupatia mwongozo mzima wa kuangazia vipengee vyote vya utafiti wetu kwa kina kinachofaa. Tumeonyesha matokeo ya utafiti wetu ili kuthibitisha kama tumeyafikia madhumuni yetu. Halikadhalika tumetoa mapendekezo ambayo kutokana na utafiti wetu huu tunataraji yatawafaa watafiti wa usoni watakaoshughulikia dhana ya kifo na dhana nyinginezo katika ushairi na fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

5.1 Muhtasari wa tasnifu

Utafiti wetu ulidhamiria kuchanganua uwasilishaji wa dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchanganua taswira ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili, visababishi vya kifo na utata wa fasiri ya dhana ya kifo kama ilivyowasilishwa katika mashairi teule ya Kiswahili. Imebainika wazi kuwa swala la kifo katika mashairi teule ya Kiswahili lina taswira mbalimbali na pia hudokeza utata wa hali ya juu katika ufasiri wake. Ili kuibuka na matokeo ya utafiti huu, tulitumia nadharia ya uhalsia huku tukiegemeza utafiti wetu katika misingi ya nadharia hii ambayo ni pamoja na historia ya jamii, tajriba ya mwandishi, vielelezo, lugha na muundo wa kazi ya sanaa.

Sura ya kwanza imedokeza kuwa swala la kifo halijajadiliwa kwa kina katika tafiti mbalimbali za ushairi wa Kiswahili. Tuliteua tenzi mbili na shairi moja ambalo tulitumia katika kupata data

mwafaka za utafiti wetu. Uteuzi wetu ulikuwa wa kimakusudi kwa kuzingatia uwepo wa kifo katika kazi hizo na upana wa kujitokeza kwake. Vilevile tuliyateua mashairi yetu kwa kuona kuwa yana urasimi na lugha pevu ambayo imetumika katika kuwasilisha kifo.

Sura ya pili imeangazia mapitio ya maandishi kuhusu dhana ya kifo. Kutokana na maoni ya wataalamu mbalimbali, tulipata kuona mianya katika utafiti wa ushairi wa Kiswahili kuhusiana na dhana ya kifo. Tuligundua kuwa kifo ni swala ambalo limejitokeza katika fasihi za kiulimwengu katika tanzu zote za fasihi. Watafiti wengi wamelishughulikia swala la kifo katika mashairi simulizi ya jamii mbalimbali lakini katika ushairi andishi swala hili hutajwa tu kwa ujumla, hususan ushairi wa Kiswahili. Sura hii imeshughulikia ufasiri wa dhana ya kifo huku ikionyesha maoni ya wataalamu kuhusu chanzo cha kifo, ukweli na ukubalifu wa kifo mionganii mwa wanajamii na mjadala wa kifo katika ushairi wa Kiswahili. Ilibainika kuwa kuna fasiri kadha wa kadha kuhusu kifo kwa kutegemea taaluma mbalimbali kama vile dini, sayansi, sosholojia na uwanja wa fasihi. Pia ukweli wa kifo katika fasihi huonyesha uhalisia wa kimaisha mionganii mwa wanajamii. Kifo ni tukio la kihalisia na humkumba kila kiumbe wakati wake ukifika. Licha ya kuwepo kwake bado mwanadamu hasadiki kuwa kifo ni mwisho wa maisha. Mwanadamu huishi kwa matumaini ya maisha mazuri na ya milele kesho ahera. Dhana ya kifo kwa hivyo hubaki kuwa tata kuhusiana na mwanzo na mwisho wake.

Sura ya tatu imeshughulikia njia na mbinu za utafiti pamoja na muundo wa utafiti. Muundo uliotumika ni wa kimaelezo. Muundo huu ulitusaidia kujibu maswali ya lini, wapi na nani, kuhusiana na tukio la kifo kama walivyosawiri watunzi wa mashairi teule ya Kiswahili. Data zote zilikusanywa kupitia njia ya maktaba. Mtafiti aliteua matini tatu za ushairi wa Kiswahili na

kujikita maktabani na kuzichambua kwa kina huku akirejelea malengo ya utafiti. Uchanganuzi ulijumuisha ufanuzi na matumizi ya majedwali ili kuweka wazi fasiri ya taswira ya kifo, visababishi vyake na utata unaoibuka kuhusiana na dhana ya kifo katika mashairi teule ya Kiswahili.

Sura ya nne nayo imejikita katika uchambuzi wa data za utafiti ili kuonyesha taswira ya kifo pamoja na visababishi vyakiofia kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Tuligundua taswira anuwai za kifo ambazo zinajitokeza katika mashairi teule ya Kiswahili. Ili kugundua taswira hizo, tulitegemea matumizi ya misamiati katika uwasilishaji wa hisia na mandhari ya usimulizi. Illobainika kuwa kifo ni kitu katili, kinatamausha, humkumba kila kiumbe, hakibagui, kina upweke na sio mwisho wa maisha. Taswira hizi ni changamano na hivyo huibua utata katika ufasiri wa dhana ya kifo. Vilevile tuligundua kuwa mazingira ya mtunzi huchangia namna anavyowasilisha mada yake. Mazingira ya mtunzi hujumuisha vipengee vyakiofia wakati, dini au utamaduni, na lugha. Pia sura hii imejadili utata unaoijitokeza katika uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Utata huu tumegundua kuwa hujitokeza kwa namna ifuatayo: adhabu na kuzawadiwa peponi, mazungumzo na Mungu, utabaka na mwanzo na mwisho wa maisha. Pia tumejadili visababishi vyakiofia ambavyo tulibaini kuwa ni Mungu, shetani na mta kwa mta.

Utafiti huu uliegemezwa katika nadharia ya uhalsia. Vipengee vyakiofia nadharia hii kama vile historia ya jamii, tajriba ya msanii, lugha, vielelezo na muundo vimetumika. Kupitia kipengee cha historia na tajriba ya mwandishi tuliweza kubaini jinsi mazingira na matukio ya kimaisha zinavyoingiliana. Tukio la kuanguka kwa mji wa Pate ambao ulikuwa maarufu mwambao wa

Afrika Mashariki lilimchochea mtunzi wa *Inkishafi* kusawiri dhana ya kifo kikamilifu. Kifo kikachorwa kama tukio ambalo lipo na litamkumba kila kiumbe hai maana dunia ni mapito tu kwa mwanadamu. Kipengee cha lugha nacho kilijidhihirisha katika uteuzi wa vina faafu ili kusawiri kifo kwa namna inayoibua hisia za kutamauka mbele ya kifo. Waaidha, vielelezo kupitia uteuzi wa msamiati vilitupatia uwezo wa kufasiri utata wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Muundo wa utenzi uliotumika katika tenzi mbili za *Inkishafi* na *Utenzi wa Mwana Kupona* ulituchorea mawanda mapana ya kifo kupitia maisha duniani na kesho ahera kwa kusimuliwa kwa urefu unaofaa.

5.2 Taamuli

Utafiti huu ulilenga kuchanganua uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili. Ili kufikia lengo hili tulizingatia madhumuni mahususi ambayo ni pamoja na kubaini taswira ya kifo, kutambua visababishi vyta kifo na kuonyesha utata unaoibuka katika uwasilishaji wa dhana ya kifo katika mashairi teule Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa taswira ya kifo ina sura mbalimbali katika mashairi teule Kiswahili. Kifo husawiriwa kama tukio la kutamausha, kitu katili, humkumba kila kiumbe bila ubaguzi wowote na si mwisho wa maisha. Taswira hizi zimebainishwa kupitia mazingira ya mwandishi ambayo yanaathiri mkondo wa utunzi wake. Pakubwa mazingira ya Kiislamu ya watunzi hawa yamechangia kwao kuwasilisha kifo kwa kuegemea misingi ya dini ya Kiislamu. Wameonyesha kuwa kifo ni tukio la kimaisha na humkumba kila kiumbe lakini si bayana ni wakati upi kifo huja kumchukua kiumbe. Mazingira ya jela aliyotumia mtunzi wa shairi la ‘Usiniuwe’ katika *Sauti ya Dhiki* yamemsaidia kuonyesha hofu ya kuuliwa na watawala. Kupitia

mtoto aliye tumboni mwa mamake, tunapata taswira ya unyonge mbele ya mamlaka yenyewe nguvu lakini iliyojaa ukatili mwangi. Unyonge wa mtoto huyu huonyesha kutamauka kwa mwanadamu mbele ya mauti na upungufu wa uwezo wake kukwepa kuuawa na kifo.

Ili kuvielewa visababishi vyakiofia kifo katika jamii, nadharia ya uhalisia katika vipengee vyake vyatajriba ya mwandishi na historia ya jamii ilitumika. Tuligundua kuwa mafunzo ya kidini na imani za jamii huelekeza fikra za watanzi kufasiri visababishi vyakiofia kifo kwa njia nyingi. Visababishi vyakiofia vilivyojitokeza ni pamoja na Mungu, shetani na mtu kwa mtu. Mungu amesawiriwa kama mwenye nguvu na mamlaka juu ya kifo. Siku ya kiyama Mungu atawapa watu hukumu kuhusiana na matendo yao huku watu wema wakienda peponi na wabaya wakipelekwa jehanamu iliyio na moto wa milele. Shetani kwa upande mwengine amechorwa kama katili na asiye na huruma. Ameonyeshwa kama mwasi wa Mungu na kila mara anatia juhudhi ili kupotosha viumbe na kwa njia hiyo husababisha kuangamia kwao. Kunao pia watu ambao huwaua wenzao. Kupitia taswira ya mtoto tumboni mwa mamake katika shairi la ‘Usiniuwe’ katika *Sauti ya Dhiki* mtunzi huyu anatuonyesha kuwa mama wa mtoto huyu ana dhamira ya kumwavya mwanawe hali ambayo itasababisha kifo chake kwa kuwa siku zake za kuzaliwa hazijatimia. Tajriba ya mtunzi huyu katika maisha ya kifungo na historia ya jamii yake ambayo ilisheheni utawala mbovu zinamfanya ajiwasilishe kama mtoto akisihi asiuawe.

Swala la kifo ni tata. Utata huu hujitokeza katika kuelewa mwanzo na mwisho wa maisha, maisha baada ya kifo, na uwezo wa kuzungumza na Mungu katika ufu.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu unabaini kuwa kuna maandalizi anayokuwa nayo mwanadamu katika hatua ya kukabiliana na mauti. Maandalizi hayo hujumuisha vitu kama vile wosia, toba na maelekezo kwa moyo ili nafsi ya mwanadamu isije ikaangamia. Japo kifo ni tukio la kutamausha mwanadamu haishi tamaa ya kuishi duniani leo wala kesho kule ahera.

Utafiti huu pia umechangia kuziba mwanya wa tafiti za awali ambazo zilishughulikia kifo kwa kikitaja juujuu kama tulivyodokeza katika mapitio ya maandishi. Wataalamu mbalimbali walioishughulikia dhana ya kifo wameipa umuhimu mkubwa katika ushairi simulizi wa jamii mbalimbali huku ushairi andishi ukitafitiwa kwa ufinyu. Utafiti wetu ni mchango kiasi katika uwanja wa ushairi andishi ambao umetafitia kifo kwa kina kwa kuziteua tenzi mbili na shairi moja kama kiwakilishi cha jamii nzima ya ushairi wa Kiswahili.

Kifo ni swala halisia katika maisha ya mwanadamu. Wakati wa kifo watu huwa na huzuni na masikitiko makuu. Hali ya kutamauka hushika kani huku mwanadamu akiangalia utamu wa maisha na ufupi wake. Uhalsia huu huweza kumulikwa kifasihi kama tulivyofanya kwa kurejelea mashairi teule ya Kiswahili. Kifo hakiwezi kupuuzwa katika maisha ya mwanadamu. Wanaoishi daima watazungumzia vifo vyta wenza au kifo chao. Wataonekana wenye hofu au ukakamavu ili wakabiliane na mauti.

Ni mapendekezo ya utafiti huu kuwa kifo ni kiungo cha maisha kinachofanya uhai kuthaminiwa zaidi. Uwepo wa kifo hupatia maisha maana na ukosefu wake huyafanya kukosa kufasiriwa. Kutokana na utata wa dhana ya kifo, ni muhiimu:

- 1) Utafiti zaidi ufanyike kwa kuzingatia dhana ya uhai ili kuweka mwangaza zaidi kuhusu mpaka baina ya kifo na uhai na chanzo cha kifo.
- 2) Utafiti huu unaweza kuwa msingi mzuri kwa utafiti mpana kuhusu mada hii, au utafiti linganishi wa kifo katika ushairi na tanzu nyinginezo za fasihi ili kubainisha nyenzo za uwasilishaji wake katika kuibua taswira anuwai za kifo.

5.4 Hitimisho

Utafiti wetu ulidhamiria kuchanganua uwasillishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili ili kuonyesha kuwa hili ni swala nyeti la kifasihi na kihalisia ambalo halipaswi kupuuzwa. Kwa kutumia nadharia ya uhalisia tumebaini kuwa kifo kipo na wanajamii wana mitazamo tofauti tofauti kukihusu katika mikondo ya visababishi vyake na taswira yake. Mashairi teule ya Kiswahili yanaonyesha kuwa wanajamii hawatazami kifo kama mwisho wa maisha bali wanakiona kama hatua ya mapito kutoka duniani ambayo si makao ya kudumu hadi ahera ambako kuna kuishi daima dawamu.

MAREJELEO

- Abedi, S. A. K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.
- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Oxford. Oxford University Press.
- Abdulaziz. M. H. (1979). *Muyaka: The 19th century Swahili Poetry*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.
- Addinall, P. (1991). *Philosophy and Biblical Interpretation: A Study in the Nineteenth Century Conflict*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Akivaga, S. K. and Odaga, A. B. (1982): *Oral Literature: A School Certificate Course*. Nairobi. Longman.
- Alembi, E. (2001): *Reconstruction of the Abanyole Perceptions of Death through Oral Funeral Poetry*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Helsinki.
- Ali, S. A. (1980). *Inkishafi*. (Mh. Mlamali, M). Nairobi. Longman.
- Arege, T. (Mh). (2013). *Tunu ya Ushairi*. Nairobi. Oxford.
- Beidelman, T. (1963). Witchcraft among the Kaguru katika Witchcraft and Sorcery in East Africa. London.
- Birsch, D. (2000). *Philosophical Issues: a brief introduction*. New York: McGraw – Hill.
- Carnley, P. (1997). *The Structure of Resurrection Belief*. Oxford: Oxford University Press.
- Caudwell, C. (1947). *Illusion and Reality: A Study of the Sources of Poetry*. New York: International Publishers Co.
- Charity, A. C. (1966). *Events and Their Afterlife: The Dialects of Christian Typology in the Bible and Dante*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Chimerah, R. & K, Njogu (1998). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Longhorn.

- Chiraghdin, S. (1971). (Mhr). *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh Bhalo*. Nairobi: Oxford University Press.
- Chomsky, N. (1990). “Language and Mind” katika: Mellor, D. H. (Mhr): *Ways of Communicating*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Cuddon, J. A. (1979). *A Dictionary of Literary Terms*. London. Penguin Books Ltd.
- Despelder, A. L & A. L, Stickland (1998). *The last dance: Encountering Death and Dying*. California. Mayfield Publishing Company.
- Evans- Pritchard, E. E. (1976): *Witchcraft, Oracles and Magic Among the Azande*. London. Oxford University Press.
- Finnegan, R. (1970): *Oral Literature in Africa*. London. Oxford.
- Gehman, R. (1999): *Who are the Living Dead? A Theology of Death, Life After Death and the Living Dead*. Nairobi. Longman.
- Gibbe, A. G. (1990). *Al-Inkishafi: Chemchemi na Kilele cha Ushairi wa Kiswahili*. Chuo Kikuu cha Moi: Idara ya Kiswahili.
- Giddens, A. (1990). *Sociology*. Cambridge: Polity Press.
- Gikandi, S. (1987). *Reading the African Novel*. Nairobi: Heinmann Kenya Limited.
- Habwe, J; Mattei, A & Nyonje, N. (2010). *Darubini ya Isimujamii*. Nairobi: Phoenix.
- Halliday, M. A. K. & R. Hassan. (1985): *Language, Context and Text: Aspects of Language in a Social Semiotic Perspective*. Oxford: Oxford University Press.
- Hawthorn, J. (1985). *Studying the Novel: An Introduction*. London. Edward Arnold – A division of Hodder & Stoughton.
- Heidegger, M. (1962). *Being and Time*, tr. Macquarrie, J & Robinson, E. San Francisco: Harper & Row.

- Hussein, E. N. (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim*. Oxford.
- Jahadhmy, A. A. (1993). *Kusanyiko la Mashairi: Anthology of Swahili Poetry*. Nairobi. E. A. E. P. L.
- Kastenbaum, R. (1975). "Is death a life crises? On confrontation with death in theory and practice". In N. Datan and L.H. Ginsberg (wah) *Life span developmental psychology normative life crises*. New York: Macmillan.
- Kelly, H. A. (2006). *Satan: A Biography*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Kenny, A. (1979). *The God of the Philosophers*. Oxford: Oxford University Press.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.
- (1983). "Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili " katika *Makala ya Semina za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Khatib, M. S. (1982). *Utenzi wa Pambazuko la Afrika*. Arusha. East Africa Publications Limited.
- Khatib, M. S. (1985). "Uhakiki wa Mapitio ya vitabu: Utenzi wa Mwanakupona" katika *MULIKA 17*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kimmel, D. L. (1980). *Adulthood and aging: An interdisciplinary development view*. (2nd ed.) New York: John Wiley and Sons.
- King'ei, K & Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Kombo, D. K. & Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kough, M.I. (2001). *The art of witchcraft and burial rituals among the Tiv: The Christian effect*. Makurdi: Onaivi Printing & Publishing Co. Ltd.
- Krathwohl, D. R. (1993). *Methods of Educational and Social Science Research: An Integrated Approach*. New York: Longman.

- Louden, R. B. (1992). *Morality and Moral Theory: A reappraisal and reaffirmation*. Oxford: Oxford University Press.
- Lukacs, G. (1938). ‘Realism in the Balance’ in *The Norton Anthology of Theory and Criticism*, L. V. B. (2001). Norton. New York.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam. Mture Educational Publisher Ltd.
- Madumulla, J. S. & Khamis, A. M. (Wah). (1989). *MULIKA 21*. Dar es Salaam: TUKI.
- Macmillan. (2002). *Macmillan English Dictionary*. Oxford: Macmillan.
- Maganga, M. A. (1971). “Maisha ya Shaaban Robert na Mawazo Yake” katika *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*. Oxford: Oxford University Press.
- McOnyango, O. O. (1995). “Kutathmini Kutukuka kwa Muyaka” katika *Baragumu*. Chuo Kikuu Kishiriki - Maseno.
- Massamba, D. P. B. (1983). “Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili” katika *Makala za Semina ya Kiswahili ya waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mayoka, J. M. (1984). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Marketing Co. LTD.
- Mbiti, J. S. (1969). *African Religions and Philosophy*. Nairobi: Heinemann.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longhorn.
- Mlamali, (1980). *Ikisiri ya Inkishafi*. Nairobi: Longman.

- M' Ngaruthi, T. K. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
- Mnyampala, E. M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mohamed, S. A. (1980). *Dunia Mti Mkavu*. Nairobi: Longhorn.
- (1988). *Kiza Katika Nuru*. Nairobi: Oxford University.
- (1995). *Amezidi*. Nairobi. Oxford University Press.
- Mohamed, M. (1977). *Malenga wa Mrima*. Nairobi: Oxford University Press.
- Morwood, J. (1996). *Through Death's Gate*. Centre for Sacred Sciences.
- Msami, H. (Mh). (1982). *Malenga wa Vumba*. Nairobi: Oxford University Press.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mugambi, J. & N. Kirima. (1976). *The African Religious Heritage*. Nairobi. Oxford University Press.
- Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatuz za Kale*. Dar es Salaam. TUKI.
- Mulokozi, M. M & K. K. Kahigi. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mukuria, D. M. (2001). "Making Kiswahili a True National Language of Kenya." *Katika Shitemi, N. na wengine (wah)*. *Kiswahili a Tool for Development: The Multidisciplinary Approach*. Eldoret: Moi University Press.
- Muriasi, M. (2013). *Guide to The River and the Source*. Kakamega: Lurambi Publishers.
- Mwanje, I.J. (2001). *Qualitative Research Process: Social Science Research Methodology Series, Module 2*. Addis Ababa: OSSREA
- Nabhany, A. S. (1971). *Utenzi wa Mwanakupona*. Nairobi. Oxford University Press.
- Nandwa, J. (1976): *Oral Literature Among the Abaluhya*. M. A. Thesis. University of Nairobi.

- Nanyama, W. D. (2005). '*Mtoto wa Kike katika Riwaya ya Kiswahili*'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Maseno.
- Nassir, J. (1971). *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh Bhalo*. Nairobi: Oxford University Press.
- Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Njozi, H. M. (1992). "Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics" katika *Baragumu*. Chuo Kikuu Kishiriki – Maseno.
- Nochlin, L. (1971). "Realism." New York. Penguin Books.
- Okombo, O. (1983). *Masira Kindaki*. Nairobi: Mawazo Publications.
- Ogola, M. (1996). The River and The Source. Nairobi: Focus Publishers.
- P'Bitek, O. (1963): 'Concept of Jok Among the Acholi and Lango'. In: *Uganda Journal Vol. 27*.
- Rinpoche, L. Z. (2011). *Life, Death and After Death*. Boston: Boston Press.
- Robert, S. (1967). *Wasifu wa Siti binti Saad*. Nairobi: Nelson.
- Ruo, K. R. (1988). "Suala la Ushairi wa Kiswahili" katika *Makala ya Semina ya kimataifa ya Uandishi wa Kiswahili III: Fasihi*. Dar es Salaam. TUKI.
- Russeu, B. (1979). *History of Western Philosophy*. London: Unwinbacks.
- Shariff, I. N. (1988). *Tungo Zetu: Msingi wa Mashairi na Tungo Nyinginezo*. New Jersey: The Red Sea Press.
- Shorter, A. J. (1973). *African Culture and the Christian Church: An Introduction to social and Pastoral Anthropology*. London: Geoffrey Chapman Publishers.
- Simpson, J. A & Weiner, E. S. C. (1989). *The Oxford English Dictionary*. 2nd Ed. Vol. IV. London: Oxford University Press.

Sivananda S. S. (1997). *What Becomes of the Soul after Death?* Himalayas. The Divine Life Trust Society.

Stomberg, R. N. (1968): *Realism, Naturalism and Symbolism: Models of Thought and Expression in Europe 1848-1914*. New York: Walker and Company.

Timammy, R. na A. Swaleh (2013). ‘A Thematic Analysis of Utenzi wa Mwanakupona: A Swahili/Islamic Perspective’ katika *International Journal for Innovation Education and Research*. Vol. 1-03, 2013.

Truex, D. (1996). *Text-based Analysis: A Brief Introduction*. Imesomwa Januari 2011
<http://www.cis.gsu.edu/~dtruex/Presentations/tbintppr.pdf>

Topan, F. (Mh). (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinmann.

TUKI. (2006). *English-Swahili Dictionary*. 3rd Ed. Dar es Salaam: TUKI.

Turuka, U. H. A. (1971). “Yasemayo Mashairi” katika *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*. Oxford: Oxford University Press.

Vuzo, A. M. (1999). Mwongozo wa Siku Njema. Nairobi: Macmillan Publishers.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M & K. Njogu. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Longhorn.

Walibora, K. (1996). Siku Njema. Nairobi. Longhorn.

Wallah, W. (1988). *Malenga wa Ziwa Kuu*. Nairobi: Heinmann.

Wamitila, K. W. (2001). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix.

Wamitila, K. W. (2002). *Kichocheo cha Fasihi*. Nairobi. Longhorn.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamus ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications.